ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.

14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini

32. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
33. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
34 .Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani

55.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

57.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

58. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

62.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

63.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

65.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

66.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

67.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

68.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

69.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndg. Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Sita – Tarehe 4 Aprili, 2012

(Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (*Pandu Ameir Kificho)* alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Hati Mezani, Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 122

Mashimo Katika Kituo Cha Daladala Darajani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Pamoja na kazi kubwa ya kuweka lami na kuweka mpangilio mzuri wa gari kwenye Kituo cha gari za daladala Darajani, kuna maeneo ambayo yameanza kuchimbika na kuweka mashimo.

Mhe. Waziri, Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuyafanyia matengenezo maeneo yaliyoharibika kabla ya mvua za masika kuanza.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu:

Mhe.Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe.Mwakilishi swali lake namba 122 kama ifuatavyo:-

Mhe.Spika, nakubaliana na Mheshimiwa kwamba lami kwenye kituo cha barabara, eneo la kituo cha Daladala kidogo imeanza kuharibika mbele na nyuma kweli kuna mashimo mengine. Lakini kama amepita sehemu hiyo ameona kwamba tumeanza kazi kwa kushirikiana na mfuko wa barabara na baadhi ya wafadhili wanaoishi mitaa ile ambao tunawashukuru sana, tumeanza kujaza fusi na Ishaallah tumepangana na wenzetu wa Mfuko wa barabara tuweze hata kuitia lami barabara ile.

Kwa hiyo tunakiri kwamba barabara ina matatizo, lakini Serikali imeliona kwa hiyo tunajitahidi kuiziba ili iweze kupitika kabla ya mvua za masika kuchanganya ili kazi iwe nzuri ipasavyo.Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mhe.Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa katika eneo hilo la daladala kumeibuka kuna watu wamekuwa wakichimba dawa (kujisaidia) katika miti ya kati kati ya kituo cha daladala, na kuchafua hali ya hewa ya mazingira ya pale. Je, Serikali ina mpango gani kuweka ulinzi katika eneo lile.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Ni kweli mazingira yalivyo pale Darajani wenzetu wanaofanya biashara pale huwa wana utaratibu usioridhisha, wala usiotakiwa kwenda pembezoni mwa bustani na kujisaidia. Tena ajabu kwamba choo kipo karibu pale hata mita mia tatu hazitimii, na choo kile kinatunzwa, tumemuweka muwekezaji kakitengeneza na kipo safi.

Kwa hiyo labda ningetoa wito kwa wafanyabiashara waliokuwepo pale wote, na watumiaji wa njia ile basi wakitumie choo kile. Tunahimizwa kuhusiana na maradhi ya kuambukiza kujihadhari na uchafu katika mji wetu. Moja ni juu ya ustaarabu wa kutumia choo. Choo Darajani kipo na kipo safi kabisa. Kwa hivyo mimi ningetoa wito wenzetu wajitahidi kukitumia choo kile.

Pili naomba Mhe. Spika, wale wafanyabiashara waliokuwepo pale ambao hawaruhusiki kuwepo katika Skuli ya Vikokotoni, wanaweka biashara zao mpaka katika uzio wa skuli ya Vikokotoni. Lile sio eneo la biashara, biashara tumewawekea Saateni waende, hilo naliomba ni ombi maalum kwa wale wafanyabiashara wanaotundika.Kufanya biashara mbele ya Skuli ya Vikokotoni si mahali pake.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa pamoja na kuhimiza usafi wa mazingira. Lakini Mhe. Spika, katika kituo cha Darajani ambacho ni kituo kikubwa sana kabisa pana jaa la kudumu, haliondoki na sasa hivi takataka zilizokuwepo pale zinatoa harafu mpaka ukipita barabara kuu. Haoni kuwa Mheshimiwa pamoja ya kuwa anasisitiza kwenye vyoo, lakini na lile jaa lina hatari zaidi na linahitaji kuondolewa moja kwa moja.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, lile jaa kwa sababu soko lolote ni lazima pawe na mahali ambapo taka zinakusanywa. Sasa pale jaa lilipo yaani soko lote lile kubwa la Darajani taka zinakusanywa pale. Tatizo kwamba, kweli nakiri kwamba tunachelewa kuziondoa. Hilo tutajitahidi Baraza la Manispaa kwamba taka zisikae zaidi ya kutwa moja, tufanye kutwa ziondolewe asubuhi na jioni au mchana ili zisilale kuweka mji wetu katika hali ya haiba nzuri.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha katika siku hii ya leo kuamka katika hali ya afya.

Kwa kuwa vyoo ni kitu muhimu kwa binaadamu. Na kwa kuwa eneo la Darajani ni eneo ambalo ndio Waunguja wote, na Wazanzibari wote utawakuta katika eneo lile. Je, hakuna haja ya kuona Mhe. Waziri sasa hivi kwamba tubadilike tuongeze vyoo, na kwenye vyoo hivyo tuweke watu ambao wataweza kutoza malipo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, mimi nakubaliana naye moja kwa moja ushauri wake alioutoa ni sahihi kabisa kwamba tuongeze vyoo, tuvitumie na tutajitahidi kuviweka katika hali ya usafi. Na ni lazima nikiri kwamba kuna baadhi ya vyoo kwa sababu labda nyenginezo tu baada ya kuwa vyoo vimegeuzwa matumizi mengine. Sasa hivyo vyote sasa hivi, wizara yangu imejitahidi kurekebisha hali hiyo na tutavirudisha kuwa vyoo kwa matumizi ya wananchi wetu. Ahsante.

Nam. 148

Uimarishaji wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Aliuliza:

Kikosi cha Zimamoto na Uokozi ni muhimu sana katika kutoa huduma za Uokozi katika jamii yetu, lakini kutokana na Serikali kutokiwezesha ipasavyo, kimekuwa na matatizo mengi yanayowatanza katika utekelezaji wa majukumu yao.

(a) Mhe. Waziri, Je, Kikosi hicho kinamiliki gari ngapi za kuzimia moto, Unguja na Pemba.

(b) Ni gari ngapi kati ya hizo bado zinafanya kazi na ni ngapi zimeshakuwa mbovu.

(c) Je, kikosi kinamiliki gari ngapi za kubeba majeruhi wa majanga ya moto (Ambulance), Unguja na Pemba.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi -Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 148 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kinamiliki jumla ya gari 20 Unguja na Pemba, kati ya hizo, gari saba(7) zipo Mjini Unguja, nne(4) zipo Uwanja wa ndege Unguja, mbili (2) Kitogani Mkoa wa Kusini Unguja, mbili (2) zipo Kigunda Mkoa wa Kaskazini Unguja, mbili (2) zipo Chanjaani Pemba, mbili (2) zipo Uwanja wa Ndege wa Karume Pemba na moja (1) ipo Mahonda. Aidha, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kina mpango wa kupata gari nyengine tatu (3) za kuzima moto na mbili (2) za kubebea wagonjwa na majeruhi (*Ambulance*) hivi karibuni.

b) Jumla ya gari 17 kati ya hizo ishirini (20) zinafanya kazi, tatu (3) kwa sasa ni mbovu. Juhudi zinafanywa ya kuzitengeneza. Kama nilivyosema juhudi zinafanywa na Kikosi chetu cha Zimamoto kuzifanyia matengenezo gari hizo mbovu kwa kuwatumia wanafunzi wa kikosi.

c) Kikosi kinamiliki jumla ya gari tatu (3) za kubebea majeruhi, mbili kati ya hizo zipo Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Unguja na moja ipo Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume, na moja ipo Uwanja wa Ndege wa Pemba. Ahsante.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa : Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza.

Mhe. Waziri kama utakumbuka jana ulivyokuwa unajibu swali langu Nam. 149 ulisema kwamba, kwa mujibu wa utaratibu wa Kimataifa kwamba moto unatakiwa uwe umeshadhibitiwa ndani ya dakika tano tangu ulipoanza kuwaka. Sasa nikitizama hii takwimu ya hizi gari unazoeleza ulizonazo za kuzimia moto hasa ukiangalia kwa kule Pemba, naona sijui itachukua dakika ngapi kwa gari kutoka Chanjaani mfano kwenda Wete, kwa ajili ya kwenda kuuzima moto. Hili nahisi ni tatizo.

(a) Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuweka vituo vyengine katika maeneo kama hayo.
(b) Katika maelezo yako umetuambia kwamba una gari moja pale Mahonda, mimi nilikuwa nataka kujua gari ya pale ni ya aina gani. Maana nakumbuka kulikuwepo ki- *land rover* kidogo ambacho nahisi moto kama utakuwa wa nyumba mbili tu umeshika hakiwezi kuzima.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakiri kama alivyosema kwamba jana nilizungumza kimataifa moto ule unatakiwa uzimwe ndani ya dakika tatu, vyenginevyo utaleta hasara. Pia nakiri kwamba tuna mapungufu kama nilivyosema, lakini hivi sasa Wizara yetu ya Nchi, Ofiri ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupitia kitengo hichi cha Zimamoto kama nilivyosema, nishaagiza gari nyengine. Pia tuna mipango ya kufungua vituo zaidi hasa Bemba, tuna mpango wa kufungua kituo Wete na Mkoani. Tayari tumeshajiandaa, hivi juzi tumefanya uhamisho, vijana wetu wengi tumewapeleka Pemba ili kwenda kushika nafasi katika sehemu hizo. Na hizo gari mpya zikija pia tutayapeleka katika sehemu hizo. Kwa hiyo hili kwa kweli tumejiandaa na taratibu zipo njiani.

Mahonda kweli kuna ki- *land rover* kimoja, lakini ni lazima nikiri kwamba kinasaidia mpaka hapo tutakapopata gari nyengine. Kwa sababu kwenye mashamba ya miwa mara kwa mara kunatokea moto, na hicho hicho Mhe. Mtando amesema kidogo lakini muhimu zile zana nyengine. Lakini kinafanya kazi nzuri sana. Lakini nakiri kwamba tunajiandaa kutanua wigo wa shughuli zetu. Ahsante.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa fursa ya kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Waziri wakati alipokuwa akijibu swali amekiri kwamba, Pemba kuna uchache wa gari hizi za kuzimia moto, pia pamoja na vituo ambavyo vipo Mbale, na kasema kwamba wana mpango wa kuongeza vituo.

Sasa napenda kumuuliza Mhe. Waziri kwa sababu kakiri na kwa sababu gari zilizopo Pemba ni chache, na hizo chache zilizopo tumekwenda Uwanja wa Ndege juzi gari inayofanya kazi ni moja na wakati kuna gari mbili.

(a) Sasa ili kupunguza usumbufu na huku wakisubiri gari nyengine, ni lini gari iliyokuwepo Uwanja wa Ndege Chake Chake Pemba itafanyiwa utaratibu, ili iweze kukidhi haja na kusaidia lile jengine lililopo.

Je, wale askari waliokuwepo Chake Chake hawana hata sehemu ya kukaa, banda lao limeanguka lipo nyang'a nyang'a, na ikiwa wao hawawezi kupata utulivu, hata ukitokea huo moto basi watakuwa

hawawezi kwenda kuuzima kwa utulivu. Ni lini atawasaidia ili waweze kupata makazi ya kudumu, mazuri na pindi ikitokea moto waweze kukidhi haja vizuri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba kulikuwa na gari moja tu Pemba ambayo ilikuwa inafanya kazi, lakini hivi sasa ipo gari ya pili ambayo tulikuwa tunatafuta usafiri zaidi ya miezi miwili. Hiyo gari ipo tayari wakati wowote itakwenda Pemba kusaidia kuongeza nguvu kule.

Pia ulisema kuhusu makaazi ya wafanyakazi. Hilo tunalishughulikia na nafikiri ukipita pale Chanjaani utaona pana ujenzi, tayari tumeshavuka hatua ya msingi, ule ni ujenzi wa ofisi na makaazi ya wale askari ambao wapo zamu, ili wasiwe wanakaa kwenye miti, wakati wa moto wanatafutwa. Kwa hiyo wote watakuwa pale kama kambini na kazi hiyo inaendelea.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Kwa vile moto hutokea sehemu zote za hatari hasa baharini na kwenye nyumba refu ambazo zinajengwa hivi sasa. Je, Idara yako ya uokozi hivi sasa ina meli ngapi za kisasa ambazo zina zana za kuzimia moto, pamoja na ndege za kisasa za kuweza kuzima moto kwenye nyumba refu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kuhusu gari nafikiri nimeelezea zile gari tulizonazo. Na vifaa pia sina orodha kamili ila nitaitafuta, lakini kwa kweli tunajivunia jeshi letu la Zimamoto na Uokozi, hivi sasa lina zana za kisasa kabisa, zina winji hata za kwenda nyumba ya ghorofa hata mita mia au mia na hamsini juu, na pia tunao wazamiaji na pia tunao watu wana zana mpaka za kuingia kwenye visima. Kazi hiyo wanaifanya kwa nguvu kubwa sana.

Mhe. Spika, kwa kweli hivi sasa meli za kuzimia moto hivi sasa hatuna. Ikitokea shughuli kama hizi za moto wa baharini, basi tunatumia ile tagi ya Shirika la Bandari ambayo vijana wetu wanaingia mle na zana zao wanakwenda kuzima moto.

Mfano hivi juzi tu iliungua meli moja, kwa kweli vijana wetu walitumia tagi hiyo na zana zao, na wana mashine kama nilivyosema za kisasa kabisa. Kule hawakwenda na maji, yale yale maji ya chumvi wametumia na pampu zao, ikawa wanatumia yale maji ya chumvi wana *circulate* na wamezima moto, na wamefanikiwa vizuri kabisa.

Nam. 10

Ukosefu wa *INCINERATOR* Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Miongoni mwa vifaa muhimu katika hospitali kubwa kama vile Mnazi Mmoja ni *"INCINERATOR"* ya kuchomea taka. Kifaa hicho katika hospitali hiyo hakipo au hakifanyi kazi vizuri suala ambalo linapelekea kurundikana kwa taka za hospitali hapa Mjini.

(a) Je, Mhe. Waziri, Wizara inafahamu suala hilo.

(b) Kama inalifahamu Wizara inawaeleza nini wananchi kupitia Baraza hili.

(c) Je, taka hizo kuendelea kuzagaa katika eneo hilo la Hospitali ya Mnazi Mmoja si kuhatarisha afya za wafanyakazi na wananchi kwa ujumla.

Mhe.Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe.Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 10 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe.Spika, swali hili limeulizwa kipindi kilichopita likiwa na namba 45 na tukiangalia *hansard* tutalikuta. Nitarudia tena kusema yale yale kwamba Hospitali ya Mnazi Mmoja ina *incinerator* mbili (2), ya umeme na ya kuni. *Incinerator* inayotumia kuni inafanya kazi, na tatizo lake liko kwenye bomba la kutolea moshi, limekuwa bovu, limeharibika kwa hivyo moshi hauendi juu. Pia kuna shimo maalum la kuzikia mazalia. Changamoto zinazoikabili hospitali ya Mnazi Moja katika kuhifadhi na kuangamiza taka taka, ni kutokana na idadi kubwa ya taka zinazozalishwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, na Hospitali binafsi ambazo zinaletwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa madhumuni ya kuchomwa.Uwezo wa mashine za kuchomea taka ni mdogo kulinganisha na taka zinazozalishwa, na wala hakuna mfumo unaoeleweka wa kuhifadhi mabaki ya jivu baada ya uchomaji taka. Hali hii ndiyo inapelekea taka kuchomwa katika ufukwe wa bahari, hali ambayo ni hatari kwa wafanyakazi wa Hospitali, jamii, mazingira na hata kiuchumi kwani fukwe ni eneo la kitalii.

Nitakachoongezea kusema ni kuzagaa kwa taka katika eneo la Hospitali ya Mnazi Mmoja, ambalo halihatarishi tu afya za wananchi na wafanyakazi kwa jumla, bali mahala kama hospitali ambapo hutegemewa iwafundishe watu usafi penyewe pakawa pachafu ni "aibu".
Lakini hili si tatizo la *Incenerator* pekee, bali ni la wahamiaji wanaohamia hospitali wakati wagonjwa wao wakilazwa, ambao wanakuwepo hospitali saa 24 bila ya wao kuzingatia saa za kukagua wagonjwa, nao ni ndugu na jamaa wa wagonjwa hao. Hawazingatii saa za kuangalia wagonjwa na kutoa nafasi kwa hao wafanyakazi kidogo tulio nao kufanya usafi. Wananchi tunapowaambia inakuwa ni mgongano wa mahusiano.

Mhe.Spika, bila ya kufuata taratibu za saa za kutazama wagonjwa watu kuwepo hospitali, suala hili litakuja kila kikao.Nachukua nafasi hii kwa kutumia Baraza hili kuwaombeni Wawakilishi na wananchi kwa ujumla, kufuata taratibu zinazowekwa ili hospitali yetu iwe safi.

Mhe.Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe.Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, anasema kwamba jibu hili limejibiwa katika kikao kilichopita, lakini nakwambia tatizo bado lipo pale pale, na ndio maana hili suala likarudi tena hapa Barazani. Ushahidi wa huo Makamo wa Kwanza wa Rais alitembelea na akaelezwa tatizo la suala hili, na akaagiza yatafutwe makontena ya dharura kuhifadhia taka hizo.

(a) Je, agizo la Makamo wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad umelitekeleza kiasi gani.

(b) Kwa kuwa mashine za kuharibia taka taka katika hospitali hii ni muhimu kama zilivyo mashine nyengine, Je, kuna utaratibu gani juu ya kuzifanyia matengenezo kama zilivyo mashine za ICU.

Mhe.Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nashukuru kwamba Mwakilishi ameelewa kwamba Makamo wa Kwanza wa Rais ametembelea hapo, na tulikuwa wote na tukalijadili suala hilo la usafi kwa kuchoma taka pamoja na maagizo yakatolewa. Kati ya maagizo yaliyotolewa, ni kushirikiana na wataalamu wa mazingira wa Wizara yake juu ya kutafuta ufumbuzi.

Mhe.Spika, naomba kidogo nilieleze hili ni kwamba taka za hospitali ziko kama aina nne. Kuna taka zile zinazotoka kwenye upasuaji, kuna taka taka za makaratasi na mambo ya maofisi, kuna taka taka ambazo ni hatari za vyuma yaani vigae na sindano ambazo ukizichoma tu kwa moto wa kawaida haziungui na kuna taka taka nyengine za mionzi. Kwa hivyo, taka taka nyengine unaweza kuchoma zikaungua, lakini sindano na vigae haviungui vinahitaji *temperature* isiyopungua 800 mpaka 1200.

Mhe.Spika, baada ya mjadala pale kwenye *site* na baada ya kuwasiliana katika vikao vyetu, kulikuwa na mawazo kwamba labda kuchimbwe shimo au yatafutwe makontena yaingizwe nje ya mji iwe taka zinawekwa huko.Lakini mimi nasema hiyo nayo sio *solution*, kwa sababu ukizitia kwenye mashimo zikianza kuoza huko unakopeleka nako itakuwa ugomvi na wananchi. Mhe.Spika, pia ukisema uzizike basi unakwenda kuhatarisha maji yalioko chini ya ardhi, kwa sababu zile zitaingia kwenye mikondo ya maji. Mhe.Spika, ufumbuzi uliokuwepo pekee ni kupata *machine* inayoweza kuzichoma hizo katika *temperature* iliyokuwa ya juu sana.

Mhe.Spika, kwa mashauriano na wenzangu na wale wa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, tumekubaliana kwamba itafutwe *machine*, na *machine* hiyo ni ya kisasa inapatikana huko Ulaya thamani yake ni dola 200,000, na unachokitia humo huwa hakitoki kitu chochote sio msumari, si sindano, si taka na hakuna kinachotoka ukaweza kukitupa na kusababisha tena hatari. Mhe.Spika, tumeshawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha tulizingatie hilo katika bajeti, tumeshafikisha kwa wahisani, kama kuna suala ambalo nimelifikisha kwa wahisani wengi hakuna

kama hili. Pia Mhe.Makamo wa Rais amezungumza na Balozi wa Ujerumani kwamba atusaidie, na *document* hizi tumeshamfikishia Balozi wa Ujerumani, tumeshazungumza na Wachina, tumeshazungumza na Oman, nimeshazungumza na kila anayekuja pale tatizo lako ni nini, basi imekuwa kila ninaloulizwa nasema ni hilo.

Mhe.Spika, hilo ni suala ambalo tunalielewa na tunalishughulikia lakini si suala la hapo kwa papo kama vile unavyoniita jina langu.Nashukuru kwamba Mhe.Mwakilishi anakunwa na hili na naomba kwamba yeye ni mfanyabiashara, basi tuwatafute wafanyabiashara akitoa mia au akitoa mbili nipate kidogo niagize hiyo *machine*, na mheshimiwa hilo sio jipya kwa Wizara ya Afya. Kwa taarifa yenu tumechimba kisima pale Mwembeladu tumetatua tatizo la maji kwa msaada wa wahisani kwa kupitia hapo basi na waje wafanyabiashara watusaidie, maana uchafu ule unahatarisha hata yale mazingira ya bahari. Mhe.Spika, nadhani nimeeleza vya kutosha.

Nam. 119

Kutelekezwa Uwanja wa Kariakoo Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Uwanja wa Kufurahishia Watoto Kariakoo unakabiliwa na uchakavu mkubwa.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuujenga uwanja huo ikiwa ni sehemu ya kuenzi matunda yaliyoachwa na viongozi wetu.

(b) Je, Serikali kwa nini imewahamisha watu waliokuwa wakitumia eneo la uwanja huo kwa shughuli za kujipatia kipato kabla ya mipango ya kujenga haijakamilika.

(c) Mhe. Waziri lini ujenzi wa uwanja huo utakamilika na kuondoa kero ya eneo hilo hivi sasa kutumika kwa mambo yasiyofaa kwa jamii, kama vile disko na uuzaji wa vilevi.

(d) Ni kiasi gani cha fedha kinachotarajiwa kutumika katika mradi wa uwanja huo na lini ujenzi wake utakuwa umekamilika.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe.Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 119 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe.Spika, kwa sababu swali hili linajirejea mara kwa mara kwa faida ya Mhe. Mwakilishi na wananchi naomba kumjibu swali lake.

a) Mhe. Spika, napenda ifahamike kwamba viwanja vya kufurahishia watoto Kariakoo mwanzoni vilikuwa chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, lakini kwa sasa viwanja hivyo viko Wizara ya Fedha kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*), kwa ajili ya kuvifanyia matengenezo makubwa na kuviongezea ufanisi katika kutoa huduma. Imani yangu ni kwamba mipango thabiti iliyoandaliwa ya kuvifanyia matengenezo hayo itaweza kuenzi matunda yaliyoachwa na viongozi wetu, ya kuwapatia watoto wetu sehemu za kupumzikia na kucheza.

b) Serikali imeamua kuwahamisha watu waliokuwa wakitumia eneo la Uwanja wa Kariakoo ili kuruhusu shughuli za matengenezo hayo zifanyike kwa ufanisi mkubwa.

c) Muda wa kukamilika kwa ujenzi huo utabainika kwenye mkataba utakaofungwa kati ya mjenzi na *ZSSF* baada ya kupatikana kwa mjenzi huyo. Hivi sasa kazi ya kutafuta mjenzi imeanza baada ya kukamilika shughuli za kutangaza tenda.

d) Mhe. Spika, kwa kuwa bado taratibu za kumtafuta mjenzi unaendelea kulingana na maombi ya tenda si rahisi kujua kiasi cha fedha kinachotarajiwa kutumika katika mradi huo.

Mhe.Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe.Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe.Spika, kwa kuwa eneo hilo kwa muda mrefu halitumiki na kugeuka gesti bubu.

a) Je, serikali ina mpango gani kuwapa ulinzi katika eneo hilo.
b) Kwa kuwa pembea za watoto zimekuwa zina muda mrefu na hazijafanyiwa matengenezo, hamuoni kwamba ni hatari kwa watoto wetu katika kipindi hiki.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, mwanzoni mwa suala hili nimesema kuwa Mhe. Mwakilishi kwa sababu analirejea mara kwa mara, maelezo yangu yote niliyoyatoa hapa ni ya uhakika, na kwa kweli kama nilivyosema kuwa viwanja hivi vya Kariakoo vilikuwa kwenye Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, hivyo serikali iko makini kwa kushirikiana pamoja na Wizara ya Fedha kuyashughulikia matatizo ya viwanja hivi cha Unguja na cha Pemba. Mhe. Mwakilishi kwa vile wewe ni mfanyabiashara nakuomba tushirikiane pamoja na wewe ili kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niongeze kulingana na yale masuala ya ziada yaliyoulizwa na Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, suala lake la kwanza ambalo Mhe. Mwakilishi ametuuliza kuhusiana na gesti bubu tutalifanyia kazi kwa kushirikiana na mfuko ili tuweze kuona ni kiasi gani tutakavyoweza kuweka ulinzi katika eneo hili.

Suala lake la pili, linaloeleza kwamba zile pembea ni mbovu na utumiaji wa pembea zile kwa watoto wetu naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba kiwanja kile kwa sasa tumekifunga, na hakuna watoto wanaoruhusiwa kutumia zile pembea kwa sababu hali yake ni mbaya.

Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba tayari tumeshatangaza tenda, na tayari tumeshazifungua tenda zile, hivi sasa tuko katika hatua ya kuangalia yule ambaye ametoa kiwango hafifu ili tuweze kuangalia jinsi gani tutakavyoweza kumkabidhi na ujenzi kuanza. Mhe. Spika, ni matarajio yangu kwamba wakati wowote ule baada ya bodi kukaa na kuidhinisha, hatua zitaanza za ujenzi na tunatarajia katika kipindi cha miezi 12 kiwanja kitakuwa kimeshakamilika.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kuweza kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe.Waziri atakubaliana na mimi kwamba sasa hivi mkandarasi ameshapatikana, lakini mkandarasi huyo aliyepatikana si mfanyakazi mzuri kwa sababu ameshajenga jengo ambalo la *ZRB* linavuja maji.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, mkandarasi kupatikana ni baada ya kukabidhiwa kazi, kwa sasa kama nilivyoeleza kwamba wazabuni wamewasilisha zabuni zao na tumeshazifungua na tunaziangalia, hivyo tutakapokamilisha na tutakapomkabidhi kazi, ndio tutasema huyo ni mkandarasi ambaye aliyepatikana.

Mhe. Spika, vile vile nataka niseme kwamba hiyo kazi ambayo Mhe.Mwakilishi anasema imeharibika kwa kweli mimi sijaiona ilivyoharibika, kama ni jengo la ZRB limejengwa vizuri sana, na sote ni mashahidi na jengo liko njiani. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi aje tukae tuzungumze anambie katika eneo ambalo lililoharibika ili mkandarasi huyu aweze kulirekebisha.

Nam. 144

Nyongeza za Mishahara kwa Wafanyakazi wa SMZ

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) - Aliuliza:-

Napenda kuipongeza Serikali kwa kufanya mabadiliko makubwa ya nyongeza za mishahara na posho kwa wafanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, jambo ambalo linazidi kuamsha ari ya uzalendo kwa wataalamu wetu, na kuimarisha maslahi bora ya wafanyakazi.

(a) Je, ni kiasi gani cha nyongeza walichopata Mahakimu wa Mkoa, Wilaya na Mahakama za mwanzo.

(b) Je, wafanyakazi wa kada ya Uhasibu, Wakaguzi wa ndani na Wakaguzi wa nje wamepata kiasi gani cha nyongeza ya mishahara yao.

(c) Je, Wanasheria wa Ofisi ya Muendesha Mashtaka wamezingatiwa vipi katika kuinua maslahi yao, na kwa nini Serikali isiwapandishe katika kiwango cha juu kama ilivyofanya kwa Mahakimu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 144 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.Mhe. Spika, mshahara wa mtumishi ni siri kati yake na muajiri, hivyo sitotaja kiasi wanacholipwa ila kwa taarifa ya Baraza lako tukufu mishahara ya Mahakimu wa Mikoa na Wilaya ni ya kiwango maalum (*Duty Post Salary*) na haina nyongeza ya kila mwaka, na Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo inategemea kiwango cha ujuzi (*Establishment Salary*), na ina nyongeza za kila mwaka.Mhe.Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe.Mwakilishi swali lake Nam. 144 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wafanyakazi wa kada ya uhasibu na wakaguzi wamepewa nyongeza kwa kutegemea elimu zao na uzoefu wa kazi katika ngazi *za "General Scale"* sawa sawa na wafanyakazi wengine katika utumishi wa umma, isipokuwa kwa Mhasibu Mkuu wa wizara na Mkaguzi Mkuu wa wizara ambao wana majukumu makubwa ya kusimamia fungu la matumizi na mapato ya Serikali katika wizara na taasisi zinazojitegemea.

(b) Wanasheria wa Serikali (*State Attorneys*) na waendesha Mashtaka (*Prosecutors*) wamewekewa ngazi maalum za mishahara ambazo ziko juu ukilinganisha na watendaji wengine, na pia wanapata posho maalum ambazo wengine hawapati.

(c) Wafanyakazi wa kada ya uhasibu na wakaguzi wamepewa nyongeza kwa kutegemea elimu zao na uzoefu wa kazi katika ngazi za *"General Scale"* sawa sawa na wafanyakazi wengine katika utumishi wa umma isipokuwa kwa Mhasibu Mkuu wa Fungu na Mkaguzi Mkuu wa Wizara kama nilivyokwishaeleza kwenye jibu la swali la kifungu (a).

Mhe.Mbarouk Wadi Mussa: Mhe.Spika, nakushukuru kunipa nafasi nimuulize Mhe.Waziri swali moja la nyongeza. Katika swali langu nilipokuwa nimeuliza nilikuwa nataka kujua nyongeza waliyopata Mahakimu wa Mkoa na Wilaya ingawa Mhe.Waziri amesema kwamba ni siri ya muajiriwa na tajiri wake.

Mhe.Spika, mimi nilikuwa nataka kujua ni sababu zipi Mahakimu wa Mkoa na Wilaya wakaingia katika ile nyongeza hawa wa Mahakama za mwanzo hawakupata nyongeza.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, nilisema mwanzo kwamba kuna suala la *duty post salary* na kuna suala la *establishment salary*. *Duty salary* ni mshahara ambao unalipwa kutegemea na nafasi, na *establishment salary* ni mshahara unaolipwa kutegemea na ujuzi, muda wako wa kuajiriwa kazini, kwa bahati nzuri katika mgawanyo wa mishahara ya Mahakama, wafanyakazi wa Mahakama ya mwanzo hawana elimu sawa sawa kama walivyo wafanyakazi wa Mahakama ya Wilaya na Mkoa. Kwa hivyo, hawa wanategemea mishahara inayotokana na *establishment salary* kutokana na viwango vyao vya elimu na muda wao wa kazi. Mhe.Spika, hata hivyo katika kuzingatia uzito na umuhimu wa masuala yao, serikali kupitia wizara yangu imetengeneza utaratibu wa kuwalipa posho wafanyakazi hawa wa Mahakama ya mwanzo mpaka hapo Tume yao ya Utumishi ya Mahakama itakapoweka utaratibu maalum kuzingatia *scheme of service* ya wafanyakazi wa Mahakama.

Mhe.Saleh Nassor Juma: Mhe.Spika, nashukuru na mimi kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.Kwa kuwa Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo ni Wazanzibari na wana haki sawa sawa na Wazanzibari wengine, ikiwa ni pamoja na kupata nyongeza ya mishahara.Na kwa kuwa taasisi zote za utumishi wa umma wameongeza mishahara bila ya kujali taaluma.

Je, kuendelea kuwaachia hawa Mahakimu wa mwanzo kutowalipa mishahara, hivyo si kuwanyima haki yao ya msingi na kuwabagua na watumishi wengine wa serikali.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe.Spika, kwanza nataka nikubaliane nae kwamba Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo ni Wazanzibari sawa sawa na watumishi wengine wowote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Lakini nataka niseme kwamba Mahakimu wa Wilaya na Mahakimu wa Mikoa, ni Mahakimu ambao kwa nafasi zao wanateuliwa kupitia utaratibu uliopo. Na Mahakimu wa Mahakama

ya mwanzo ni watu ambao wanafanyakazi, au wameajiriwa na bado hawajaingia katika nafasi za uteuzi, hii ndio tofauti. Na wao itakapofika maamuzi kwamba serikali itaamua kuwa na wao wateuliwe, basi nadhani hilo litakuwa sio tatizo. Lakini kwa sasa utaratibu uliopo kama nilivyosema mwanzo kuna *duty post salary* na kuna *establishment salary*. Mhe.Spika, hawa Mahakimu wa Mahakama ya Wilaya na Mikoa wako katika ngazi ya *duty post salary* hawategemei viwango vya elimu.

Mhe.Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe.Spika, na mimi naomba niongezee kidogo majibu ya nyongeza kutokana na suala liloulizwa. Mhe.Spika, pamoja na majibu mazuri na ya uhakika ambayo amezungumza Mhe.Waziri napenda niseme kwamba Mahakimu wa Mikoa na Mahakimu wa Wilaya na Mahakimu wa mwanzo, hawa wote tunajua kwamba wanafanyakazi ngumu.

Lakini Mahakimu wa Mikoa na Mahakimu wa Wilaya wako katika sehemu moja kama alivyosema Mhe.Waziri.Mahakimu wa mwanzo kwa kweli hapo mwanzo katika nyongeza walikosewa kutokana na zile nyongeza ambazo ziliongezwa. Suala hili tuliliona, na suala hili tukalizingatia, na suala hili kwa sababu ni wengi hawa, tukamshauri Mhe.Rais na kwa juhudi zake na upendo wake Mhe.Rais amekubaliana na sisi kwamba hawa wataongezwa mshahara wao kulingana na yale mapendekezo ambayo tuliyasema.
Mhe.Spika, katika sherehe za siku ya sheria, Mhe.Rais alitamka hadharani kwamba Mahakimu hawa watalipwa nyongeza yao, watalipwa mshahara mpya ambao tumeupendekeza na zaidi ni kwamba watapewa *arrears* zao kuanzia hapo ambapo wenzao wamelipwa. (*Makofi*).

Nam. 71
Malipo ya Umeme

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:-
Inasemekana kuwa bei ya umeme inayolipwa na wateja hapa Zanzibar ni kubwa kuliko bei inayolipwa na wateja Tanzania Bara.

(a) Je, ni sababu zipi za kimsingi zilizosababisha hali hiyo.

(b) Bei inayolipwa na wateja kutoka kisiwani Unguja ni sawa au tofauti na ile inayolipwa Pemba. Kama ni tofauti ni kwa kiasi gani.

(c) Kwa sababu bei za umeme Tanzania Bara imeongezeka kwa 40%. Hali ikoje kwa Unguja na Pemba.

(d) Nini ushauri wa Serikali kuhusu kadhia hiyo ya bei ya juu ya umeme.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe.Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjbu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 71 lenye (a), (b), (c), na (d) kama hivi ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, sababu kubwa iliyopelekea kuwa na bei tofauti na zile za Tanzania Bara ni kuwa bei tunayonunua umeme kutoka *TANESCO* bado ni kubwa.

b) Mhe. Spika, bei za umeme zinazolipwa na wateja wa Unguja na Pemba ziko sawa.

c) Mhe. Spika, bei za umeme wa Unguja na Pemba nazo pia zitaongezeka kwa wastani wa asilimia 87.

d) Mhe. Spika, ongezeko la bei ya umeme imetokana na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji, hasa baada ya *TANESCO* kununua umeme unaozalishwa kwa mafuta badala ya kuzalishwa na maji kulikosababishwa na ukame.

Mhe.Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kwanza nashukuru kwa kupata majibu ya swali langu isipokuwa swali (d) kuhusu ushauri wa serikali sikujibiwa.

a) Lakini Mhe. Spika, ningeliomba kujua kwa sababu sisi tunalipia umeme zaidi kuliko kule Bara unakotoka, mpaka hivi sasa kwa sababu umeme tunaotumia kutoka Bara ni Pemba na Unguja, na kabla

umeme wa Pemba haujapatikana, serikali yetu ilikuwa ikidaiwa deni kubwa sana la umeme, hivi sasa serikali yetu inadaiwa kiasi gani.

b) Mhe. Spika, ni nini hasa ushauri wa serikali kuhusu hili suala la umeme ambalo deni lake kila siku linazidi na hatuna *control* nalo, ili serikali iweze kufanya njia ya kutupatia umeme wetu mbadala ambao utakuwa chini ya mikono yetu wenyewe.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kuhusu deni tunalodaiwa wizara yangu kupitia Shirika la Umeme Zanzibar kutoka *TANESCO,* hili deni tayari tumelishughulikia. Mimi mwenyewe tarehe 25 Januari, 2012 nimefanya ziara pamoja na Meneja wangu wa Shirika la Umeme nikaonana na Waziri wa Nishati Mhe. Ngeleja pamoja na Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania Bara *TANESCO,* tumelizungumzia suala hili na tumefikia muafaka. Kwa hivyo, deni hili liloongezeka lisilokuwa rasmi tayari limeshafutwa.

Mhe. Spika, kuhusu suala lake la pili ni kwamba bado tunalipa umeme Zanzibar kwa kiwango kikubwa kulinganisha na hii bei ambayo tunayonunulia sasa hivi umeme kutoka *TANESCO* bado iko juu. Kwa hivyo, kama tutapunguza bei kutoka *TANESCO* basi Zanzibar nako tutapunguza bei hii ya kununulia umeme.

UTARATIBU

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, suala langu ni kuwa hivi sasa Zanzibar inadaiwa kiasi gani cha fedha kwa suala hili la umeme, naona sijajibiwa sio utaratibu wa kulipa madeni, ni kiasi gani tunadaiwa na kutokana na deni hilo je, ina mpango gani wa kufanya kila inavyowezekana tukawa na umeme wetu wenyewe. Naona vipengele hivi viwili bado sijajibiwa sahihi.

Mhe.Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nimesema deni tunalodaiwa na *TANESCO* deni ambalo ni la zamani lisilokuwa rasmi tayari limeshafutwa. Kwa deni tunaloendelea nalo sasa hivi kwa umeme tunaotumia kwa kipindi hiki, basi hilo nitakujibu kwa maandishi, lakini la nyuma lisilokuwa rasmi tayari limefutwa.
Mhe.Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mataifa mengine yanayoendelea huzalisha umeme kwa kutumia taka, jua na upepo. Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itatumia lini njia hizi ili kuondosha mzigo kwa wananchi wake.

Mhe.Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, sitomwambia kwamba tutatumia umeme wa aina gani kwa kipindi hiki, lakini serikali imo mbioni na imeshazungumza na wawekezaji mbali mbali kwa suala hili la kuwekeza umeme mbadala Zanzibar, ukiwemo umeme wa upepo, umeme wa gesi, umeme wa *solar* na umeme wa takataka. Kwa hivyo, bado hatujaamua umeme gani au kampuni gani ambayo tutaikubali na kuwa ituzalishie umeme huo Zanzibar.

Mhe.Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, kwa kuwa katika *Freedom and Unity,* kitabu alichokitunga Mhe. J. K. Nyerere ameeleza kwa uwazi kabisa madhara ya nchi kuwa tegemezi, madhara ya kutegemea mataifa mengine, na kwa kuwa Zanzibar hadi leo hii tunategemea Tanganyika kwa ajili ya umeme. Je, ni lini serikali yetu itatutoa katika madhila haya ya kuwa tegemezi katika suala hili.

Mhe.Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe.Spika, siku zote mambo mazuri hayataki haraka.Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi nakuhakikishia kwamba lengo la serikali hii basi kuliondoa tatizo hili Zanzibar, hivyo tuko mbioni na tukijaaliwa si muda mrefu tutafanikiwa juu ya hilo.

Mhe.Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niongezee kidogo kwa lile swali ambalo ameliuliza Mhe. Saleh Nassor.

Kwanza, tayari wenzetu *European Union* wameshateua wataalamu kutoka Ujerumani ambao wanatusaidia sasa hivi kufanya *study* itakayoweza kutuongoza Zanzibar twende katika umeme wa aina gani. Ni matarajio yangu muda wowote katika miezi miwili ijayo *study* hiyo itakuwa iko tayari na Zanzibar itakuwa iko tayari kujua twende katika umeme wa aina gani.

Lakini la pili, hivi sasa tayari kumeshajitokeza wawekezaji kutoka nchi mbali mbali kama China, Swaziland, India, Tanzania ambao wako tayari kuwekeza katika sekta ya umeme.

Lakini la tatu, tayari serikali imeshafanya maamuzi kwamba Zanzibar tunakwenda katika umeme wa kujitegemea.

Nam. 47

Upekuzi wa Gari

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa (Kny. Mhe. Rashid Seif Suleiman) - Aliuliza:

Kila mwaka mpya Idara ya Leseni na Jeshi la Polisi hufanya upekuzi wa gari hasa za abiria. Utaratibu huo huleta usumbufu mkubwa kwa abiria.

Je, wizara ina mkakati gani wa kupunguza au kuondoa kabisa usumbufu huo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kujibu swali Nam. 47 la Mhe. Rashid Seif Suleiman kama hivi ifuatavyo:-

Upekuzi wa gari haufanywi na Idara ya Usafiri na Leseni ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano lakini hufanywa na Askari Polisi. Idara ya Usafiri na Leseni hufanya ukaguzi (*vehicle Inspection*) na ukaguzi huu hufanywa wakati wowote inapobidi. Ukaguzi huu wa kila mwaka ni kwa ajili ya upasishaji wa gari kwa ajili ya kupata ruhusa ya kuendesha chombo hicho kwa mwaka unaofuata. Utaratibu huu ni wa kisheria.

Katika kuondokana na usumbufu unaotokana na ukaguzi huu, Idara ya Usafiri na Leseni ina mpango wa kutafuta njia bora za kisasa ambazo nchi nyengine wanazitumia ili nayo iweze kufuata utaratibu huo. Katika juhudi hizi, Kampuni ya *VIVAS* ya Dar es Salaam imeonesha nia ya kutaka kusaidia katika hili.

Nam. 155
Bei ya Bidhaa mbali mbali

Mhe. Salim Abdulla Hamad - Aliuliza :-

Katika kuwatendea haki wananchi, serikali huwa inaangalia na kufuatilia sana bei ya bidhaa mbali mbali wanazotozwa wananchi wanaponunua bidhaa hizo ambazo huwa zinaingizwa kutoka nje.

(a) Je, chombo kama hicho kipo katika serikali yetu.

(b) Kama kipo je, kinafanya kazi ipasavyo.

(c) Serikali ina maelekezo gani kuhusu hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Ahsante sana Mhe.Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe.Mwakilishi swali lake Nam. 155 lenye kifungu (a), (b) na (c) kwa kuanza na utangulizi ufuatao:-

Mhe.Spika, ni imani ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwamba sote tunaelewa kuwa nchi yoyote ile ina wajibu wa kuwalinda wananchi wake kwa usalama na ubora wa bidhaa.Sio tu zinazoingizwa nchini, lakini hata zile zinazozalishwa ndani ya nchi.

Itakumbukwa kwamba, katika siku za nyuma Mhe.Spika, serikali ilianzisha Tume ya Bei chini ya sheria ya kudhibiti bei (*The Price Control Act)* Nam. 12 ya mwaka 1985, ambapo tume hiyo ilikuwa inapanga bei ya bidhaa kwa mujibu wa sheria iliyokuwepo.

Mhe.Spika, kutokana na mabadiliko ya sera za kiuchumi na kibiashara zinazopelekea kubadilika mara kwa mara, hivyo bidhaa hupangwa kulingana na nguvu ya soko. Serikali imeanzisha sheria ya kuangalia mwenendo wa biashara na kumlinda mtumiaji (*The Fair Trading and Consumer Protection Act of 1995*). Mbali na sheria hiyo, kuna sheria nyengine ambazo zinasaidiana na hiyo ambazo ni Sheria ya Mizani na Vipimo nambari 2 ya mwaka 1983, Sheria ya Biashara ya mwaka 1989, Sheria ya Viwango vya Bidhaa na sio viwango vya elimu ya mwaka 2011 na Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2006.

a) Mhe. Spika, ndio chombo hicho kipo na kimeundwa kwa mujibu wa sheria ya kuangalia mwenendo wa biashara na kumlinda mtumiaji ya mwaka 1995, ambayo pamoja na mambo mengine imeweka masharti ya kuwepo kwa taasisi ya kuangalia mwenendo wa biashara na kumlinda mtumiaji.

b) Mhe. Spika, taasisi hiyo inafanya kazi kwa mujibu wa sheria.

c) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inapenda kutoa wito kwa wananchi wote, kuipa mashirikiano taasisi hiyo ya kuangalia mwenendo wa biashara na kumlinda mtumiaji, ili watakapokuwa wanapita kufanya ukaguzi wa bidhaa katika maduka na masoko, kuweza kuangalia kama bidhaa hizo zinauzwa kwa mujibu wa bei zinavyotangazwa.

Mhe.Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, naomba nishukuru kwa kupata majibu mazuri ya swali langu. Mhe.Spika, kwa sababu bidhaa na hasa bidhaa ya chakula inakuwa bei yake inapanda mara kwa mara, na si rahisi kuteremka, pengine unaweza ukakuta bidhaa ya namna moja katika duka hili kuna bei yake na duka lile kuna bei nyengine. Je, chombo hiki kinapita kuangalia hizi biashara zinavyouzwa, na pale penye matatizo kuweza kuchukua hatua. Kama ni hivyo, tokea chombo hiki kufanya kazi na Mhe.Naibu Waziri kasema kuwa kipo kinafanya kazi, na kuwa mtindo huu wa kuwa kila mtu kuuza bei anayotaka upo unaendelea.Ni wangapi wameshawahi kuchukuliwa hatua.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, tumekuwa tukisema sana ndani ya Baraza lako kwamba, wizara imekuwa ikiweka utaratibu ili kufuatilia suala zima la upandaji wa bei. Na kwa kufanya hivyo Mhe. Spika, tulishaeleza lakini nitarudia kwa manufaa ya Baraza lako kwamba, tumefanya kazi ya kuweka kanuni na taratibu baada ya kukutana na wafanyabiashara, ili kuangalia bei tokea bidhaa zinaagizwa kutoka nje mpaka zinapoingia nchini.

Mhe. Spika, katika upangaji wa bei hizo, tunahakikisha kwamba mtumiaji hapati hasara na vile vile mfanyabiashara naye hapati faida kubwa. Tumekuwa tunakutana nao na tokea tumeanza kufuata utaratibu huo kwa kweli bidhaa Mhe. Spika, na hasa za vyakula kidogo bei zake zimetulia. Kwa sababu mfanyabiashara hatakiwi kuongeza bei ya bidhaa, mpaka tutakapokuwa tunakutana nao na kukubaliana kwa pamoja.

Mhe. Spika, inawezekana kabisa kwamba kuna wafanyabiashara wengine wanaongeza bei kinyume na utaratibu, na zaidi hawa wafanyabiashara wa rejareja. Ndio maana nimetoa wito hapa kwa niaba ya wizara kwamba wananchi watusaidie katika hilo, kila watapokuta bei ambazo zimetangazwa na serikali hazitumiki bei ambazo tunazitoa kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya wanakuwa na nakala hizo, pamoja na masheha wakikuta bei hizo hazitumiki basi watoe mashirikiano yao kwa kuwasilisha taarifa hiyo katika Wizara ya Biashara Mhe. Spika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali la nyongeza lenye kifungu *a* na *b*.

(a) Mhe. Spika, mara baada ya kuanza kwa Serikali hii ya Awamu ya Saba, wizara yake kupitia Mhe. Waziri ilikuwa na utaratibu wa kutoa muongozo wa bei za vyakula na vitu mbali mbali kila baada ya muda, lakini sasa utaratibu ule umesitishwa. Naomba kujua wizara iliona nini hata ikawa sasa haitoi utaratibu ule kwa wananchi.

(b) Miongoni mwa sababu ambazo wizara ilikuwa ikitueleza za upandaji wa bei za bidhaa ni pamoja na mfumko wa bei wa dunia, ambao umeathiriwa na mtikisiko wa dunia ikiwa ni pamoja na bei ya mafuta na suala zima la maharamia kule Somalia. Sasa kuna kauli gani ya serikali kwa sababu naona mambo yamepungua, bei ya mafuta imeshuka kidogo, na Somalia kidogo shuwari, sasa tutafutiwe hiyo sababu nyengine mtwambie ili wananchi wajue.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, tumesema katika Baraza lako tukufu na tutaendelea kusema kwamba, upangaji wa bei za bidhaa na hasa za vyakula ni baada ya kukaa kwa pamoja na wafanyabiashara. Lakini nimekubali hapa kwamba, kwa kuwa tunaokaa nao ni wafanyabiashara wakubwa, inawezekana kabisa kwamba wafanyabiashara wa rejareja wakaongeza bei kinyume na utaratibu.

Sasa hapa Mhe. Spika, ni suala la kusaidiana, tunaposema wananchi tusaidiane nao ni pamoja na wawakilishi wao, tusaidiane katika kulisimamia hili ili kuona kwamba bei hizo hazipandishwi kinyume na tunavyokubaliana na wafanyabiashara wanaoleta vyakula hivyo hapa nchini.

Mhe. Spika, hatuwezi kukataa kwamba bei ya vyakula kwa kiasi kikubwa inatokana na bei katika soko la dunia. Kama soko la dunia bei yake ni kubwa, sisi hatuwezi tukasema bei yetu tutaiweka ndogo, kwa sababu yule muagiziaji hana budi kupata faida yake. Lakini na suala la uharamia pamoja na kwamba linashughulikiwa lakini bado halijamalizika. Kwa hivyo, na hilo pia bado ni suala ambalo linazingatiwa katika kuweka bei ya bidhaa ambazo tunaziagiza hapa nchini.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, baada ya jawabu nzuri ambazo ametoa Mhe. Naibu Waziri wangu, naomba kidogo niendeleze lile swali la Mhe. Hija Hassan kuhusu kutangaza bei za bidha. Naomba niwahakikishie kwamba mtindo wa kutangaza bei za bidhaa utaendelea kama kawaida, ulisita kidogo baada ya kuwa kulikuwa na mvutano wa bei baina ya soko la dunia na kuanguka kwa dola ya Marekani. Lakini bei zikitulia tu, bei zitatangazwa na mtindo huo utaendelea kama kawaida.

Swali la pili ni suala la bei za vyakula kama mchele, sukari na unga. Kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba mazungumzo baina ya wafanyabiashara na Wizara ya Biashara yanafanyika kila mizigo inapoingia, na ni kweli kwamba ilikuwa bei ni kubwa lakini sasa zimeshuka.

Mhe. Spika, bei za vyakula kwa mfano mchele ulikuwa unauzwa tani dola 580 ukashuka mpaka ukafikia tani moja dola 535, bei ya sukari ilikuwa ikiuzwa tani moja dola 850 ilishuka mpaka ikafikia tani moja dola 750, na bei ya unga ilishuka kwa asilimia 8. Vile vile sarafu ya Tanzania ilipata kidogo msuli ikatuna, kwa hivyo dola ilianguka kutoka shilingi 1,800 mpaka shilingi 1,600. Kutokana na hali hiyo bei za bidhaa vile vile zilishuka, pakiti moja ya mchele ilishuka kutoka shilingi 56,000 mpaka kufikia shilingi 46,000, na sasa hivi pakiti moja ya mchele iko shilingi 52,000 mpaka 52,500. Bei ya sukari imeshuka mpaka shilingi 72,000 kwa pakiti moja kutoka shilingi 85,000, na bei ya unga ilishuka kutoka shilingi 52,000 mpaka kufikia shilingi 46,000 na mwengine shilingi 49,000.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nataka niwathibitishie wananchi wote kwamba bei za bidhaa katika Afrika Mashariki ziko chini Zanzibar tu, ukiangalia bei za mchele, sukari kwa Kenya uko zaidi ya asilimia 20 ukilinganisha na bei za Zanzibar. Tanzania Bara sukari inaanzia shilingi 2,500, Zanzibar ni shilingi 1,700, ukienda Uganda kuna mpaka viwanda vya kuzalisha sukari sasa hivi sukari ni shilingi 3,600 mpaka 4,000 kwa kilo kwa pesa za Tanzania, ukienda Rwanda bei ya sukari imepanda mpaka juzi Wizara ya Biashara na Viwanda imetangaza kwamba sukari kuingiza Rwanda ni bila ya ushuru kwa sababu imefika kilo moja dola mbili kwa Rwanda.

Kwa hivyo, tumshukuru Mwenyezi Mungu na Wafanyabiashara na jitihada za serikali ya Zanzibar kuona kwamba, bei za bidhaa za vyakula kwa Zanzibar sasa hivi ziko chini kabisa, ukilinganisha na bei zote za Afrika Mashariki. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 39

Mabadiliko katika Elimu ya Ufundi

Mhe. Ismail Jussa Ladhu (Kny. Mhe. Rashid Seif Suleiman) – Aliuliza:

Kutokana na umuhimu wa Elimu ya Ufundi hapa nchini. Je, kuna mabadiliko gani yaliyofanywa na wizara kuendeleza elimu hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Nakushukuru sana Mhe. Spika, na kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 39 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba elimu ya ufundi ina umuhimu mkubwa, na haina budi kubadilika kutokana na mabadiliko ya maendeleo ya sayansi na teknolojia duniani, ambayo yamechochea kasi ya maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii ulimwenguni. Katika kuamini hilo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweka kipaumbele katika maendeleo ya ufundi, ili iweze kuchangia katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Katika Sekta ya Elimu, wizara imeanzisha vyuo viwili vya Mafunzo ya Amali huko Mkokotoni na Vitongoji, ambapo mafunzo mbali mbali ya fani za ufundi kama vile umeme, utengenezaji wa mafriji na *air condition*, ufundi wa gari na ufundi vyuma unafundishwa kwa vijana mbali mbali. Miongoni mwao ni walioacha masomo kabla ya kumaliza Kidato cha Pili au waliomaliza Kidato cha Nne.

Pia Chuo cha Ufundi cha Karume, hivi sasa kimepandishwa hadhi na kuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume. Taasisi hiyo inatoa mafunzo ya stashahada ya fani mbali mbali za ufundi badala ya *FTC* kama ilivyokuwa hapo zamani. Tunatarajia, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume itaanza kutoa mafunzo ya shahada za fani za ufundi katika kipindi cha miaka mitatu ijayo. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Spika na nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake fasaha na mazuri, lakini naomba kuuliza swali la nyongeza lenye kifungu *a* na *b*.

a) Pamoja na kazi nzuri inayofanywa ya kuanzishwa vyuo hivyo alivyovitaja vya Mafunzo ya Amali ambavyo vinatoa mafunzo ya aina nyingi, lakini bado wengi wa wahitimu wa vyuo hivyo wanapata shida ya kujiajiri kutokana na kukosa uwezo wa hata kuwa na vifaa vinavyotumika katika kazi kama hizo. Serikali ina mpango gani wa kuiga mfano mzuri wa nchi kama Upande wa Ujerumani Mashariki, Ambao vyuo kama hivi vinapomaliza huwakabidhi wale vijana wanaohitimu kile kiboksi chenye zana kamili za kufanyia kazi waliyofunzwa ili waweze kuingia katika soko na kuweza kupata kazi za mikono za aina mbali mbali.

b) Mhe. Spika, katika kusaidia hilo pengine na katika kuanzisha vyuo hivyo vya Mafunzo ya Amali, tunafahamu sheria za Zanzibar zimeweka utaratibu wa kutoza *Development Skill Levy* kwa wawekezaji ambapo ni asilimia 5 inapaswa kwenda katika kusaidia kuanzisha na kusukuma mbele mafunzo ya ufundi. Je, fedha hii inakusanywa na kama inakusanywa ni kiasi gani kimepelekwa Wizara ya Elimu ili kusaidia shughuli hizo. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali : Mhe. Spika, Mheshimiwa alizungumza ni namna gani ambavyo baada ya mafunzo yale ambayo tunawapa wanafunzi wetu miaka mitatu tunaweza kuwasaidia. Mhe. Spika, tuna Mfuko ambao wafadhili wametujengea vile vyuo wametupa Mfuko ule. Mwanafunzi anapotoka pale hukabidhiwa mkopo ili uweze kumsaidia yeye katika ile fani ambayo amesomea kwa kununua hivi vifaa. Kwa hivyo, Mfuko huo nimhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba upo na tunatarajia kwa sababu mafunzo yale ni ya miaka mitatu, *batch* ya mwanzo itatoka mwaka huu hivyo wale wanafunzi waliopo pale basi watafaidika na huu Mfuko.

Mhe. Spika, swali (b) ambalo aliliuliza Mhe. Mjumbe ni kweli kuna fedha ambazo zinatolewa na wawekezaji ambao biashara zao tayari zinajiendesha kusaidia Vyuo vyetu vya Amali.

Mhe. Spika, Baraza la Mapinduzi liliunda kamati ya Kufuatilia na Kutathmini ugawaji wa fungu hili la asilimia 5 ambalo tulipata kwa wawekezaji. Naamini pesa hizo zikianza kutumika na hii si kwa vyuo vya serikali tu vya amali Mhe. Spika, tuna vyuo vingi vya binafsi. Kwa hivyo ni kwa ajili ya vyuo vya serikali na vile vyuo vya binafsi vilivyoko mitaani ambavyo vimejisajili, basi fedha hizi zinaweza kutusaidia sana kukwamua yale matatizo mbali mbali ambayo tunayo katika vyuo vyetu vya amali.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, tunasubiri hiyo ripoti ya Kamati ya Baraza la Mapinduzi tuwasilishiwe ili tujue huo mgao utakuwa wa kiasi gani. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Nassor Ali Salim: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kuna Mfuko wa *Tanzania Education Authority*. Je, taasisi zetu zinafaidika nini katika mfuko huu.

Mhe.Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe.Spika, taasisi zetu za elimu zinafaidika na mfuko huu. Kwa mfano, hivi karibuni tu chuo chetu cha *SUZA* kimepata fedha ambazo zimesaidia kununua vifaa vya sayansi. Lakini na taasisi yetu ya Karume imeshafaidika na pesa hizo wameshasaidiwa kompyuta na mambo mengine kama hayo.

Kwa kweli Mhe.Spika, nataka niwaambie Waheshimiwa Wajumbe wako kwamba, sisi na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya Tanzania Bara tunashirikiana nayo vizuri, tunapanga nayo, tunazungumza nayo na kuna mikopo ambayo wanatoa wenzetu hawa na taasisi zetu hazifungiki kuomba mikopo hiyo.Uzuri wa taasisi zetu zina bodi zake ambazo zinajiendesha na kujiamulia.

Kwa hivyo, wao wakiona wanahitaji kuchukua mikopo hiyo basi wanaweza kuchukua kwa kuwasiliana na wizara, kwa sababu wizara iwasiliane na Wizara ya Fedha, mwisho wa siku pesa zile zitalipwa na serikali. Sasa ni lazima wapitie hizo njia. Mhe.Spika, kwa ufupi nilitaka kusema kuwa tunafaidika na mfuko huo.

Hoja za Serikali

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Upimaji na Tathmini ya Elimu Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe.Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nakushukuru tena kwa kunipa fursa ya kuchangia na mimi katika mswada huu ambao uko mbele yetu, Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Upimaji na Tathmini ya Elimu Zanzibar.

Mhe.Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai wenye afya na kutuwezesha kukutana leo hii na kuendelea na majadiliano yetu kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Upimaji na Tathmini ya Elimu Zanzibar.

Mhe.Spika, pili nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia mswada huu.Vile vile napenda kumshukuru Mhe.Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri hapo jana na hatimae mswada huu kufanikiwa vizuri kwa Waheshimiwa Wawakilishi kuweza kuchangia vizuri. Pia napenda kuwashukuru waheshimiwa wote ambao walichangia kutupa mapendekezo yao, na nawaahidi wizara itayafanyia kazi masuala mbali mbali ambayo yalijitokeza katika mswada huu ili uweze kuwa imara zaidi.

Mhe.Spika, tatu naomba nimshukuru Mhe.Waziri wangu ambaye nimefanya kazi nae kwa kipindi cha mwaka mmoja na zaidi sasa, malezi ambayo alinilea ni malezi ya mapenzi makubwa, aliweza kuiunganisha wizara tukaweza kufanya kazi pamoja. Mhe.Spika, nataka nikiri mbele ya Baraza lako tukufu kwamba mbali ya yale mapenzi ambayo nilipewa na baba na mama, miaka 18 ambayo nilipata malezi katika chama changu basi mtu wa tatu katika maisha yangu ambaye sitomsahau ni Mhe.Waziri wangu. Kwa sababu nimeingia katika wizara ile nikiwa kama kipofu ambaye macho yangu yako wazi, sijui pa kuanzia wala pa kumalizia.Lakini kwa busara zake niliweza kufanya kazi zangu za kila siku ambazo serikali hii ilinikabidhi. Mhe.Spika, namshukuru sana Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban na namuombea dua Mwenyezi Mungu amjaalie amuongoze katika wizara mpya aliyopangiwa hivi karibuni.

Mhe.Spika, sasa naomba niende katika hoja za wajumbe, nimsaidie waziri wangu katika kufafanua hoja mbali mbali ambazo zimejitokeza.Mhe.Spika, mimi nataka niende kwa Mhe. Rashid Seif Suleiman ambaye ni katika mmoja ya waliochangia mswada huu, na nianze kusema kuwa namshukuru sana kwa kutoa ufafanuzi kuhusu upimaji na tathmini. Napenda kumhakikishia kuwa maelezo na mtazamo wake unalingana na mtazamo wetu, na ninakubaliana nae kuwa upimaji na tathmini haumaliziki tu katika kufanya mitihani, au kutoa matokeo, bali ina maana pana zaidi kama alivyosema kuangalia mambo mbali mbali ya kuchangia katika kuleta elimu bora.

Mhe.Spika, suala hili pia alilichangia Mhe.Mohammed Haji Khalid. Nataka nikubaliane nao, na niseme hilo ndilo lengo la wizara.Mhe. Spika, ili kuleta elimu bora basi pia ni kuhakikisha kama walimu wanasomesha vile ambavyo unatakiwa kusomesha, kama jana alivyozungumza Mhe. Mohammed alipokuwa akitoa mchango wake. Yeye ni mwalimu mzuri na ni mwalimu wa zamani, kwa hivyo alieleza vizuri sana namna takwimu hizi ambazo inatakiwa wizara ielekeze.

Mhe.Spika, Mhe. Rashid Seif Suleiman pia alizungumza kuhusu kutolewa matokeo ya mtihani wa kidato cha pili, ambapo alisema katika muda wote wa ualimu wake matokeo ya mitihani hayo hakuwahi kuyaona.Napenda kumhakikishia Mhe. Rashid kuwa mojawapo ya majukumu ya chombo hichi kwa mujibu wa kifungu cha 5 (g) ni kutoa matokeo, na kutoa vyeti kwa wanafunzi waliofaulu jambo hili tutalitekeleza.

Kuhusu kifungu cha 4 (3) nakubaliana nae kuwa kina makosa na kimerekebishwa, na kilivyokusudiwa kifungu hichi Mhe.Spika, ni kuwa bodi itachagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuwa makamo mwenyekiti, na sio mwenyekiti kama ilivyojionesha kwenye mswada wenyewe.

Mhe.Spika, napenda kutoa ufafanuzi kuhusu jina la bodi na wajumbe ambao hawakuwa wajumbe kwa muda wa miaka mitatu. Wajumbe hawa sio wa kudumu na sio waajiriwa wa bodi. Bodi zenye wajumbe kama hawa ziko nyingi tu kama vile Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, na ndio maana mbali ya wajumbe wa bodi chombo hiki kinafanya kazi yake ya kawaida ambapo hawa ni wa kudumu na wameajiriwa na bodi. Mhe.Spika, tumepokea mchango wa Mhe. Rashid Seif Suleiman na namhakikishia kuwa tumekusudia kuleta mabadiliko ya dhati katika chombo hiki na tutaweka watendaji ambao watakuwa na uwezo na tunatarajia hao wataweza kuleta mabadiliko.

Mhe.Spika, namshukuru pia Mhe.Abdalla Juma Abdalla kwa mchango wake mzuri na ushauri aliotupa, ni kweli uwezo wa wanafunzi wetu kwa lugha ya Kiingereza na katika masomo ya hesabu ni mdogo. Suala hili linatupa changamoto kubwa kwa wizara, na tunajaribu kutafuta mbinu mbali mbali za kuinua usomeshaji wa masomo haya na hata masomo mengine.

Hata hivyo, nataka kutofautiana na Mhe.Abdalla Juma Abdalla kuhusiana na kushuka kwa kiwango cha elimu hapa Zanzibar. Kwani ushahidi unaonesha kuwa wanafunzi wengi wanafanya vizuri, na ndio maana wanapata sifa za kuendelea na masomo ya juu. Mhe.Spika, wanafunzi wetu wa masomo ya juu wameongezeka sana, na katika baadhi ya miaka wanafunzi wetu wanafanya vizuri sana lakini kuna kipindi huwa ni wastani.

Kuhusu wingi wa masomo, suala hili limefanyiwa kazi sana kwa vipindi tofauti, na ndio maana katika ngazi ya msingi baadhi ya mada zimechanganywa pamoja.

Kuhusu ubaguzi kwa wenzetu, mimi Mhe. Spika, niseme hili sina ushahidi nalo na napenda kuwahakikishia wajumbe kuwa tunapata mashirikiano ya hali ya juu kutoka kwa Mhe.Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi wa Tanzania Bara.Mhe. Spika, leo hii tunatarajia kuwa Mhe. Waziri huyu kufika hapa Zanzibar kufanya ziara ya siku mbili, na kufanya mazungumzo kuhusu masuala mbali mbali yanayohusu elimu, penye matatizo tunakaa pamoja na kujadiliana na kutafuta njia ya kutatua.

Kuhusu mtihani wa kidato cha nne, hili tayari tumelizungumza. Kuhusu kazi za katibu ni kweli hazikutajwa, lakini kama nilivyotangulia kusema yeye atakuwa ni mwajiri wa bodi, atakuwa katibu wa bodi katika masuala ya kuweka kumbukumbu za vikao vya bodi, lakini yeye si mjumbe wa bodi kutokana na kuwa hatokuwa na kura ya maamuzi.

Mhe.Spika, pia tunamshukuru Mhe.Rufai Said Rufai amezungumza suala la chombo hichi kuitwa Baraza la Mitihani.Suala hili Mhe.Mwanasheria Mkuu jana alilitolea ufafanuzi wa kutosha na mimi nisingependa kulizungumzia tena.

Kuhusu chombo hichi kusimamia walimu wa skuli za *tuition*. Mhe.Spika, haya si mamlaka ya chombo hichi katika kusimamia masuala haya, wenye mamlaka kuhusu walimu ni Idara ya Mafunzo ya Ualimu, Idara ya Msingi na Sekondari zinasimamia skuli zetu mbali mbali.

Lakini Mhe. Spika, nataka nikubaliane na Mhe.Rufai Said Rufai kama skuli zetu nyingi zimekuwa na matatizo haya ya ugomvi kati ya walimu ambao wanasomesha pale, na wale walimu ambao wanatoa *tuition*. Mhe.Spika, katika

ziara ambayo nilikwenda karibuni matatizo haya niliyakuta, na tulijaribu kuyatatua na pale ambapo tuliona ni makubwa sana, basi tulizifunga *tuition* zile. Moja ya skuli ambayo tuliifunga *tuition* ile ni skuli ya Darajani.

Lakini katika ziara zangu Mhe.Spika, nilikuwa nikizungumza na walimu wetu kwa sababu inaonekana haya masuala ya *tuition* yameshaleta maneno makubwa sana, na hata pale tulipojaribu hizi *tuition* kuziweka kikomo tunaposema kama mwisho wa *tuition* uwe ni saa mbili, basi kwa njia moja au nyengine inakuwa wenzetu hawatufahamu. Sasa Mhe. Spika, niseme suala hili la *tuition* tunalifanyia kazi na kuzungumza na walimu wetu kwa urefu.

Mimi nasema Mhe.Spika, walimu wetu kama kweli wanafundisha inavyotakiwa kufundisha, wakamaliza *syllabus* zao, wakafanya *test* za wiki, wakafanya *revision* kwa ajili ya yale ambayo wameyasomesha, basi mimi umuhimu wa *tuition* nauona ni mdogo sana. Faida inayopatikana niseme ni ndogo kuliko ile hasara ambayo inazalishwa na *tuition*. Kwa hivyo, suala hili Mhe.Spika, wizara tunalifanyia kazi, na tutakapopata muafaka basi tutalizungumza na watu wote watalisikia.

Mhe.Spika, naomba niendelee kwa Mhe.Mussa Ali Hassan, nazipokea pongezi zake alizotupa na ushauri aliotupa naupokea kwa niaba ya wizara yetu, bodi itazingatia mahitaji ya wanafunzi na wasimamizi wa mitihani watapatiwa mafunzo, na usimamizi wa mitihani tunahitaji kwa kadri ya uwezo wetu kuhakikisha kuwa mitihani yetu haivuji.

Mhe.Spika, katika hili nataka nilieleze Baraza lako tukufu kuwa hivi sasa kumezuka madalali wa mitihani, ambao kinapokaribia kipindi cha mitihani huzunguka maeneo mbali mbali kuwarubuni wanafunzi, kuwarubuni wazazi kuwa kuna mitihani ambayo imevuja. Mhe.Spika, wizara suala hili tumeshalisemea sana, hata katika mitihani yetu ya karibuni nilikusanya vyombo vyote vya habari nikazungumza navyo wakati waziri wangu alikuwa kazini nje ya nchi, nikawaambia kuwa tunaanza mitihani yetu nikawatahadharisha wazazi na wanafunzi juu ya utapeli huu wa biashara iliyoingia ya mitihani.

Kwa hivyo, niliwaomba wanafunzi wajikite katika masomo yao, sio wasubiri mivujo, wenyewe wanaita hii ni *life jacket.* Mhe.Spika, hii haitatusaidia sana katika kuimarisha elimu bora Zanzibar, mwisho wa siku ni kurithi vijana ambao elimu yao inakuwa legelege na bila shaka elimu ikiwa legelege basi maendeleo hayatapatikana.

Mhe.Spika, naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya waziri wangu na wizara yangu kwa jumla, kuwakumbusha wazazi na wanafunzi juu ya kadhia hii ambayo imeingia ndani ya nchi.

Mhe.Spika, kuhusu somo la sayansi kupewa mkazo suala hili tunakubaliana nae Mhe.Mussa Ali Hassan na tunalifanyia kazi ijapokuwa tuna *challenge* kubwa ya walimu wa sayansi, lakini hivi karibuni tumepata kidogo kuajiri walimu kwa hivyo hawa naamini wataweza kutusaidia.

Mhe.Spika, Mhe.Hija Hassan Hija pia namshukuru na ni kweli kuwa serikali inatumia fedha nyingi kwa ajili ya mitihani katika skuli zetu, kwa mwanafunzi wa kidato cha nne serikali inalipa milioni 40 kwa wanafunzi wa serikali kwa ajili ya kufanya mitihani.
Hoja ya kufanya mitihani yetu ya kidato cha nne tayari mheshimiwa imeshajibiwa.

Mhe.Spika, namshukuru Mhe.Hamza Hassan Juma kwa mchango wake yeye amezungumza sana kuhusu suala la chombo hichi kuitwa Baraza la Mitihani, na ameelezea hasara iliyopatikana kwa wanafunzi wetu kufutiwa matokeo yao, umaskini wa familia zetu na hasara kubwa kwa watoto wa kike ambao wanaweza kuolewa.

Pia amezungumzia haja ya kuanzisha Baraza letu la Mitihani, pia amezungumzia umuhimu wa elimu kama rasilimali ya nchi yetu na ametaka tusiwaangushe katika kufanya majumuisho. Mhe.Spika, namhakikishia Mhe.Hamza Hassan Juma kama hatutowaangusha ingawa wakati mwengine ili tuweze kupona na kupata uzima, ni lazima tumeze dawa, hata kama dawa hiyo ni chungu ili mradi maradhi tuliyonayo tuweze kuyaondoa. Mhe.Spika, suala hili la mitihani namuachia Mhe.Waziri wangu atalitolea ufafanuzi kwa wote ambao wamechangia suala hili kwa jumla.

Mhe.Mohammed Haji Khalid yeye alizungumza sana kuhusu usimamizi mbovu katika mitihani, kuwa ndio chanzo cha matatizo ya wanafunzi wetu kufutiwa matokeo haya ya mitihani. Napenda kukubaliana nae kwamba katika baadhi ya vituo vyetu wasimamizi wa mitihani wamechangia katika wanafunzi kufanya udanganyifu. Wizara hili tunalifanyia kazi na wote watakaogundulika kuwa walizembea watachukuliwa hatua.

Mhe.Spika, pia ni kweli katika baadhi ya skuli zetu idadi ya wanafunzi ni wengi mno. Hili wizara inajitahidi kukamilisha madarasa mapya, ili angalau kupungua idadi ya wanafunzi. Ingawa Mhe. Spika, inaonekana kuwa idadi ya wanafunzi inaongezeka siku hadi siku, madarasa tunajenga lakini kwa kweli na kuzaa tunazaa.

Mhe.Spika, naomba pia nimshukuru Mhe.Saleh Nassor Juma kwa mchango wake ambao alielekeza katika kuunga mkono mswada huu, ambapo amesema kuwa mswada huu utaipa hadhi nchi yetu na mimi nakubaliana nae. Pia alitaka mswada huu uwe kuanzishwa Baraza letu la Mitihani kama walivyosema wajumbe wengi ambao wamechangia.

Pia alishauri wajumbe wengine waongezwe kama vile Mkurugenzi wa Idara ya Elimu ya Msingi na Mkurugenzi wa Mafunzo ya Ualimu. Mawazo haya ni mazuri, lakini tuliona kuwa bodi yetu itakuwa kubwa sana, na tunaweza kushindwa kuihudumia kikamilifu inaweza ikashindwa kufanya kazi kwa ufanisi. Idadi ya wajumbe 11 tunaona ni idadi ya kutosha, kwa hivyo Mhe.Spika, namuomba mheshimiwa akubaliane na sisi idadi hii ya wajumbe iwe kama vile ambavyo imeonekana katika mswada huo.

Mhe. Spika, baada ya hapo naomba kuwashukuru wajumbe wote ambao wamechangia na naunga mkono hoja hii.

Mhe.Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe, na pia kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuchangia Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Upimaji na Tathmini ya Elimu Zanzibar.

Mhe.Spika, napenda kumshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mchango wake alioutoa na kusaidia kutoa ufafanuzi wa hapa na pale.

Ninachopenda kumwambia Mhe.Naibu Waziri wangu ni kwamba amshukuru Mwenyezi Mungu, kwa vile amemjaalia kupata nafasi ya kujifunza namna ya kuendesha wizara.

Mimi nashukuru sana kwamba Mhe. Naibu Waziri amejifunza vizuri sana namna ya kuendesha wizara, na kwa kweli alikuwa msikivu, hashindani, habishani, maana alikuwa anajua kwamba anahitaji kupata elimu.

Siku moja niliwahi kuwa Wete tukizungumza na Walimu Wakuu, akazungumza yeye baada ya kukaa nikawaambia huyu kijana mpeni msaada mkubwa sana, anaweza akaja kuwa waziri kamili huyu kutokana na uwezo wake alionao. *(Makofi)*

Kwa hivyo, mimi nashukuru sana kwamba ni msikivu sana, na ni mtu ambaye kidogo anajifunza vizuri, anasikia vizuri sana na anafahamu anavyoelekezwa vizuri sana kwa hiyo namtaka asiwe na wasi wasi, alichokwishakipata nina hakika na kwa Mhe. Ali Juma Shamuhuna atakipata, na atafanikiwa mbele zaidi katika masuala ya kujielimisha asiwe na wasi wasi.

Mhe.Spika, hivyo ndivyo kazi zetu zinavyokwenda, na sisi tulijifunza hivyo hivyo kwa tuliowakuta wakatupa madarasa na walitufundisha na wakatuelekeza mpaka tukawa tunaweza kuteua maneno ya kusema katika chombo hichi na kujua yepi tuyawache katika chombo kama hichi.

Mhe.Spika, mswada wangu ulichangiwa na jumla ya Waheshimiwa Wajumbe 21 naomba niwataje kwa kumbukumbu.

1. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
2. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
3. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
4. Mhe. Hassan Hamad Omar
5. Mhe. Salmin Awadh Salmin
6. Mhe. Fatma Mbarouk Said
7. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
8. Mhe. Suleiman Hemed Khamis

9. Mhe. Ussi Jecha Simai
10. Mhe. Panya Ali Abdalla
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman
12. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
13. Mhe. Rufai Said Rufai
14. Mhe. Mussa Ali Hassan
15. Mhe. Hija Hassan Hija
16. Mhe. Hamza Hassan Juma
17. Mhe. Mohammed Haji Khalid
18. Mhe. Saleh Nassor Juma
19. Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Mhe.Spika, kuna wajumbe wengine walichangia kwa maandishi. Kwanza naomba kumshukuru sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kwamba mbali ya michango aliyoitoa kwa kuzungumza, lakini pia alinileta na michango ya kunifahamisha yale mambo kwa maandishi kabisa. Namshukuru sana Mhe. Jussa kwa jitihada ile ambayo imesaidia sana kufahamu zaidi. Maana kuhifadhi mara moja sio rahisi, lakini aliona hivi vipengele ambavyo ameona vina matatizo, basi ni vizuri niviandike, basi aliviandika na alinikabidhi.

Wengine waliochangia kwa maandishi ni;
20. Mhe. Asha Abdu Haji
21. Mhe. Abdi Mosi Kombo na
22. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa.

Mhe.Spika, wote hawa nawashukuru sana, na kwa kweli michango yao ilikuwa ni michango ya maana sana katika mswada huu, nina mategemeo makubwa kwamba michango waliyoitoa ile tukiiweka katika sheria hii, basi hii sheria itakuwa nzuri sana, na kwa kweli itatekelezeka vizuri sana. Nakubaliana nao kabisa moja kwa moja.

Mhe.Spika, Mhe. Mwenyekiti yeye alianza kuzungumzia kwa niaba ya kamati yake ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, na alitoa rai moja nzuri sana ya kuanzishwa kwa kiwanda cha kuchapisha mitihani hapa Zanzibar. Mhe.Spika, ni wazo zuri na wizara inalichukulia kama ni hatua ya muda mrefu na kama hali ya fedha itaruhusu, basi tutaanzisha kiwanda cha kuchapisha mitihani hapa hapa Zanzibar. Lakini ni jambo ambalo linatakiwa kuwa na wafanyakazi mahiri sana, wafanyakazi waaminifu, wafanyakazi watakaoweza kuifanya kazi hii bila ya kutoa siri ya namna yoyote, kwa sababu kuchapa mitihani ni kitendo cha siri sana, hakitakiwi kila mtu akijue. Lakini hata hivyo ni wazo zuri, basi tutafikiria huko mbele tufanye kitu gani *Inshaallah*.

Halafu alitaja kuainisha utaratibu maalumu wa kutoa matokeo ya mitihani. Hadi hivi sasa wizara Mhe. Spika, inatangaza matokeo ya mitihani kwa njia ya redio, na wakati mwengine huchapishwa kwenye magazeti. Vile vile wizara hutangaza matokeo yake katika tovuti yake iliyoanzishwa hivi karibuni. Bodi itakapoundwa rasmi, itaandaa utaratibu mzuri wa kutoa matokeo ya mitihani na kuyafikisha maskulini. Mbali ya kutoa matokeo bodi itawatunuku vyeti na stashahada watahiniwa waliofaulu. Hivi sasa wanafunzi wanaofaulu mitihani ya kidato cha pili, hawatunukiwi vyeti vya bodi, bali hutumia vyeti vya kumalizia masomo vinavyotolewa na skuli zao.

Mhe.Spika, uteuzi wa wajumbe wa bodi. Mhe.Mwenyekiti ametutanabahisha hapa kwamba ukiacha Mwenyekiti wa Bodi na Mkurugenzi wa Bodi, wajumbe waliobakia huteuliwa na waziri. Suala hili mwakilishi katika bodi ya wajumbe wa vyombo vya usalama, mjumbe huyu yumo, bahati mbaya amesahauliwa kutajwa katika rasimu ya Kiswahili, lakini ametajwa katika rasimu ya Kiingereza.

Mhe.Spika, uwezo wa kuchunguza na kuthibitisha vyeti kutoka taasisi. Wizara haina pingamizi juu ya suala hilo, suala hili liliingizwa na kamati na sisi tunalipokea vizuri. Mhe.Spika, nataka hapa kidogo wajumbe wafahamu kwamba, ni vyeti gani tunavyovichunguza. Anaweza kuja mtu hapa, mfano anatoka Tabora au Mwanza akaja na mwanawe. Akasema mwanangu ameshasoma kule na sasa hivi anafaa kuingia hapa kidato cha kwanza. Kwa hivyo, huwa tunataka kile cheti chake tukione ili tuchunguze, tuthibitishe kwamba kweli alimaliza darasa la saba kwa ajili ya kuingia kidato cha kwanza, hivyo ndio vitu tunavyovichunguza. Wengine huja kwa ajili ya kutafuta kazi hasa na wakaja na vyeti hapa wakasema mimi nimepata kule, nimesoma katika chuo gani sijui au nimesoma sijui ufundi gani. Kwa hivyo, hii bodi kazi yake kuchukua vyeti vile na kuvifuatilia na kuona kwamba kweli ni vyeti halali, hiyo ndio kazi tutayoifanya kwa ajili ya ndani ya nchi yetu.

Mhe.Spika, mjumbe mwengine alikuwa ni Mhe. Ismail Jussa Ladhu, namshukuru sana kwa kuchangia mswada huu. Mhe.Jussa amechangia mswada huu katika ile nafasi yake ya kusoma sheria vizuri. Napenda nikiri kwamba mswada wa Kiswahili una makosa mengi kama alivyoainisha na wakati mwengine tafsiri iliyofanyika hailingani na tafsiri ya Kiswahili na maana katika lugha ya Kiingereza.Makosa aliyoyataja Mhe. Spika, naahidi tutayafanyia kazi vizuri na tutarudi katika kuyafanyia kazi vizuri makosa hayo, ili mswada huu ulingane baina ya mswada wa Kiingereza na mswada wa Kiswahili uwe sawa sawa.

Vile vile alizungumzia suala la ushirikishwaji wa wadau. Mhe.Spika, hapa nataka niseme jambo moja, suala la kuanzisha bodi hii sio suala ambalo limekuja juzi baada ya matokeo haya yaliyotokea ya wanafunzi kufutiwa matokeo yao. Ndio maana katika uwasilishaji wangu nilisema kwamba katika Sera ya elimu ya mwaka 2006 huu ulikuwa ni wajibu wa kutekeleza suala hili. Kifungu hiki cha sera ndicho kilichosababisha kumteua huyu Mkurugenzi wa bodi hii, kwa sababu tunataka tuanzishe hiki kitengo kwa vitendo sasa hivi ndio maana yake. Kwa hivyo, maoni juu ya mswada huu yalianza tangu mwaka 2009, na katika hatua hizo, wizara ilikusanya maoni ya wadau mbali mbali wa elimu kutoka mikoa yote ya Unguja na Pemba huo mwaka 2009. Rasimu ya mwanzo ilipowasilishwa katika vikao vya makatibu wakuu, walishauri kuwa ni vyema kwamba baadhi ya taasisi ziwe na sheria yake peke yake, na hayo mapendekezo yaliyotolewa na wadau siku hizo juu ya suala hili, yalizingatiwa katika kuandaa rasimu hii. Ndio maana tukaweka sheria yake peke yake badala ya kuweka katika sheria ya elimu moja kwa moja.

Pia wadau ambao ni wajumbe wa kamati ya uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwa mfano Mwenyekiti wa chama cha Walimu na Wenyeviti wa Bodi mbali mbali za elimu walichangia rasimu hii kabla ya kufikishwa katika vikao mbali mbali vya serikali, tulijadili hili na hawa ni wajumbe wetu na tuliwaalika na walikuwepo.

Mhe.Spika, napenda kumuhakikishia Mhe. Ismail Jussa kuwa rasimu hii imepata michango ya wadau wa elimu. Siwezi kukataa kwamba pengine kuna wengine wachache tumewaacha hatukuwaalika, lakini mchango wake utasaidia katika kufanikisha nyengine, na tukawaalika wengine wengi zaidi, hicho ni kitu muhimu sana. Tushirikiane katika mambo yetu. Nakubaliana na ushauri wake.

Mhe.Spika, kuhusu bodi kutoa shahada. Bodi hii haitakuwa na mamlaka ya kutoa shahada, mamlaka yake ni kwa utoaji wa vyeti vya ngazi ya elimu ya lazima na vyeti vya stashahada ya ualimu. Vyuo vikuu ndivyo vyenye mamlaka ya kutoa shahada kwa mujibu wa sheria ya vyuo vikuu, huko ndiko wanakotoa shahada hizo, sisi tutatoa hizi ngazi za mwanzo tu. Mhe.Spika, hapa nataka kufahamisha kwamba, hii bodi tunayoianzisha, tumeiita *bodi ya tathmini na upimaji*, kwa sababu sasa tunachotaka kufanya ni kwamba tuitathmini elimu kuanzia chekechea. Je hiyo elimu inayotolewa chekechea inamjenga mtoto, hiyo kazi ya kwanza.

Mhe.Spika, kazi ya pili tuitathmini kuanzia darasa la kwanza. Je, hiyo elimu tunayoitoa darasa la kwanza mpaka darasa la saba, inamjenga mtoto vizuri katika kufahamu elimu hii. Hapa ndio linakuja lile suala ambalo Mhe.Rashid Seif alilizungumza, suala la kushughulikia matatizo yanasababishwa na nini. Pengine matatizo yanasababishwa na kutokuwa na *furniture*, watoto kuandika chini au watoto kutokupata walimu wazuri, hii ndio tathmini ambayo tutakuwa tunaifanya kwa ajili ya kutathmini elimu hapa Zanzibar, ili kiwango chetu cha elimu kiwe kizuri zaidi kuliko ilivyo hivi sasa, hiyo ndio shabaha ya bodi hii.

Mhe.Spika, uteuzi wa wajumbe wa jumuia ambao unafanywa na waziri baada ya kushauriana na jumuia zenyewe, huo ndio ukweli. Kwa kweli waziri hatotaja tu kwamba wewe kutoka jumuia fulani ingia katika bodi hii, tutashauriana na hizo taasisi zinazohusika na hizo jumuia zenyewe watatuletea jina, *of course* wenyewe watatafuta *modality* au njia ya kuweza kuwapata hao watu wale ambao tunawataka tuwaingize katika bodi hii.

Mhe.Spika, kuhusu Mwakilishi wa Baraza la Mitihani la Tanzania, kama vile uteuzi wa wajumbe wanaowakilishi jumuia mbali mbali, ni vyema zoezi lenyewe likapewa fursa ya kumpendekeza mwakilishi wao kwa waziri, na waziri akafanya uteuzi kwa njia hiyo hiyo, ndio tutajenga mashirikiano na kunufaika kutokana na uzoefu na utaalamu wao.

Mhe.Spika, tunao wajumbe hapa Zanzibar ambao wanaingia katika Baraza la Mitihani na wanaingia katika Baraza la Mitihani la Tanzania kwa nafasi zao. Ni wale wakurugenzi, kama kamishna wa elimu anaingia kule, mkurugenzi

wa hii bodi anaingia kule na anaingia kwa nafasi yake. Kwa hivyo, michango ya kule tunaipata na hapa ndani wamo vile vile. Kwa hivyo, hawa kutoka katika Baraza la Mitihani Tanzania tunao tayari ndani, isipokuwa huyo mmoja ndio tunamshirikisha kuingia katika bodi hii kwa ajili ya kupata michango zaidi. Mhe.Spika, uzoefu ni kitu muhimu sana, kwa sisi tunaoanza ni vizuri tukapata uzoefu kwa wenzetu kwenye masuala haya.

Kifungu cha 9(1) kuelezea bayana maslahi, sababu za kimsingi za kuweka, isipokuwa tu pale ambapo bodi itaelekeza vyenginevyo, Mhe. Ismail Jussa alisema sehemu hii itolewe. Mimi ningependa kumuomba ili kuwapa nafasi bodi kushughulikia masuala yake vizuri, basi ningemuomba sehemu hii tusiitowe iendelee kuwepo. Maelezo hayo yamewekwa ili kuipa bodi uwezo wa kuzingatia kwa kiasi gani ushiriki wa mjumbe unaweza kuathiri maamuzi, pale ambapo pameweza kuathiri, basi bodi inaweza kumtaka asishiriki au asipige kura. Mtu wa *declare interest*, bwana hee! Tunazungumza habari ya mitihani, lakini mwanangu kafanya mtihani, kwa hivyo ukishapitisha maamuzi hayo mimi itakuwa tabu kidogo. Kwa hivyo, anaweza akaombwa kidogo, usishiriki katika maamuzi yetu kwenye suala hili kwa sababu wewe ni *interest part* kwenye masuala haya. Tunaweza tukakubali.

Kwa hivyo, namuomba Mhe.Mjumbe hii aiache ili tuweze kupata nafasi bodi ifanye maamuzi, kuliko tukaweka *strict* kwamba wewe toka, tunaweza kukosa *quorum* wakati mwengine. Zanzibar tumezaliana hapa sisi kwa sisi. Kwa kweli hata wajumbe wanapozungumza suala la kwa nini Zanzibar tumeathirika sana na matatizo haya ya mitihani, mimi nasema pengine tumeathirika sana kwa sababu ya kujuana sana.

Mhe.Spika, mtoto wa Mhe. Hamza Hassan, anapoambiwa kuna karatasi ya mtihani imevuja, basi ana marafiki zake anawapelekea na hao anaowapelekea wana marafiki zao wanawapelekea, na hao nao wana marafiki zao wanawapelekea. Kwa hivyo, hapa inasambaa upesi zaidi kuliko Bara kutokana na mahusiano yetu. Kwa hivyo, karatasi moja ya mtihani inaweza ikasambaa pengine katika skuli tatu au nne, kwa sababu watu wanajuana ndio hao kwa hao. Sisi hapa tumechanganyika tuko hao kwa hao, hivyo utakuta athari hii imetupiga sana sisi kwa huku kujuana kwetu.

Mhe.Spika, katika hali hiyo ndio tunapata haya. Kwa hivyo, hata katika bodi hii, tunaweza tukasema kwamba mwenye *interest* asishiriki hasa. Sasa ukisema asishiriki hasa, hata katika kutoa mawazo tunaweza tukapata matatizo, bora asipige kura wakati tukifika kwenye uamuzi wa kupiga kura. Maelezo haya yamewekwa katika bodi mamlaka ya uamuzi kwa kuzingatia kesi yenyewe. Kwa mfano, kuhusu usimamiaji wa mitihani, wakati mwengine ni vigumu kupata wasimamizi ambao hawana uhusiano kabisa na baadhi ya watahiniwa kutokana na mazingira ya nchi yetu, katika mazingira hayo, bodi inaweza kutoa ruhusa kwa mtu huyo, lakini wakati huo huo kuandaa mazingira ya kumuangalia. Kifungu hiki kinaipa bodi mamlaka ya kupima uzito wa suala lenyewe na mazingira, badala ya kufunga moja kwa moja.

Mhe.Spika, kuhusu kifungu cha 24(1) na (2) kufuta na kubakisha kanuni. Busara ya kufuta kifungu cha 24(1) na kumpa changamoto waziri achukue hatua za haraka kwa kuandaa kanuni mpya. Mhe.Spika, sheria tunazozitunga hapa huwa tunazifuta, lakini kanuni hatuzifuti, hii inapelekea kidogo uvivu wa kuandika kanuni mpya. Kwa sababu kanuni kama haikufutwa basi ile kanuni inaendelea kutumika. Kwa hivyo, bora uifute ili waziri sasa awe hana chengine cha kufanya isipokuwa atunge kanuni mpya, hii inaharakisha utungaji wa kanuni mpya. Ndio maana tukasema hizi kanuni zilizokuwa katika sheria hii zifutwe, zikifutwa sasa waziri atakuwa hana kanuni, hawezi kuzitumia zile kanuni. Kwa hivyo, itabidi akae kitako na watu wake atunge kanuni mpya, ili ziweze kufanya kazi, ndio maana tukasema bora zifutwe, maana zikibakia zinachelewa. Mhe.Spika, tuna sheria nyingi tumepitisha hapa, lakini kanuni hazijatungwa. Ukiuliza unaambiwa ipo kanuni ya zamani tunaitumia, basi inakuwa ni matatizo.

Vile vile Mhe.Spika, napenda kumshukuru Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa kutoa mchango wake wa maandishi kama nilivyokwishasema mwanzo. Nakubaliana na mchango wake wa kuongeza maneno katika kifungu cha 22(2) (j) cha mswada kinachohusu viapo, makosa na adhabu kwa kuongeza maneno.

Kuhusu mswada wa kuanzisha Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu. Suala hili nakubaliana nalo na hivi sasa liko katika maandalizi. Pia nimeupokea na kuukubali mchango wake wa marekebisho ya kifungu cha 5(a) kuhusu uzoefu na sifa za mwenyekiti wa bodi. Tunayachukua mapendekezo yake ya kuwa sifa za kuwa mwenyekiti awe na shahada ya elimu pamoja na uzoefu wa miaka 7 badala ya miaka ile tuliyoitaja pale kwenye sheria.

Namshukuru sana Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kutokana na mchango wake kuhusu pendekezo lake la mwenyekiti wa bodi hii asiwe miongoni mwa wanasiasa. Nakubaliana naye mia kwa mia. Tutajitahidi lakini ni kazi

ngumu kidogo maana wengine hawafichi, hujificha dakika tano wakafunguka baada ya dakika 2, sasa hilo ndio tatizo.

Kuhusu shahada ya digrii kwa mwenyekiti iliyokusudiwa ni shahada katika fani yoyote katika chuo kikuu kinachotambuliwa. Suala jengine mkurugenzi kuwa muaminifu na muadilifu. Sifa hii huzingatiwa katika uteuzi wa viongozi mbali mbali, hata kama haikutajwa kwenye sheria. Hilo tutajitahidi sana kuchunguza.

Kuhusu ufafanuzi wa bodi kufanya mitihani ya 'O' na 'A'. Kama nilivyotangulia kusema bodi hii itashughulikia upimaji wa tathmini kwa ngazi ya elimu ya lazima, kwa kuanzia bodi itaendelea kushughulikia mitihani ya darasa la saba, kidato cha pili na pia itaendelea na utaratibu wa upimaji kuanzia elimu ya maandalizi, ngazi mbali mbali za msingi na sekondari. Kuhusu mitihani ya kidato cha nne na kidato cha sita utaendelea kufanywa na Baraza la Mitihani la Tanzania, hadi hapo itakapofika hatua ya kuridhika kuwa bodi imeshapata uzoefu wa kutosha na kuna haja ya kufanya mitihani yake yenyewe katika ngazi hiyo.

Mhe.Spika, kuhusu adhabu na makosa mbali mbali. Nakubaliana na mawazo yake. Mhe.Spika, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ilishauri kurekebisha kifungu cha 22(2)(j) na adhabu itakuwa kulipa faini isiyopungua milioni moja na isiyozidi milioni tano, sio laki tatu tena, kamati iliongeza hapa au kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitano, hizo ndio adhabu ambazo zitatumika. Nawashukuru sana wajumbe wa kamati kwa kazi hiyo waliyoifanya nzuri.

Mhe.Spika, kuhusu posho la wajumbe, kikawaida posho watakazolipwa wajumbe huwa haziainishwi katika sheria. Kiutaratibu bodi huwasilisha mapendekezo ya posho kwa waziri na yeye ndiye anayetoa maamuzi kutokana na uwezo wa kifedha, kwa hivyo inakuwa hazitajwi kuwa posho inakuwa ni kiasi gani.

Mhe.Hassan Hamad Omar, alishauri wizara kujipanga vyema katika uanzishaji wa bodi. Napenda kumuhakikishia kwamba wizara imejipanga vyema juu ya kuanzishwa kwa bodi hii, na inayachukua mapendekezo mbali mbali yanayotolewa na Wajumbe wa Baraza hili tukufu na kuyafanyia kazi.

Mhe.Spika, kuhusu kujitoa katika Baraza la Mitihani.Mhe.Spika, wizara haina nia ya kujitoa katika Baraza la Mitihani, bali litazidisha mashirikiano baina ya vyombo hivi kama ilivyoelezwa katika sheria hii. Pindipo ikitokea migogoro itasuluhishwa kwa kufuata taratibu zilizopo. Napenda kukiri kuwa Baraza la Mitihani la Tanzania limefanyakazi kubwa katika ufanyaji wa mitihani na utoaji wa vyeti mbali mbali kwa wanafunzi wetu wengi. Uzoefu na utaalamu wao bado tutauhitaji. Mhe.Spika, hili suala la kuvuja mitihani na kadhia iliyotokea. Mhe.Spika, wajumbe wasiwe na wasi wasi nitalizungumza mwisho nitakapofika.

Mhe.Salmin Awadh Salmin, alizungumzia kuhusu adhabu ya wanafunzi kufutiwa mitihani ya kidato cha nne, suala hili nitalitolea ufafanuzi kwa pamoja na hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wengine waliochangia kwenye suala hili mwisho wa mazungumzo yangu.

Mhe.Spika, kuhusu kuanzishwa kwa Baraza la Mitihani la Zanzibar. Mhe.Spika, kutumia jina la Baraza sio lazima na jina bodi litatumika sana tu na wala halipotezi maana ya chombo kilichokusudiwa. Mfano mzuri, tunayo bodi ya mikopo ya elimu ya juu, chombo hicho kimeundwa hakina tofauti na bodi ya upimaji na tathmini ya elimu. Kwa hivyo, kwetu sisi chombo chetu kitajulikana kama ni bodi ya upimaji na tathmini ambayo itashughulikia sio tu na mitihani, bali pia na masuala ya tathmini ya elimu. Kimtazamo bodi ya upimaji na tathmini ni zaidi kuliko kushughulikia masuala ya mitihani.

Mhe.Mwanasheria Mkuu, alitoa ufafanuzi mzuri tu jana katika mchango wake. Kuhusu kazi za katibu wa bodi. Katibu wa Bodi hii atakuwa na taaluma ya sheria na pia atakuwa ni mtendaji katika chombo hiki anayeshughulikia masuala ya kisheria katika bodi. Yeye hatokuwa ni mjumbe bali majukumu yake ni kuandaa kumbukumbu za vikao vya bodi. Maana vikao vinaitishwa na mwenyekiti akishauriana na mkurugenzi au wakati mwengine wajumbe wanapoomba haja ya kufanya kikao.

Kuhusu kuanzishwa kwa kamati za bodi. Nakubaliana na mapendekezo ya Mhe. Mjumbe kwa kifungu cha 14 kifanyiwe marekebisho, natoa na kijifungu kidogo (1) na kijifungu kidogo cha (2) katika kifungu cha 14(1) isomeke, bodi itaanzisha kamati kwa madhumuni ya kusaidia katika utekelezaji wa kazi zake. Katika kifungu kidogo cha 14(2) isomeke, bodi inaweza kuanzisha kamati nyengine kama vile bodi itaona inafaa kila baada ya muda. Kifungu

hicho kitafuatiwa na kifungu kidogo cha 4(3), nakubaliana na ushauri wa Mhe. Salmin Awadh Salmin kama alivyoshauri.

Mhe.Suleiman Hemed Khamis, namshukuru Mhe. Mjumbe kutokana na mchango alioutoa kuhusu suala zima la kuimarisha ubora wa elimu yetu. Napenda kumuhakikishia kuwa moja wapo ya madhumuni ya kuanzishwa kwa sheria hii, ni kuhakikisha kuwa Zanzibar inatoa elimu iliyo bora, na inayolingana na vigezo vya kimataifa. Nakubaliana na yeye kwamba mara tu baada ya sheria kupitishwa na kuanza kutumika basi kanuni nzuri tu ziandaliwe. Namuhakikishia kuwa tumeshajiandaa kwa hilo na tutaanza kuandaa kanuni katika maeneo yaliyoainishwa katika kifungu cha 23(2) cha sheria hii.

Vile vile aliuliza juu ya lengo letu kuhusu upimaji na tathmini ni nini. Lengo hasa kama lilivyotajwa ni kuweza kupimwa kwa kiasi gani skuli zetu zimefanikiwa katika kuyafikia malengo ya elimu yaliyopangwa na kama hayakufikiwa, ni hatua gani zichukuliwe katika kurekebisha dosari zitakazoonekana. Kwa kufanya upimaji na tathmini ndio tutaweza kutambua dosari za mipango yetu ya elimu.

Mhe.Spika, kuhusu kufutwa kwa matokeo ya mitihani hilo nitalizungumza kwa jumla. Mhe.Fatma Mbarouk Said, namshukuru Mhe. Mjumbe kwa mchango wake alioutoa, aliulizia kuhusu mjumbe wa nafasi maalumu anatokea wapi. Hii imekusudiwa kuwa ni mjumbe anayeingia katika bodi kutokana na cheo chake, kama ilivyotajwa katika hiyo sheria. Huyo atakuwa kaingia katika nafasi maalumu. Maana yake akiondoka katika kile cheo tu basi kwenye bodi hii yeye sio mjumbe tena, kwa sababu ile nafasi ndio hana. Anayeteuliwa ndiye anayeingia katika bodi hii.

Mhe.Spika, pia wizara imeangalia mfumo wa elimu na chombo hiki kitasaidia kukuza elimu katika nchi yetu, kwa sababu upimaji na tathmini itafanywa kwa ufanisi zaidi hasa ikisimamiwa na chombo huru. Pia alitaka kujua vyuo ni vipi. Vyuo maana yake ni vyuo vya ualimu vya Zanzibar vinavyotoa mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti na diploma, ndivyo ilivyokusudiwa. Mhe.Mjumbe hakuwa na maswali mengi, maelezo mengine aliyotoa ilikuwa ni mchango tu ambao tunaupokea.

Mhe.Spika, Mhe. Abdalla Mohammed Ali, mbali na mchango alioutoa, aliulizia kuhusu mitaala inayotumika alitaka kujua hasa kwa nini kuna tofauti ya mitaala, ni kweli kuwa mitaala inayotumika katika ngazi ya maandalizi na msingi ni tofauti kati ya mitaala yetu na ile ya Tanzania Bara. Tofauti hiyo inatokana na kuwa mitaala ya ngazi hizi zaidi inaangalia mazingira yetu halisi kwani katika ngazi hizi za elimu ndio tunawaandaa vijana wadogo ili kukabiliana na mambo mbali mbali, hivyo ni vizuri kuelewa mambo muhimu yalioko katika mazingira yao. Hata hivyo, tofauti ya mitaala haimaanishi kuwa mitaala yetu ni dhaifu.

Katika elimu ya maandalizi na msingi, tumeandaa mitaala mipya hivi karibuni ambayo inaendana na mfumo wetu wa elimu, ambapo elimu ya lazima inaanzia ngazi ya maandalizi ya miaka miwili, na elimu ya msingi ya miaka sita. Mitaala ya elimu ya sekondari ni sawa sawa kati ya mitaala yetu na ile inayotumika Tanzania Bara. Kwa hivyo, kuanzia kidato cha kwanza kwendea huko tunatumia mtaala mmoja hapa kwetu na skuli za Tanzania Bara.

Mhe.Spika, kuhusu skuli binafsi kufanya mitihani hii. Mhe.Spika, mitihani hii itakayoandaliwa na bodi itahusisha skuli zote iwe binafsi au serikali, kama rasimu ya sheria inavyobainisha. Chombo hiki ndicho kitakachokuwa na uwezo wa kutoa vyeti rasmi, hivyo wanafunzi wote watapata nafasi ya kutahiniwa na watakaopasi watatunukiwa vyeti. Mtu akisema kwamba aah! Mimi sitaki kutumia utaratibu huu, basi ni hiyari yake, atakuwa anasomesha watoto ambao watakuwa hawana vyeti vinavyotambuliwa. Vyeti vitakavyotolewa na bodi hii ndivyo vyeti vitakavyotambuliwa.

Mhe.Ussi Jecha Simai, yeye alishauri kuwa chombo hiki kiitwe Baraza la Mitihani la Zanzibar, kama nilivyotangulia kujibu kuwa hakuna lazima ya kuita Baraza la Mitihani, jina lililochaguliwa linakidhi haja ya sheria hii hasa ukitilia maanani kwa chombo chetu hakitoangalia mitihani tu, bali kitahusika katika ufanyaji wa tathmini ya elimu yetu, ni chombo ambacho kitatathmini elimu kwa jumla. Kuhusu mitaala ya elimu. Nimeshajibu swali hili kuwa mitaala yetu ya maandalizi na msingi imepitiwa hivi karibuni na mitaala hiyo ni mizuri na hakuna haja ya kukhofu kuwa labda ina kasoro. Hata hivyo wizara inakiri kuwa kuna changamoto nyingi katika kuinua ubora wa elimu yetu, kama vile uhaba wa vifaa vya kufundishia, wingi wa wanafunzi ukilinganisha na madarasa, walimu wa kutosha. Changamoto hizi tutaendelea kupambana nazo na kusogea hatua kwa hatua kwa kadiri ya uwezo wetu.

Mhe.Spika, katika hili mimi naona nimeanza kuona muangaza mzuri kidogo, nafikiri matatizo yatapungua kwa muda mfupi, mambo ya *furniture*, mambo ya walimu ni kwa muda mfupi tu yatapungua, kwa sababu nimeshaanza kuona kumeanza kuchomoza hali ya hewa kidogo nzuri juu ya masuala haya.

Mhe.Spika, waziri mwenzangu aliyekamata wizara hii atakuja kuyachambua haya mambo ambayo tayari yameanza kujichomoza, ambayo ni mazuri sana kutatua matatizo haya ya mabanda yetu na mambo mengine.

Kuhusu sifa za wajumbe wa kamati. Kamati ya bodi itakuwa na wajumbe watakaoteuliwa kuwa ni wajumbe wa bodi ya upimaji na tathmini, ambayo jumla yao ni 11, baadhi wanateuliwa kwa mujibu wa dhamana zao na wengine ni wawakilishi wa jumuia zao, kama ilivyo katika kifungu cha 4(1) mpaka (j) kinavyoonesha. Kuhusu kuongezwa kwa adhabu, hilo tayari nimelifanyia kazi kama Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza hili iliwashauri.

Mhe.Panya Ali Abdalla, na yeye alishauri kuwa chombo hiki kiitwe Baraza la Mitihani. Suala hili tayari nimelitolea ufafanuzi. Pia napenda ifahamike kuwa mswada huu haukuja kwa sababu ya kufutiwa wanafunzi wa kidato cha nne matokeo. Maamuzi ya kuanzisha bodi ya upimaji tathmini ya elimu yaliyokua yameshafikiwa zamani tokea kuanza kwa Serikali ya Mapinduzi ya Awamu ya Saba, ndio maana mkurugenzi wake, alikwishachaguliwa na Mhe. Rais siku nyingi, hivyo sio sahihi kuhusisha kuanzisha kwa chombo hiki na kufutiwa wanafunzi wa Zanzibar matokeo yao kutokana na udanganyifu, kuhusu kutekelezwa kwa adhabu kama ilivyopangwa. Napenda kumuhakikishia Mhe. Mjumbe kuwa adhabu hizo zitatekelezwa pindipo makosa yatatendeka.

Mhe.Rashid Seif Suleiman yeye ameshajibiwa na Naibu Waziri, na Mhe. Abdalla Juma Abdalla pia ameshajibiwa na Naibu Waziri, Mhe. Rufai Said Rufai, Mhe. Mussa Ali Hassan, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Saleh Nassor Juma, wote hao michango yao imeshapokelewa. Vile vile wale waliochangia kwa maandishi michango yao tumeichukua na tutaifanyia kazi kama kawaida.

Mhe.Spika, nataka kusema jambo moja ambalo linahusu tatizo la wanafunzi kufutiwa mitihani. Mhe.Spika, tatizo hili ni la muda mrefu, limeanza siku nyingi na inaelekea vijana wetu walilizowea na vijana wetu walipunguza kasi ya kujisomea na wakawa wanajiandaa kungojea kuvuja kwa mitihani.

Mhe.Spika, nilikuwa nikiwaambia kila nilipopata nafasi, jamani tabia hii ya kungojea kuvuja kwa mitihani iwacheni itawaleteeni matatizo mbele ya safari. Mhe.Spika, mwaka sikumaliza haya matatizo yametokezea. Aliyoyasema Mhe. Naibu Waziri wangu ni kweli yapo. Kwa hivyo, nasema hivi, hata kama tutafika wakati wa kuanzisha Baraza letu la Mitihani hapa, kwa mujibu wa taratibu zetu tusije tukaruhusu utaratibu huu wa wanafunzi kukopia. Katika hili tutaharibu umadhubuti wa elimu yetu hapa Zanzibar na tutakuwa tunatoa wataalamu ambao kwa kweli watakuwa *fake*. *(Makofi)*

Mhe.Spika, nawaomba sana wazee walizingatie sana suala hili, kuruhusu wanafunzi kufanya mitihani kwa kungojea kuvuja, kunasababisha kutoa wataalamu wasioziweza kazi, wakati sisi tunataka tutoe wataalamu wa kweli. Kwa maana hiyo, tunataka turejeshe sifa ya wataalamu wa Zanzibar. *(Makofi)*

Kwa mfano, wataalamu wa Zanzibar ambao wako nje wanatajikana vizuri, tena ni wataalamu wazuri tu, yaani huwezi kuamini kama tunao wataalamu wa Zanzibar ambao wako kwenye Kampuni za *SCANIA* wanavumbua na kutengeneza gari kubwa. Lakini walisoma vizuri na wamepita katika Chuo chetu cha Mbweni hapa na wamepata utaalamu na wamekwenda mbele na kujiendeleza, basi wao ni wataalamu wazuri sana. *(Makofi)*

Vile vile kuna madaktari wengine wako Zaire, Uarabuni wamefungua hospitali, tena wanategemewa na hata wale wenyewe waliopo pale, kwa sababu walisoma vizuri. *(Makofi)*

Sasa leo unamruhusu mtoto akakopie na wala hatilii mkazo kusoma, kwa sababu anajua siku itafika atakopia. Kwa hivyo, hana wasi wasi wa kusoma, ndio unakuta haya matatizo ambayo tuliyoyakuta kwenye *script* zetu za mitihani, mwalimu au sijui nani amempa kikaratasi mtoto ajaze, kikaratasi hiki ndio maswali yenyewe na hili ndilo swali No. 7 au 8 ukifika lijibu.

Mhe.Spika, ni *fill the black*, yaani ujaze katika pengo panapo *sheep* uandike *ship*, basi mtoto anaandika na ukimaliza mpe mwenzio. Hivyo, mtoto anachukua karatasi ile na kuandika kwenye daftari lake la Kiingereza panapo *sheep*

andika *ship* ukimaliza mpe mwenzio. Kwa kweli inasikitisha *yes* imetokezea na Wajumbe wa Kamati wamekwenda wameona, yaani inasikitisha. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, huyu mtoto alikuwa tayari amekwisha kuji-*tune* katika kukopia, kwa hiyo anachopewa kwenda kukopia anakikopia vile vile kilivyo, karatasi ya Kiingereza chini anaandika ukimaliza mpe mwenzio, ndivyo ilivyoandikwa mule, ina maana yule Kiingereza hajui au anachokiandika hakijui, lakini yeye yuko katika kukopia. Kwa kweli haya ndio matatizo na tumeyaona. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe.Spika, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na wazee wanaonisikiliza, kwamba watahadhari sana katika kuwa-*encourage* watoto kwa kuwanunulia mitihani kwa kuambiwa hii mitihani imevuja, waache tabia hiyo na badala yake wawahimize kusoma. *(Makofi)*

Mhe.Spika, wamefutiwa mitihani watoto ambao kwa kweli ni mahodari na akili zao zinafanyakazi vizuri, lakini waliingia katika dimbwi hili la matatizo. Kwa kweli kama wangelijibu maswali kwa kutumia akili zao wenyewe, basi wangepasi lakini wametumbikishwa. *(Makofi)*

Kwa mfano, kuna mwanafunzi mmoja aliniuliza na kuniambia kwamba Mhe. Waziri nataka niulize, nilimwambia haya niulize, hivi akikujia mwenzio na karatasi ya mtihani na kukwambia huu ndio mtihani wenyewe na unauzwa shilingi 30,000/= hutomnunulia ah! Nikamwambia mimi nisingemnunulia, nikamuuliza kwani wewe umenunua, aa! Nakuuliza tu mwalimu. Mhe.Spika, ameondoka kwenye uheshimiwa na kuja kwenye uwalimu na hili ndilo tatizo Mhe.Spika.

Mhe.Spika, namshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa maelezo yake aliyotoa kwenye masuala ya jina. Hata hivyo, alisema neno moja ambalo nataka niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe, kwamba hii ni mbegu inaweza kumea au kuvia, lakini tuichukue mbegu hii na tuanzishe hii Bodi kwa jina hili na tutatizama mbele ya safari, basi ikimea na tukifuata sheria pamoja na taratibu nadhani tutafika mahala na kuanzisha chombo chetu wenyewe hapa, lakini tusi-*rush* hivi sasa tunaweza kujitia kwenye matatizo.

Vile vile alisoma kifungu cha Katiba kwamba *item* ya 16 inazungumzia Baraza la Mitihani pamoja na yanayohusiana nayo, sasa ndio unakuja mambo ya vyeti na mengine.

Mhe.Spika, sisi tunataka watoto wetu wafanye kazi Zanzibar, Tanzania Bara, Uganda, Kenya, Rwanda, Burundi, kwa sababu tunayo *East African Community* tuwaachie watoto wetu wafike huku, na wala tusizozane hapa katika mitihani na tukafanya mitihani, na halafu ikawa haiji kutambuliwa baadae, ikawa matokeo yake cheti hicho kikawa kinatambuliwa hapa Zanzibar peke yake si uzuri.

Hili suala tunakwenda nalo na sisi tunaanzisha hii mbegu ambayo Mhe. Mwanasheria Mkuu ameielezea na tumuombe Mwenyezi Mungu azidi kutusaidia tufike mahali pazuri katika masuala haya, tusivamie. Ninakuombeni wenzangu tuwe wastahamilivu.

Sasa ninataka kuzungumzia kuhusu kufutwa kwa matokeo. Baraza la Mitihani limefuta matokeo ya Watahiniwa 3,303 waliobainika kufanya udanganyifu katika mitihani ya mwezi wa Oktoba, 2011. Kati ya watahiniwa waliofutiwa matokeo watahiniwa 2 ni mitihani ya maarifa, ni *qualified test* na watahiniwa 3,301 ni mtihani wa kidato cha nne kwa upande wa Zanzibar.

Watahiniwa wa skuli 1,010 wa skuli 30 za serikali na za binafsi wamefutiwa matokeo na watahiniwa wa kujitegemea 1,056 wamefutiwa matokeo katika vituo 36 vya kufanyia mitihani kwa Unguja na Pemba.

Hivyo jumla ya watahiniwa kutoka Zanzibar ambao matokeo yao yamefutwa kutokana na udanganyifu ni 2076. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 63.0 ya watahiniwa wote waliofutiwa matokeo yao. Kwa upande wa Tanzania Bara watahiniwa kutoka vituo 53 wamefutiwa matokeo yao.

Kwa upande wa watahiniwa wa Zanzibar, watahiniwa waliofutiwa matokeo wengi ni kutokana na udanganyifu wa kuwa na mfanano wa majibu usio wa kawaida. Hili limepingwa sana. Mfano wa majibu usio wa kawaida unapatikana vipi wanasema. Kwa sababu wanasema hawa watoto wanafanya *revision* pamoja lazima wataandika mambo yanayofanana. Hii ndio hoja inayozungumzwa.

Lakini sio mfano kama huo unasemwa. Mfanano huo ninaousema darasa zima wanaandika panapo *sheep* aandika *ship*, na mwisho ukishamaliza mpe na mwenzio, ndio mfanano huo, wote wakaandike namna hiyo? Sasa hilo ndio linakuwa ni tatizo. Unajua hasa hapa kuwa kulikuwa na mchezo umechezwa. Sasa huo unaitwa mfanano usio wa kawaida.

Udanganyifu mwengine ambao umesababisha wanafunzi wetu wengi kufutiwa matokeo, ni watahiniwa kubaibinika kuwa na *script* za maandiko tofauti au kuwa na *script* za maandiko ya somo moja, pengine kuwa na makosa yote mawili katika karatasi moja ya mtihani.

Katika *question* ya kwanza ni hati nyengine, *question* ya pili ni hati nyengine, na ya tatu ni hati nyengine. Utajiuliza wameandika vipi hawa? Ina maana kulikuwa na usimamizi dhaifu. *Of course* karatasi hizi zilikuwa zimetoka nje. Zimeingizwa katika madarasa na watu wameshaandikiwa majibu. Hilo ni tatizo ambalo pia limeonekana limechomoza pale.

Sasa kwa nini watu wakajibu nje ya darasa. Hili tatizo limegundulikana vile vile hati zinatofautiana, au wakati mwengine hati ulizoziandika katika somo la historia ni tofauti na hati ulizoziandika somo la Kiingereza. Na hili Mhe. Spika, hawa Baraza la Mitihani hawakujibu tu, walipoona mfanano huu waliwapa wataalamu wa maandishi na wakathibitisha kwa hati hizi ni hati za watu mbali mbali, kutoka Polisi wamethibitisha masuala haya hazikufanana. Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani Tanzania Dr. Joyce Ndanichako akifuatana na maafisa wa Baraza walifika Zanzibar tarehe 3 Februari, 2012 na kuwa na kikao cha pamoja na uongozi wa Wizara kuzungumzia dosari mbali mbali zilizoonekana katika mtihani wa kidato cha nne mwaka 2011. Kikao hicho kichofanyika kabla ya matokeo hayajatangazwa.

Uongozi wa wizara ulipata nafasi ya kuona mifano ya dosari zilizojitokeza, na kutoa ushauri na hatua ambazo Baraza la Mitihani lingepaswa kuchukua katika kurekebisha dosara hizo. Katika ziara hiyo Katibu Mtendaji pia alifanya vikao na Kamati za Mitihani za Mikoa ya Unguja, ambayo iliwashirikisha Makamanda wa Polisi wa Mikoa. Mikutano kama hiyo pia ilifanyika Kisiwani Pemba siku ya Jumapili tarehe 05 Februari, 2012 huko Chake Chake.

Mhe.Spika, aina za udanganyifu. Baadhi ya udanganyifu uliofanywa na watihaniwa katika vituo vya kufanyia mitihani vya Zanzibar ni hii ifuatayo:-

(a) Watahiniwa kubainika kuwa na miandiko tofauti ama kama *booklet* moja au kwenye masomo tofauti.

(b) Watahiniwa kuwa na mfanano wa majibu usio wa kawaida. Aina hii ya udanganyifu iligunduliwa kwa watihiniwa wa skuli zetu nyingi za Zanzibar, kama vile Chuo cha Kiislamu Mazizini, Chuo cha Kiislamu Pemba, Skuli ya Sekondari ya Jang'ombe, Skuli ya Sekondari ya Hamamni, Skuli ya Sekondari ya Pwani Mchangani, Skuli ya Sekondari ya Regeza Mwendo, Skuli ya Sekondari ya Mwanakwerekwe C, Skuli ya Sekondari ya Uzini, Skuli ya Sekondari ya Uzi, Skuli ya Bilal Islamic Seminary, Skuli ya SUFA, Skuli ya FILTER FEDERAL, Skuli ya Sekondari Fuoni, Skuli ya Sekondari ya High View na Skuli ya Sekondari ya Laureate.

Mhe.Spika, watahiniwa wengi wa skuli zetu walifutiwa matokeo yao kutokana na udanganyifu wa aina hii. Katika aina hii ya udanganyifu, watihiniwa waliandika majibu yanayofanana katika vipengele vyote na wote walikosa kwa jibu la aina moja. Kwa mfano, katika Chuo cha Kiislamu Micheweni swali la 1 Somo la *Physics* watahiniwa walikuwa na majibu ya kufafana katika vipengele vyote na walikosa kwa kuandika (d),(c),(a) na (b) katika maswali No. 2, 7, 8 na 10.

Mhe.Spika, namna gani unasahihisha karatasi za mwanafunzi unakuta darasa zima wamepata A na darasa zima wamepata D na darasa zima wamepata C, darasa zima wamekosa E, yaani katika yale maswali ya kukosa wamekosa wote na katika kupata wamepata wote. Hii inakuja katika mfano wa namna kama hiyo, hii ni *genius* yaani wanakosa namna kama hii na wanapata katika namna hiyo ya kufanana. Hii imeonekana kuwa ina matatizo.

Pia katika somo la physics watahiniwa waliokosa kwa kuandika F katika 2 r, katika V na O. Hapa ndipo panapo kichekesho zaidi. Hii ni *multiple choice* Mhe.Spika. Swali la kwanza majibu yake ni A basi wote wameandika A, swali la pili jibu lake ni C, basi wote wameandika C, swali la tatu jibu lake ni A basi wote wameandika A, swali la

sita jibu lake ni B, wote wameandika O, na katika ile *choice* hamna ile *letter* O, maana ile multiple *choice* kapewa jibu A, B, C au D lakini wote darasa zima wameandika O jibu la swali lile.

Sasa unajua hii O nyinyi mumeipata wapi na haimo katika hili swali. Mfano mwengine ni katika Skuli ya Kiislamu Mazizini. Katika mitihani ya somo la jiografia swali nambari moja, watahiniwa waliandika majibu ya kufanana katika vipengele vyote kumi na walikosa vipengele viwili kwa kuandika A. Katika watahiniwa walioandika majibu ya kufanana katika vipengele vyote vitano, na walikosa kwa kuandika herufi ya O ambao si moja wapo ya chaguo katika swali hilo.

Halafu kulitokea na matatizo mengine Mhe.Spika. Kuna baadhi ya *script* zilikosekana katika *papers* zile za bahasha za mitihani, zikaja zikaonekana dakika ya mwisho. Kwa kweli kuna mwanafunzi yeye nambari yake tuseme ni kumi na nane, ipo hapa. Lakini yeye ni *student* anatumia S, kaandika nambari yake S nambari ya kituo kumi na nane. Lakini kuna mtu mwengine kumuandikia E kwa maana ni *private student*, nambari yake ya kituo kile kile lakini ni kumi na nane vile vile. Kwa hivyo mwanafunzi kajibiwa na mtu mbali na yeye mwenyewe kajibu, yeye mwenyewe kajibu kama *student* na mtu aliyemuandikia kama ni private. Unakuta kuna tofauti hizo.

Walipotia katika bahasha, hii P ndio ikaingia katika bahasha ya S na hii S haikuonekana hata ilipokwenda. Waliposahihisha kule Baraza la Mitihani, wakakuta huku kuna jina moja limekosekana na S liko wapi karatasi yake lakini ipo P na nambari ni hii hii.

Mwalimu akaandikiwa yule, eeh! bwana katika katika kituo chako kuna karatasi moja ya mwanafunzi imekosekana. Baada ya siku inafika saba au nane zile, akahangaika hangaika akaipata ile karatasi haijapelekwa kule. Akaandika barua ile karatasi akaipeleka Baraza la Mitihani, wewe uliipataje hii, halafu mbona kuna mbili hizi na zote zina nambari moja na sisi hatuna mwanafunzi mwenye P mwenye nambari hii. Haya ni mambo ambayo yamefanyika katika mitihani yetu. Mwenyezi Mungu atunusuru yasitokee tena katika mitihani ijayo.
Halafu pia kuna matatizo mengine yamesababishwa na baadhi ya karatasi kama walivyosema baadhi ya Wajumbe hapa hazikupelekwa katika kusahihishwa, yaani kuna uzembe wa aina fulani tuseme kweli. Lazima wizara yangu ichukue hatua kwenye masuala haya. Ninakubaliana na Mhe. Mussa kwamba ilivyokuwa hakazani ng'ombe wa mbele asipigwe ng'ombe wa nyuma.

Tumeunda Tume makusudi ambayo nitaieleza. Kwanza hatua nilizozichukua, tuliagiza Baraza la Mitihani kuwasilisha ushahidi wote wa skuli zilizofanya udanganyifu katika mitihani kwa ajili ya kukaguliwa tena. Baraza liliwasilisha ushahidi huo kwa ajili ya ukaguzi.

Wizara iliunda kamati ya viongozi sita kupitia ushahidi huo. Kamati hiyo iliongozwa na Kamishna wa Elimu, wajumbe walikuwa ni Mkurugenzi wa Bodi Upimaji ya Tathmini, Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu Zanzibar, Mwenyekiti wa Chama cha Walimu, Mkuu wa Kituo cha Elimu cha Chuo Kikuu cha Taifa SUZA, Makamo Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar.

Ripoti yao imethibitisha kufanyika udanganyifu katika skuli zilizofutiwa matokeo. Kwa maana hiyo, tulichukua ule ushahidi wote tukawapa wenzetu hebu tizameni kweli mambo haya yamefanyika. Wakatuthibitishia kwamba kweli yamefanyika. Halafu tukamuomba Katibu Mtendaji aje afahamishe, ndio akafanya mikutano miwili ambayo amekwisha ifanya.

Halafu Baraza la Mitihani liliagiza kuanzia mwaka 2013 mitihani yote ya taifa itasimamiwa na wizara kupitia Bodi ya Upimaji Tathmini badala ya Kamati za Mitihani za Mikoa, maana hawa zamani, wizara ilikuwa inasimamia lakini Baraza la Mitihani ikasema aah! Tukawakabidhi Mikoa moja kwa moja. Kwa hivyo hilo nalo tumewaambia sasa hivi lirejeshwe na lisimamiwe na wizara moja kwa moja.

Kuna Kamati ya Maendeleo ya Baraza lako Tukufu walikuja kuniona ofisini, walikuwa wakali, mimi nikawaambia musiwe wakali, nendeni Baraza la Mitihani mukayatizame hayo mambo. Walikwenda Baraza la Mitihani, wamo humu ndani na wakayaona hayo mambo, wakaoneshwa kuwa haya ndio mambo yenyewe tunayoyazungumza. Wakathibitisha kwamba kweli kuwa hilo suala limetokea.

Kuna Kamati ya Wazee imenijia vile vile. Eeh! Bwana wee hili suala tunalifanyia kazi, nikawaambia fanyeni kazi kadri munavyofanya, piteni kila skuli munayotaka kupita muangalie lakini musimalize kazi mpaka muende katika Baraza la Mitihani nako muende mukatizame haya mambo kweli yamefanyika?

Wamepita walimopita, humo walimopita humo. Mimi ninashukuru walivyokuja wakathibitisha wakaniambia kwamba kweli kumefanyika mambo katika skuli kwa wanafunzi wenyewe tuliowahoji. Lakini wakaniambia sisi tunaomba hii miaka mitatu ni mingi kufungiwa. Hili wazo Mhe. Spika, mimi ninakubaliana na wale Kamati ya Wazee na Wajumbe wa Baraza kwamba miaka mitatu ni mingi. Ndio maana suala hili tunalizungumza na wenzangu wa Wizara ya Elimu ya Jamhuri ya Muungano.

Hivi sasa siwezi kusema ni hatua gani ambazo zitachukuliwa, lakini hata leo mwenzangu anakuja hapa tuzungumze masuala haya kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Mimi ninashukuru sana na Waziri wa Jamhuri ya Muungano tunashirikiana vizuri sana, na tunapanga mambo yetu vizuri sana, na ninategemea tutafikia uamuzi juu ya suala hili.

Kwa hivyo ninawaomba Waheshimiwa Wajumbe watuachie tulifanyie kazi suala hili. Ni kweli miaka mitatu ni mingi sana na kwa sababu hii sheria imesema hapa *I can't find to have committed examination offense shall be excluded from all future examinations said by the council*. Sasa wao hawakuondoa yote lakini wameeka miaka mitatu, ina maana kuna upekenye hapa wa kuweza kupunguza kama itayumkinika hii adhabu kutokana na hiki kifungu cha sheria kilivyo.

Mhe.Spika, uchungu wa kufutiwa matokeo kwa wanafunzi wetu usitupeleke kutaka kuunda Baraza hilo la Mitihani, hiyo haitokuwa ndio dawa ya matatizo yetu. Jambo la msingi sote tushirikiane kuhakikisha kuwa huu mtindo unaoanza kuzoeleka na udanganyifu unaondoka, kwani hata tukiwa na chombo hicho cha mitihani, wanafunzi wanaofanya udanganyifu adhabu itakuwa ni hiyo hiyo ya kufutiwa matokeo.

Kama hatukuchukua hatua hizo, ulimwengu hautotuelewa na mitihani yetu inaweza kukosa sifa za ubora miongoni mwa wenzetu, na inaweza kutufikisha mahali vyeti vyetu vikatiliwa mashaka. Tatizo kama hili limetokea kwa majirani zetu nchini Kenya, wanafunzi elfu mia tisa wamefutiwa matokeo ya mitihani kidato cha nne mwaka huu.

Huu mchezo wa kucheza na mambo haya upo sana, na kwa kweli ulezi tunatakiwa tujikaze. Ikifika mitihani ya kidato cha nne kunatokea kasoro kadhaa katika masuala ya mitihani, baadhi ya kasoro hizo ni wanafunzi kutoandaliwa vya kutosha kukabiliana na mitihani, na kutegemea kufanya mitihani kwa udanganyifu. Kwa hivyo, ndio maana tunaunda Bodi hii ya Mitihani ili kuifanya tathmini ya elimu yetu ili wanafunzi wetu wapate maandalizi katika masomo yao.

Tunaikabidhi jukumu hili Bodi hii ishughulikie masuala haya ya kutathmini elimu yetu, ili wanafunzi wetu wapate mafunzo mazuri katika skuli zao. Vile vile inawezekana tushirikiane, tukamatane tuwafikishe watoto wetu kupata vyeti vilivyo sahihi, na wasipate vyeti walivyovifanyia *cheating* itakuwa ni matatizo.

Mhe.Spika, ninataka nimalizie kwa kusema kwamba kuna wakati fulani tulipata *division one* katika skuli moja. Walipata *division one* wanafunzi 21 wakiwa *form four* kwa sababu wana *division one* wakapata nafasi ya kuingia *form five* na *form six*.

Mhe.Spika, katika wanafunzi wale 21 *form six* tulipata *division zero* 20 na *division four* moja. Sasa hapa utaona kwamba kumbe watu kama hawakupasi vizuri wanakwenda kuboronga huko juu, na ndio hii sababu tunayosema mbona watoto wetu kila siku wanafeli, kumbe vile kuna matatizo ya maandalizi huku chini.

Wizara ya Elimu itajitahidi kusimamia maandalizi ya wanafunzi wetu huku chini, na itachukua hatua kadri inavyowezekana maandalizi haya yaweze kupatikana, lakini Baraza liiunge mkono juu ya suala hili ili wanafunzi wetu waweze kusoma vizuri. Hilo ndilo suala la muhimu. Wanafunzi walioingia *form five* Mhe. Spika, wakianza masomo tu wanatoroka hawawezi ku-*copy* kwenye masuala yale kwa sababu kumbe hawakupasi, lakini ulipita mvujo wakafanya hivi wakaonekana kwamba wamepasi. Itawezekana tutimize wajibu wetu.

Mhe.Spika, baada ya maelezo hayo kama kuna mjumbe ambaye kwa bahati sikupata kumjibu hoja yake naomba anisamehe sana, maana hii kazi ni ngumu sana. Kwa kweli katika kujenga elimu tuna kazi kubwa kweli, mpaka

watoto wetu wawe *so competent* katika masomo, hiyo ndiyo kazi ambayo tunayotaka kuifanya hivi sasa. Serikali itajitahidi kurekebisha hizi changamoto ambazo zipo, ili kuona kwamba tunapata wanafunzi wazuri sana. Mhe.Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe.Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe.Spika: Waheshimiwa Wajumbe, namshukuru sana Mhe.Waziri. Sasa naomba niwahoji wale wanaoafiki hoja hii wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)
Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Vipimo na Tathmini ya Elimu Zanzibar 2012

Mhe.Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza Zima, ili kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Vipimo na Tathmini ya Elimu Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo pamoja na Marekebisho yake

Kifungu cha 1 -

Mhe.Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri kwa ufafanuzi wao wa kina pamoja na ushirikiano wao waliotupa wa kukubali mapendekezo mengi, ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wajumbe mbali mbali.

Mhe.Mwenyekiti, sasa naomba niende moja kwa moja kwenye hoja, kuhusiana na jina ambayo hoja hii imechangiwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi.

Kwa kweli pamoja na maelezo yaliyotolewa kwenye majumuisho na Mhe. Waziri pamoja na ufafanuzi uliotolewa na Mhe. Mwanasheria Mkuu jana, lakini bado kimsingi mimi naamini na wenzangu kwamba, hatukubaliani na suala la kuwa na jina hili la Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Vipimo na Tathmini ya Elimu Zanzibar na Mambo mengine yanayohusiana na hayo. *(Makofi)*

Mhe.Mwenyekiti, kwa faida ya Baraza hili pamoja na wananchi wanaotusikiliza, nadhani ni muhimu kuelewana, kwa sababu mengi katika majibu yaliyotolewa na serikali katika kujibu hoja hii ya jina, yamejielekeza kutwambia kwamba tusiende katika maeneo ambayo sisi hatuna mamlaka nayo. Vile vile imejitokeza hoja kuwa, sisi kwa kupendekeza kubadilisha jina, tunataka kuingilia Mamlaka ya Baraza la Mitihani la Taifa, kitu ambacho si sahihi.

Kwa kweli tunachoelewana ni kwamba kuna mitihani ambayo imewekwa kisheria, hii inasimamiwa na Baraza la Mitihani la Taifa, lakini hata ile inayofanyika Zanzibar, ambayo ni mamlaka ya Zanzibar bado nayo ni mitihani Mhe. Mwenyekiti, yaani Mitihani ya Kidato cha Pili, Darasa la Saba nayo haina jina jengine zaidi ya kuitwa ni mitihani. Kwa hivyo, chombo kinachosimamia, nacho hakina jina jengine zaidi ya kuitwa ni Baraza la Mitihani, lakini litakuwa la Zanzibar kwa mamlaka ambayo sisi tunayo. *(Makofi)*

Katika kusaidia hilo Mhe.Mwenyekiti, naomba tufanye marejeo kwenye Katiba ya Zanzibar ibara ya 78(1) inayozungumzia Nguvu za Kutunga Sheria, Mhe.Mwenyekiti naomba kunukuu.

Ibara ya 78(1) kuhusu Nguvu za Kutunga Sheria inaeleza hivi:-

> "Nguvu za kutunga sheria kwa mambo yote yasiyokuwa ya Muungano katika Zanzibar yatakuwa mikononi mwa Baraza la Wawakilishi".

Lakini pili Mhe. Mwenyekiti, ikiwa hoja iliyoelekezwa ni kwamba katika orodha ya mambo ya muungano kifungu cha 16 kinazungumzia Baraza la Taifa la Mitihani la Tanzania na mambo yote yanayohusika na kazi za baraza hilo, kazi ya baraza hili ni kusimamia mitihani Mhe. Mwenyekiti ya Form IV na Form VI ambayo sisi hatuigusi kwa hivyo kwa kuliita baraza hili hatuvunji kifungu chochote cha katiba ya Muungano.

Mhe. Menyekiti ni kama vile Shirika la Bandari la Zanzibar haidhuru katika orodha hiyo hiyo ya mambo ya Muungano katika kifungu Nam. 11 Bandari imeorodheshwa kwamba ni jambo la muungano, ni kama vile Zanzibar kua na Idara ya Mtakwimu wa Serikali ya Zanzibar haidhuru katika kifungu Nam. 20 cha mambo ya Muungano suala la takwimu ni suala la muungano na mengine na mengine.

Lakini zaidi nimalizie hoja yangu Mhe. Mwenyekiti ili nifahamike zaidi, msingi wa chombo chochote na jina lake inategemea kazi zake na tukiangalia katika kifungu cha 5 cha Mswada huu ambacho kinazungumzia kazi za bodi, hatuna haja ya kupindisha maneno au kutafuna maneno kuanzia (a) mpaka yaliyoongezwa yote kwa namna moja yanahusu mitihani, tukiita vipimo, tukiita tathmini tukiita upimaji yote yale ni sehemu ya majaribio hata katika dini mtihani maana yake ni majaribio unatizamwa uwezo wako, kwa dini kutizimwa uwezo wako kama ni imani yako kwa Mwenyezi Mungu imesimama kiasi gani, kwa dunia unatizamwa uwezo wako ulichosomeshwa umekifahamu kwa namna gani.

Kwa hivyo nadhani Mhe. Mwenyekiti, Serikali ikubaliane kabisa na hoja yetu kwamba mswada huu ubadilishwe jina tuseme sheria ya kuanzisha baraza la mitihani la Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo, kwa maana hiyo sisi kama wanasheria dhamini ni kwamba inasimamia mitihani kwa sasa ya Form 11 darasa la saba ya chekechea aliyotaja Mhe. Waziri na vipimo vyengine vyote vilivyowekwa tunafahamu dhamiri yetu kwa sasa huko mbele tutakuja kuona baada ya marekebisho yatakapofanyika lakini tunaomba jina lilirudi kama ambavyo tunaomba. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Menyekiti namshukuru sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa uamuzi wake na kwa kweli hayo aliyozungumza ndio *spirit* ambayo sisi wajumbe wa Baraza la Wawakilishi sasa hivi tuelewe kwa nini tunaunda chombo hichi, na kusema hasa kwamba tutashughulikia na mitihani ya darasa la saba, Form II pamoja na mitihani ya ualimu na wale education haya ni mambo ambayo tutayashughulikia. Kama ni hilo tumekubaliana sote basi twende kwenye hilo jina ambalo unalipendekeza. *(Makofi).*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti kwa niaba yangu na wajumbe wa Baraza hili tukufu tunamshukuru Mhe. Waziri na tunaomba tuendelee. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Labda kabla hatujaendelea sasa tuweke hiyo maana hasa ya hilo Baraza la Mitihani la Zanzibar ili isije ikagongana na ile iliyoko ndani ya katiba, sasa tunafanyaje kuna maandiko ambayo tunaweka pahala Baraza la Mitihani la Zanzibar maana yake nini.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hatukujua lakini hiyo sio kazi kubwa nadhani tukubaliane niliombe Baraza lako pamoja na wewe kwamba niombe sasa hivi Kamati ya Baraza zima tuendelee na wakati tumeshakubaliana nitaifanya *draft* na niipendekeze hapa kabla hatujamaliza mswada tukikubali iingie katika kifungu cha tafsiri au ufafanuzi baadae. Lakini ile dhamira tumeshakubaliana kwa sababu hii imeshaingia kwenye hansard kwamba tumekubaliana kwamba kwa sasa baraza hili litashughulikia mitihani ambayo iko katika mamlaka ya Zanzibar ambayo ni mitihani ya kidato cha pili, mitihani ya darasa la saba, mitihani ya ualimu na mafunzo mengine ya kiufundi,

Lakini dhamira ni kwamba katika Hansard imeshaingia nini tunakusudia lakini tutakiingiza badala ya ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti: Labda nishauri jambo moja ili tufikie pahala pazuri kuacha katika tafsiri hiyo tuseme wazi wazi isipokua yale yatakayoshughulikiwa na Baraza la Mitihani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sijui tunakubaliana.

Mswada wa Sheria wa kuanzisha bodi ya Vipimo na Tathmini ya Elimu ya Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo pamoja na marekebisho yake.

Marekebisho ndio hayo tuliyosema tunakubaliana.

Kifungu cha 1 Ukurasa wa 55 jina fupi na kuanza kutumika pamoja na Marekebisho yake.

Mhe. Ismali Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kitu kimoja ambacho baadae kitaturahisishia kazi huko kote tunakokwenda, kwa sababu hapa tumebadilisha jina katika mswada tukakubaliana kwamba kote katika mswada huu kila palipotumika neno bodi patatumika sasa kwamba ni Baraza, kwa hivyo hatuna haja ya kurejea huko mbele itarekebishwa lakini tunataka kuweka kwenye rekodi. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Mwenyekiti hamna tatizo madam tuko sawa tutashughulikia hamna matatizo.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo katika kupitia vifungu hadi vifungu kila pahala penye bodi tujue sasa pana marekebisho kwamba ni Baraza.

Kifungu cha 1 Jina fupi na kuanza kutumika pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 2 Ufafanuzi

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, utakumbuka nilipokua nachangia na namuomba Mhe. Waziri pia katika hilo anivumilie nilisema kuna marekebisho mengi ya maneno ya hapa na pale ambayo sikuyafanya pale kwa ajili ya kuokoa muda, nilisema tupitishe vifungu nitayatumia hapa ni mambo madogo madogo katika kuweka sawa na hasa nimepata moyo baada ya kuona kwamba moja katika marekebisho tutakuja kupendekezewa hapa ni Shirika la Utalii na mambo kama hayo, ukiyaachia haya wakati mwengine yatakuja kutuathiri. Kwa hivyo nilikua naomba tufanye marekebisho madogo tu ikiwa Waziri atanikubalia.

Katika tafsiri ya neno mjumbe kwa nafasi yake liko *paragraph* ya 5 kutoka chini pale kuna neno mimi naona linaharibu maana nisome lile neno Mjumbe kwa nafasi yake maana yake ni mjumbe wa bodi ambaye amepata nafasi ya bodi ya kuwemo katika bodi kutokana tu na nafasi yake katika afisi anayofanya kazi. Hili neno tu mimi naona linaharibia maana lingekaa vizuri na ifahamike kama vinavyotungwa sheria nyengine zote kwamba mjumbe kwa nafasi yake maana yake ni Mjumbe wa bodi ambae amepata nafasi ya kuwemo katika bodi kutokana na nafasi yake katika afisi anayoifanyia kazi. Haina haja hii.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Mwenyekiti nakubali ahsante.

Kifungu cha 2 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 3 Kuanzishwa kwa bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 4 Muundo wa bodi pamoja na marekebisho yake

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha nne kinahusu muundo wa bodi na nilipochangia nilitoa maoni au mchango kwamba wale wajumbe wa Baraza hasa kwa kifungu (f), (h) na (i) kwamba hawa ili kuimarisha misingi ya demokrasia na uwakilishi wateuliwe au wachaguliwa na jumuiya zao. Mhe. Waziri alipokua anatoa majumuisho nimefurahi ametoa maelezo ya kati na kati kwamba amependekeza waendelee kuteuliwa na Waziri.

Lakini Waziri atashauriana na Jumuiya hizi, lakini bahati mbaya hayo yamebakia kwamba ni maelezo humu katika mswada yatakuwa hayamo, sasa katika kuweka rekodi sawa nimetizama pia marekebisho ambayo yalifanywa na kamati, naomba twende katika waraka wa kamati kwenye kifungu Nam. 14 ambayo inasema kinaingizwa kifungu kipya cha nne kile ambacho kinasomeka wajumbe wa bodi mbali ya wajumbe kwa nafasi zao watateuliwa na Waziri, mimi nilikua naomba tuongeze yale maelekezo yaliyosemwa na Mhe. Waziri kwamba wajumbe wa vifungu (f) (h) na (j) hawa watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na jumuiya wanazotoka nadhani hiyo ni muhimu ikaweko katika mswada.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Mwenyekiti hiyo pia haina matatizo kwa sababu tangu hapo unapofanya uteuzi watu ambao wanaletwa wewe

unakua kazi yako kuwataja, lakini wenyewe huko wanakua wameshachagua, kwa hivyo wewe unawataka kwamba ndio unawateua kwa hivyo sio mbaya hiyo.

Kifungu cha 4 Muundo wa Bodi pamoja na marekebisho yake

Mhe. Mwenyekiti: Marekebisho hapa ni hiyo kwa kushauriana na jumuiya zao.

Kifungu cha 5 Kazi za Bodi pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti nashukuru tena katika kifungu hiki katika michango yangu nilifanya marekebisho mengi sana ya lugha kutokana na tafsiri ya kiingereza, moja ni la (a) kwa sababu hili lilikua ni makosa makubwa sana ya tafsiri nililiandika hasa nikampelekea Mhe. Waziri kama alivyothibitisha katika majumuisho yake. Lakini katika kuweka uzuri labda naomba niyasome yale mengine ili yaingie katika hansard ili yaje yasaidie baadae katika kuyaandika vizuri kwenye mswada huu kabla ya kupelekwa kwa Mhe. Rais.

Najua Mhe. Waziri alishajibu kwamba kimsingi anakubali lakini nataka nione kwamba tunakwenda pamoja, kwamba (c) nilipendekeza kwamba yale maneno ya kuweka utaratibu maalum ya mwanzo yaondoke yaende moja kwa moja kutunga mitihani, majaribio na aina nyengine za upimaji wa wanafunzi na maendeleo yao kwa mujibu wa mtaala wa Zanzibar.

b) Nilipendekeza kwamba isomeke kuendesha mitihani kwa elimu za msingi sekondari, na mafunzo ya ualimu, na mitihani mingine katika Zanzibar kadiri itakavyoonekana inafaa kwa maslahi ya umma, hii kusimamia kukusanya na kuweka kumbu kumbu za muendelezo wa upimaji wa wanafunzi na maendeleo ya mitihani .

e) Kusimamia kukusanya na kuweka kumbu kumbu za muendelezo wa upimaji wa wanafunzi na maendeleo wanayoyapata wanafunzi kushinda mitihani inayofanywa na bodi.

f) Kuweka na kuandaa miongozo kwa skuli na vyuo inayohusu namna ya kufanya, upimaji wa maendeleo ya wanafunzi

g) Kutoa matokeo ya kuwatunukia vyeti na stashahada wanafunzi waliofaulu kwa mujibu wa mitihani inayosimamiwa na bodi siyo inayofanywa na bodi.

h) Nilipendekeza kwamba yale narekebisho ya kamati yalikua yanaharibu maana iliyokusudiwa kwa hivyo yaliyobakia yabakie kama maana ilivyo

i) Nilipendekeza yafanywe marekebisho kushirikiana na vyombo mbali mbali vya kitaaluma vya hapa nchini, kikanda na vya nchi za nje mamlaka za uratibu na usimamizi na wadau wengine husika katika kufanya utafiti, kuchapishwa takwimu na taarifa nyengine ili kukuzwa utaratibu mwengine unaofaa wa mitihani na kiwango bora cha elimu Zanzibar.

j) Kufanya tathmini ili kugundua na kuzifanyia kazi na mapungufu ya mipango ya elimu na kuinua kiwango cha wanafunzi katika kujifunza.

k) Kutunga kanuni badala ya kuweka miongozo katika iwe moja kwa moja kutunga kanuni za uendeshaji wa mitihani na kwa mambo mengine yote yanayofaa kwa ajili hiyo.

l) Kufanya mambo mengine muhimu kwa kuharakisha utekelezaji mzima wa moja au zote kati ya kazi zilizoelekezwa kwa bodi chini ya sheria hii nilikua naomba marekebisho haya yaingie katika yale niliyopendekeza.

Mhe. Mwenyekiti: Haya yote ulimuandikia Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe Mwenyekiti, katika aliyoyasema hicho kifungu (g) naona ingelikua vizuri tukasema kwamba kutoa matokeo kuwapa vyeti na stashahada wanafunzi waliofaulu kwa mujibu wa mitihani inayotungwa na kusimamiwa na bodi mengine yote nayakubali.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti nayakubali mapendekezo yake.

Kifungu cha 5 Kazi za bodi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 6 Uwezo wa bodi

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti kifungu cha 6 marekebisho yake madogo madogo tu, kwanza niseme nikiowanisha na ile ya kiingereza ili tupate usawa. Kwanza (b) pale baada ya kusema vyanzo vya mapato ya bodi na mali nyengine za bodi, kwanza hiyo bodi bodi inajirejea. Nilikua napendekeza isomeke kusimamia mapato na mali nyengine za Baraza hiyo tumeshasema inaingia moja kwa moja.

Pale (c) iliandikwa kuonesha umuhimu wa, lakini katika kiingereza imetumika kwa maana ya muhuri kwa hivyo napendekeza isomeke kuthibitisha kazi za Baraza kwa kutumia muhuri wake. Na pale (f) nilipendekeza pale inapoanza kwanza kwenye chombo chombo mara mbili, lakini nilipendekeza isomeke kualika na kuingia makubaliano na chombo au vyombo vyovyote kutoka nje ya Zanzibar halafu iendelee kama ilivyo.

Na (i) badala ya kutoyakubali na kuyapinga hii lugha iliyotumika haiendani na masuala ya mitihani, nilikua nasema kuyakataa na kuyafuta matokeo ya mitihani yaliyokua hayakutimiza masharti ya lazima ya mitihani. Kifungu cha mwisho nakiunga mkono na nilikua naomba Mhe. Mwenyekiti marekebisho hayo pia tuyaweke. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Mwenyekiti, hiyo haijabadilisha maana kwa hivyo nakubaliana nayo na itafanana na ile ya kiingereza.

Kifungu cha 6 Uwezo wa Bodi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 7 Vikao na Maamuzi ya Bado

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 7 kifungu kidogo cha 3 nilikua naomba tukiweke sawa vizuri kua Mwenyekiti anaweza kuitisha mkutano maalum wakati wowote itakapoombwa hili neno wingi iondoke, itakapoombwa na nusu ya wajumbe halafu tumalizie ile watakaokuwepo iondoke, zaidi ya nusu ya wajumbe wa bodi waliopo. Yaani isomeke Mwenyekiti anaweza kuitisha mkutano maalum wakati wowote itakapoombwa na zaidi ya nusu ya wajumbe wa bodi waliopo, hiyo ni kwa kifungu cha tatu.

Vile vile nilikua naomba tufanye marekebisho kwenye kifungu cha 6 maamuzi ya vikao vya bodi yatafanywa imeandikwa kwa wingi zaidi ya nusu makosa yale yale, sasa isomeke maamuzi ya vikao vya bodi yatafanywa kwa kuungwa mkono na zaidi ya nusu ya kura za wajumbe waliokuwepo na itakapotokea neno usawa katika kura, tuandike itakapolingana kura au kulingana na idadi ya kura Mwenyekiti atakua na kura ya maamuzi.

Mwisho kabisa kifungu cha 8 hichi nilipendekeza kitu sasa namuomba Mhe. Waziri kidogo aniambie kwamba amekubaliana na mapendekezo yangu au vipi kwa sababu hakujibu moja moja, hapa nilipendekeza nilipokua nachangia kwamba haya maneno ya mwisho au kwa kasoro katika uteuzi wa mmoja wao tuyaondoe.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ilikua ni kwamba uhalali wa matendo wa mwenendo wa uendeshaji wa baraza wowote hautoathirika kwa kutokuwepo mmoja kati ya wajumbe hilo tunalo. Lakini nilieleza kwamba tukijumuisha inapotokezea kuna kasoro katika uteuzi wa mmoja wa mjumbe wake halafu kitaendelea na maamuzi kua halali. Kwa hivyo mimi nilipendekeza kwamba haya maneno au kwa kasoro katika uteuzi wa mmoja wao yaondoke, sasa sikusikia kama Mhe. Waziri kakubali au vipi nilikua naomba jibu. Ahsante sana

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Mwenyekiti, anachokizungumza Mhe. Ismail Jussa Ladhu ni kwamba uhalali wa matendo au mwenendo wa bodi zote hautoathirika kwa kutokuwepo mmoja kati ya wajumbe. Hapo tuko sawa sawa, sasa anasema au kwa kasoro katika uteuzi wa mmoja wao, nadhani lakini mwenyewe atathibitisha pengine mtu kateuliwa katika nafasi hii hana sifa maana yeye kasema uteuzi kama anakusudia hiyo nakubaliana nae.

Lakini kama kasoro yenyewe ya kwamba Wajumbe walitakiwa wawe 11 lakini watu wawili hawajateuliwa hapo ndio kidogo tutatafautiana, sasa hii kasoro anaichukulia ipi anaichukulia zile sifa za uteuzi ndio kasoro za uteuzi wa mjumbe, au kua kuna kasoro za watu wawili hawajateuliwa mle.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba unistahamilie kidogo ili tuelewane, mimi nimetoa maoni hayo baada ya kutizama ya kiingereza kwa sababu tunaambiwa ni muhimu kutizama zote mbili kwa sababu mwisho tukitunga sheria itakayokwenda kusimama mahakamani ni ile ya kiingereza, haidhuru dhamira ya watunga sheria itatizamwa kwa majadiliano ndani ya Baraza ikija kutokezea kitu kikubwa sana hivyo ndivyo kawaida.

Sasa katika kiingereza iliyotumika kwenye ukurasa wa 80 imesema *the validity of any acts of the proceedings of the board* naamini sasa itakuwa *of the council Shall not be affected by any vacancy* ambayo hiyo itakuwa sina tatizo nayo *among its members or by any defects of the appointment of any of them* sasa mimi *problem* yangu ilikuwa hii *defects* kwamba tuseme ili tufahamiane vizuri na wenzangu tunaotunga sheria pamoja, hapa katika wajumbe waliotajwa wametajwa kwamba kuwepo na mkaguzi mkuu wa elimu, muwakilishi kutoka jumuiya za walimu.

Hawa kila mmoja kapendekezwa kwa sababu ana umuhimu wake katika kile chombo, sasa kwa mfano ikatokea uteuzi kachaguliwa mjumbe kuwakilisha walimu kumbe katoka jumuiya ya wakulima hiyo itakuwa ni *defects*, sasa kama itatokezea *defects* kama hii hili tusilikubali ndio hoja yanagu mimi.

Kwamba ile sheria tunayoitunga imalizie ile idadi ya wajumbe kama itakuwa haikutimia. Mimi nakubali ni utaratibu wa kawaida kwamba maamuzi yatakuwa ni halali madam wametimiza *quorum*, lakini ikiwa kutakuwa na kasoro kwa maana ya *defects* kwa yule mjumbe aliyechaguliwa tusihalalishe maamuzi kama yale Mhe. Menyekiti. Ndio maana nikasema hii *phrase* ya mwisho hii tuiondoe tubakishe ile ya upungufu wa idadi Ahsate sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Mwenyekiti, hiyo ina maana kakubaliana na ile hoja yangu ya kwanza kwamba kachaguliwa mtu kinyume na ile sheria inavyotaka, kwa hilo nakubalia nae.

Mhe. Mwenyekiti: Lakini kukasoreka baadhi ya mjumbe ilimradi *quorum* ipo haina tatizo nadhani kauliza hivyo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Hilo nakubaliana nae.

Kifungu cha 7 Vikao na maamuzi ya bodi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 8 Muda wa wajumbe katika bodi

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha nane vile vile kwa kuweka rikodi vizuri, kwanza atakumbuka Mhe. Waziri nilipokuwa nachangia nilipendekeza kile kifungu cha mwisho mstari wa pili kutoka chini, ‘anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine’, nilisema tuongeze ‘kimoja’ kama ambavyo Waziri ataona inafaa. Kwa sababu cha kiingereza kimetumika kwa *second term* kwamba si zaidi ya hapo, sasa ukiicha hivi hivi tu kifungu chengine kinaweza kuja na chengine na chengine. Kwa hivyo ili pakae sawa aseme anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja kama ambavyo Waziri ataona inafaa hiyo kwa nane moja.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, katika kuweka vizuri lugha tu kifungu kidogo cha 3 kipo ukurasa wa sitini nadhani pale inapoanza tuanze na neno pale itakapotokea neno lile limekosekana hapa mjumbe wa bodi kuhudhuria, na vile vile mstari wa tatu kutoka chini wa kifungu hichi cha tatu mwisho wa mstari pale kuna neno na kwa mjumbe husika hii na ukisoma kwa kiingereza ilikuwa iwe au. Yaani huyo mjumbe atakayechaguliwa kujaza nafasi kwa muda atachukua nafasi hiyo hadi atakaporejesha jukumu hilo kwa mjumbe husika au hadi pale muda wa utumishi wa mjumbe huyo katika bodi utakapokwisha, sasa lolote kati ya hayo litakalotokezea mwanzo.

Sasa hapo inaweka nafasi kwa zote mbili na nimalizie kabisa kwenye kijifungu cha nne kama kilivyofanyiwa marekebisho nayakubali hayo marekebisho, pale neno tupu tutumie neno wazi ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Mwenyekiti, hayo katika majumuisho yangu ndio niliyosema ni marekebisho ambayo tumeyakubali na vizuri ameshaweka kwenye *hansard*.

Kifungu cha 8 Muda wa Wajumbe

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti mimi kidogo nilikuwa nataka Mhe, Waziri anisaidie ufafanuzi huu, moja inazungumzia muda wa wajumbe wa bodi na tunajua bodi zote zinakuwa na muda wake aidha miaka mitatu halafu kama alivyosema Mhe. Ismail Jussa Ladhu hapa katika ile sheria ya kiingereza inavyosema kwamba anaweza kuteuliwa katika hicho kipindi chengine kimoja. Lakini kwa kuwa tumebadilisha tafsiri ya jina la mswada badala ya bodi sasa hivi kutakuwa Baraza.

Mhe. Waziri hebu tusaidie Je, huu ujumbe wa baraza utaratibu wake unakuwa unabadilika badilika kama wanavyokuwa wajumbe wa bodi, kwa sababu baraza la mitihani linakuwa ni chombo cha kila siku na kila wanavyo kaa muda mrefu wanazidi kujenga uzoefu na mambo mengine kama hivi. Jina tumeshakubaliana tunabadilisha inakuwa ni baraza, je na huu muda wa hili baraza utakuwa kama hivi sheria inavyosema.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Mwenyekiti, kwanza tumeweka wazi kwamba kila kwenye bodi sasa tutakuwa tunaandika Baraza hiyo tumeiweka wazi, pendekezo la Mhe. Ismali Jussa Ladhu la kwamba mtu atateuliwa katika kipindi cha miaka mitatu ya mwanzo, anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine cha kipindi kimoja hili naona sio tatizo ndio tunatanua demokrasia sio kwamba mtu akae pale vipindi saba au vinane yeye yupo tu pale.

Hapo bodi tayari tunafanya hivyo unateuliwa mara ya kwanza halafu unapewa fursa tena mara moja kama unaendelea na una uwezo mkubwa halafu basi, kwa hivyo mimi nafikiri huu utaratibu sio mbaya Mhe. Hamza Hassan Juma usimshughulishe sana ni vizuri kama una uhakika kwamba umefanya vizuri utakaa na hili baraza kwa muda wa miaka sita, baada ya miaka sita wewe tena usubiri uteuzi wa sehemu nyengine na hapo wataingia wengine sio mbaya.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi katika suala zima kama tarsiri ya bodi sina mashaka nayo kwa sababu najua bodi zinavyokwenda na sheria zake na taratibu zake, lakini je huu muundo wa baraza unaenda katika ule muda wake wa kazi kama hizi bodi au Baraza pengine labda Baraza katika sheria za Mabaraza muda wake unakuwa mrefu sana. Kitu ambacho ninachotaka kuelewa ni muundo wa Mabaraza, utendaji wake na muda wake unakuwa sawa sawa na hizi bodi.

Unajua wana sheria wamo wengi humu. Hata Mhe. Jussa kama ana uzoefu katika mabaraza, katika kusaidiana tunatengeneza sheria tusimuachae lazima ajibu waziri tu. Lakini nafikiri kama kuna utaratibu ambao unaturuhusu hata sisi wenyewe kama tunao uzoefu wa hivi vyombo, hata Mwanasheria Mshimba anaweza akatusaidia. Kubwa nilikuwa nataka nipate je, mabaraza *last time* yake inakuwa kama bodi au vipi. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Mwenyekiti, mimi naona haya ni masuala tunayokubaliana wenyewe, kwamba Baraza letu Mjumbe atakuwa katika kipindi cha miaka mitatu na ataweza kuongeza kipindi chengine cha miaka mitatu.

Tukenda labda kwenye tafsiri labda ya bodi, Baraza na nini itabidi tupate wanasheria ambao wewe Mheshimiwa unao katika Afisi yako waeleze kama kuna tafsiri maalum kwamba Baraza lazima livuke miaka mitatu. Hiyo mimi ipo nje ya utambuzi wangu. Mimi najua tu kwamba tukishakubaliana kwamba kipindi cha kukaa mtu ndani ya Baraza ni miaka mitatu basi tukubaliane hilo, akiongezwa tena miaka mengine mitatu tukubaliane hilo. Tukishakubaliana hilo basi sheria yetu itakuwa inafanya kazi bila ya tatizo lolote. Tafsiri hasa kwamba Baraza linakuwa lazima miaka mitano, hiyo Mheshimiwa naeleza wazi sina uhakika nayo.

Mhe. Mwenyekiti: Isipokuwa labda tuone kwa wale wanateuliwa kwa mfano Mkurugenzi. Inawezekana pangine akateuliwa, kipindi cha miaka mitano akateuliwa tena miaka mitano, ambayo kwa huku anaingia kwa nafasi hiyo ya ukurugenzi. Hii labda muitizame vile vile.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mheshimiwa hawa wengine ni *X-official*, hawa wanakuwa wanaendelea na kazi, sasa kama Rais atabadilisha ndio anakuja mwengine. Hiyo ipo nje ya uwezo wetu. Lakini wale wanaoteuliwa na Waziri *house X official* hawa watatumia hivi vipindi ambavyo nimevieleza.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mheshimiwa labda kwa kusaidia tu hiyo imekuwa *provided for expressed* katika huu Mswada. Ukisoma hichi kifungu cha 8(1) kinasema wazi, nasoma kama tulivyorekebisha. Mjumbe wa Baraza isipokuwa wale ambao wapo kutokana na nafasi zao za kazi itakuwa kipindi hicho. Kwa hivyo wale ishakuwa *expressed* katika sheria.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu cha 8 Muda wa Wajumbe Katika Bodi Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 9 Kueleza Bayana Maslahi

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna mambo kama mawili. Kwanza kuna yale maneno ambayo yapo katika 9(1) na 9(5) yanayomalizikia "isipokuwa tu pale ambapo Bodi itaelekeza vyenginevyo" ambayo nilipendekeza katika mchango wangu kwamba haya yaondoke, ili kutotoa mwanya kwa mtu ambaye ana *interest* ya moja kwa moja.
Mhe. Waziri katika majumuisho yake kaniomba kwamba nikubali kwamba haya yabakie. Nashukuru kanipa maelezo ya msingi ambayo yanaendana na hali halisi ya nchi yetu. Nataka kusema hilo kimsingi sina tatizo nalo nataka nimkubalie Mhe. Waziri. Lakini nataka kuweka *record* sawa tuwe nazo hapa hasa kwa uongozi wa wizara. Kwa sababu Mhe. Ramadhani alituahidi tukijaaliwa mchana huu tunamkosa katika Wizara hii.

Katika suala hili kuna msingi wa sheria ambayo Mhe. Mwenyekiti kwa sababu wewe pia ni wa fani hii unajua kwamba ukitoa nguvu ya madaraka popote ni lazima yatekelezwe kwa uangalifu kwa uadilifu na hekma. Lakini mara nyingi katika nchi yetu uzoefu unaonesha vyenginevyo ndio maana inakuwa inatupa mashaka sana, ndio inabidi tutunge sheria kila pahala tukatie *lock* kwa sababu ukimuachia mtu hatekelezi ile *judicially* ambayo msingi wa *power* unaoutaka.

Nataka nimkubalie Mhe. Waziri na niiondoshe kabisa *proposal* yangu lakini nataka hiyo *point* iwe *noted* tu kwamba tunakwenda hii lakini watakaosoma ni hili Baraza wazingatie hilo. Kwa sababu haya mambo ya *interest* ukiyaachia mara nyengine na tukasema chombo kile kile pale mara nyengine tunapokuwa tunaelekezana ndipo kinapokuja kutumika vibaya na ikaathiri maamuzi ambayo baadae yanawapotezea imani wananchi kwa vyombo kama hivi.

Hilo niliache zaidi katika kurekebisha ilikuwa ni katika kijifungu cha 3 (1) "Mjumbe atakaposhindwa kuweka bayana maslahi binafsi kwa mujibu wa kijifungu cha (1) cha kifungu hiki na maamuzi ya bodi (nafikiri inapaswa liongezwe neno "yaliyofanywa" lilikosekana hapa) yakamnufaisha mjumbe huyo maamuzi hayo yatakuwa ni batili na hayakubaliki. Hili neno "hayakubaliki" nadhani Mhe. Mwenyekiti, katika utungaji wa sheria haihitajiki. Ukishasema ni batili inafahamika nilikuwa nadhani tungeishia hapo.

Lakini vile vile katika hivi vifungu vidogo cha (4) na (6) ili kuokoa muda niyaseme kwa pamoja tu. Ile katika kutaja kosa kidogo kuna mapungufu katika uandishi na hii si hapa tu kila pahala imeandikwa hivyo hivyo. Inasemwa tu nitoe mfano ili nifahamike moja kwa moja. Anasema "Mjumbe atakayekwenda kinyume cha kifungu cha (1) cha kifungu hiki ametenda kosa." Kawaida ya uandishi Mhe. Mwenyekiti, atakuwa ametenda kosa na hilo limekosekana katika kila tafsiri ya vifungu vya makosa. Nilikuwa naomba hayo pia tuyarekebishe kwa pamoja. Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Mwenyekiti, mimi namshukuru sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa kukubaliana na yale maneno yale tuyawache na hili pia aliloshauri ni mashauri mazuri na nayapokea *inshaallah*.

Kifungu cha 9 Kueleza Bayana Maslahi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 10 Muhuri wa Bodi.
Kifungu cha 11 Maposho na Malipo ya Bodi.
Kifungu cha 12 Kuajiri Wafanyakazi.

Kifungu cha 13 Afisi ya mwenye Mamlaka pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 14 Kuanzishwa kwa Kamati pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 15 Kazi za Kamati Tendaji

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 15 (a) Kufanya kazi za kawaida za kiutendaji katika usimamizi wa bodi, iwe sahihi ni uendeshaji wa Baraza litakuwa sasa. Nilisema hili katika mchango wangu naomba liwe *noted*.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Mwenyekiti, sawa nakubali.

Kifungu cha 15 Kazi za Kamati Tendaji pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 16 Kazi za Kamati ya Mitihani

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 16 (1) kwanza nadhani kiutaratibu wa uandishi imeandikwa 16 (1) lakini hakun a 16 (2). Kwa hivyo, nadhani hii nambari tuirekebishe haipaswi kuwa na hiyo (1) hapo. Lakini zaidi (h) ambayo iko ukurasa wa 63 nilikuwa naomba ili isomeke vizuri isomeke kutoa mapendekezo kwa Baraza kuhusiana na mambo yanayohusika na mitihani inayoendeshwa na kusimamiwa na Baraza.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Mwenyekiti, sawa nakubali marekebisho ya lugha hayo.

Kifungu cha 16 Kazi za Kamati ya Mitihani pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 17 Mkurugenzi

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki katika marekebisho ambayo yaliletwa na kamati ilipendekezwa kwamba yale maneno ya pembeni *(marginal notes)* iongezwe Mkurugenzi wa Bodi halafu kila pahala imeandikwa hivyo. Sasa kwa tafsiri mpya itakuwa Mkurugenzi wa Baraza, lakini ilikuwa sioni hiyo mantiki ya kuongeza hayo katika hizo *notes* kwa nini asiseme Mhe. Mwenyekiti. Ukitazama katika tafsiri huku ufafanuzi limeshatajwa mkurugenzi ni nani, sasa kila palipotajwa mkurugenzi maana yake ina-*refer* kwenye mkurugenzi yule.

Kwa sababu mkurugenzi mwengine asiyekuwa yule kishafafanuliwa na hii sheria, kila anapotajwa mkurugenzi mwengine asiyekuwa yule kafafanuliwa ni mkurugenzi yupi. Kwa hivyo, mkurugenzi huyu ni yule wa Baraza sasa atakuwa au sijui tutamuitaje kwa lugha nyengine. Nilikuwa nadhani lile pendekezo la kuongezea wa Bodi ambao sasa atakuwa wa Baraza haikuwa na haja katika utungaji mzuri wa kisheria sasa ibakie mkurugenzi tu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Mwenyekiti, sawa sawa nimekubali.

Kifungu cha 17 Mkurugenzi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 18 Kazi za Mkurugenzi

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia mswada h uu kwenye kifungu hichi cha 18 nilijaribu kumshauri Mhe. Waziri aweke sawa juu ya maelezo haya ya Kazi za Mkurugenzi hapa na kwa sababu zilionekana hazikukaa vyema. Pili pia nikashauri kwamba hiki kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 18 kifutwe na kwa sababu hakioneshi mantiki yoyote na nikapendekeza iandikwe kama hivi ifuatavyo.

Kifungu cha (1) “Kwa mujibu wa masharti ya sheria hii Mkurugenzi atawajibika kwa bodi.” Lakini kifungu cha (2) kieleze kwamba “Mbali ya kazi zake za kawaida Mkurugenzi atawajibika kufanya kazi za kila siku za Bodi.”
Kwa hivyo, nilipendekeza ikae hivi ili visomeke vizuri. Lakini pia nikasema kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki atupe ufafanuzi Mhe. Waziri juu ya kifungu hiki ambacho kimeandikwa kwamba “Timu ya Uongozi inajumuisha Mkurugenzi na maofisa wengine wa Bodi.” ikiwa kama hakina maelezo basi kifutwe hakina maana yoyote.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Mwenyekiti, marekebisho yake ya hicho kifungu cha pili nayakubali, kifungu cha (4) labda neno alivyolitumia Timu

ya Uongozi lakini hii ni Sekretarieti ya Baraza ambayo itajumlisha Mkurugenzi na maofisa wengine wa Baraza. Hii ni sekretarieti sasa hapa imetumika timu, labda hili neno timu linaleta *confusion* kidogo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri anasema kwamba neno timu liondoshwe badala yake liwekwe sekretarieti nayo itajumuisha Mkurugenzi na maofisa wengine. Hilo sekretarieti ndio jina jipya kabisa ambalo katika sheria yetu humu hamna kabisa. Hii ni chombo cha utendaji cha Baraza ambacho kinafanya kazi za ndani ya ofisi ya Baraza, ni Mkurugenzi na wale maofisa walioajiriwa pale ndani ya Baraza. Sasa ndio maana walipohangaika kutafuta jina ndio wakatumia hili neno timu. Ni utendaji Kamati Tendaji ya Baraza, hii ni sekretarieti ya kila siku kwa siku.
Mhe. Mwenyekiti, katika kila ofisi kunakuwa kuna sekretarieti inayofanya zile kazi za maandalizi ya chini, halafu tena yanapelekwa kwa mabwana wakubwa kule wafanye uamuzi.

Mhe. Mwenyekiti: Unaona ipi sasa sekretarieti tuipe tafsiri au timu tuipe tafsiri ili tuone neno gani litaficha hapa.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, hiki kifungu cha (4) hivi kilivyoandikwa nilihitaji nipate ufafanuzi kwa sababu wameandika Timu ya Uongozi. Lakini kwenye ufafanuzi Mhe. Waziri akasema sekretarieti, lakini ukiangalia hili neno sekretarieti katika sheria yetu hii ni jipya halimo kabisa. Sasa tutafute neno ambalo litakuwa linaoana na hii sheria ili hii *statement* ikae vizuri.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, najua unatumia busara zako tu maana yake kanuni hasa *strictly* haziruhusu kwa sababu hii ni hoja iliyosemwa na Mhe. Salmin Awadh Salmin. Lakini nilikuwa naomba kulisaidia Baraza kwa sababu tunatunga sheria. Nadhani tukisoma ile ya Kiingereza itatusaidia na nadhani tatizo linarudi pale pale katika kutafsiri hivi vifungu mara nyengine hawa wanawahangaisha sana Mawaziri wetu inabidi tuwanyanyue mara nyingi kwa mambo ambayo pengine ni tafsiri tu. Naomba watuwie radhi sana lakini nina nia ya kutengeneza.

Mhe. Mwenyekiti, ukisoma katika Kiingereza kifungu cha 18 hapa pamezungumzwa *functions of the director* na ndio maana hata katika ile *drafting* ya Kiingereza imekaa vizuri kwa sababu haikuanza na Timu ya Uongozi imeanza na Director bado kwa sababu inamzungumzia *Director*.

Inasema *"The Director and other officers of the Board shall constitute the Management Team of the Board."* Huku ukisoma sheria kuna sehemu imetajwa kwamba kuna Mkurugenzi na kuna maofisa wengine wale ambao katika mchango wake Mhe. Salmin Awadh Salmin pia aliwataja wale walioitwa maofisa wenye mamlaka ya watu wengine wale ambao wako katika kifungu cha 13.

Sasa nadhani ingekuwa imeandikwa vizuri tu ingekuwa hata haina tatizo wala ilikuwa haina haja ya kuongeza tafsiri mpya ya neno lolote. Ingeandikwa tu "Mkurugenzi na maofisa wengine wa Baraza watakuwa ndio Timu ya Uongozi ya Baraza." Kwa sababu kinachokusudiwa hapa ndio hiyo kwa lugha nyengine sekretarieti wale watendaji, lakini ukiita Kamati ya Utendaji utapata matatizo kwa sababu tayari kule kuna sehemu inazungumzia Kamati ya Utendaji. Kwa hivyo, nilikuwa nadhani tungeanza vile vile lakini ingebadilishwa ile *drafting* tu ikasomeka Mkurugenzi na maofisa wengine wa Baraza watafanya Timu ya Uongozi ya Baraza au Timu ya Utendaji. Labda tuweke hivyo itaeleweka kwa maana ya *management*.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa kifupi tuna tafsiri hii ya Kiingereza ndio tunayoweka hapa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana nayo hiyo.

Kifungu cha 18 Kazi za Mkurugenzi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 19 Fedha na Mapato ya Bodi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 20 Makisio ya Mwaka.
Kifungu cha 21 Hesabu za Bodi na Ukaguzi

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza Wajumbe wako wasichoke kwa sababu tunafanya kazi ya kutunga sheria hasa sasa baada ya ile mijadala mingi. Mhe. Mwenyekiti, tunamuaga vizuri Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban katika wizara hii. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa na marekebisho madogo tu kwamba katika kile kijifungu kidogo cha (2) kamati ilishafanya marekebisho kusema kila alipotajwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu

iongezwe za Serikali. Lakini kuna kijifungu kidogo cha (2) cha 21 kinasema "Hesabu za Bodi zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mtu mwengine yeyote aliyeidhinishwa."

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ukenda katika Kiingereza imezungumziwa chombo bodi na hii ni mamlaka ya kawaida ya mdhibiti kwamba inawezekana imezidiwa ikaagiza timu ya wataalam wa ukaguzi wengine au chombo kingine lakini si mtu. Kwa hivyo, nilikuwa nadhani irekebishwe sehemu hii iwe "Hesabu za Bodi zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au chombo chengine chochote kilichoidhinishwa na kukubaliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kama ilivyo, ili tupate tafsiri sahihi ya Kiingereza.

Ukiangalia marekebisho ya kamati lilikuwa limewapita kidogo hili. Kile kijifungu cha 4 "Bodi italazimika kwa muda ambao si zaidi ya miezi 4 baada ya mwisho wa mwaka wa fedha kuwasilisha. Nadhani hata Mhe. Saidi alivyochangia aliliuliza hili kwamba kwa nani. Ukisoma kiingereza imetaja kwa waziri. Kwa hivyo nilikuwa nadhani lile neno kwa waziri hapa lilikosekana liingie iwe ni "kuwasilisha kwa waziri" halafu itaendelea kama ilivyo pamoja na kile cha 5 cha kiingereza kilikuwa kimesahauliwa lakini Kamati bahati nzuri wamekiona na wamekitafsiri vizuri wamekiweka na sisi tukikiweka tutakuwa tumepata kifungu safi kabisa. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Mwenyekiti, unajua matatizo haya yanakuja kutokana na kutofsiri kutoka kwenye kiingereza kuingia katika Kiswahili. Ndio maana unakuta mambo kama haya. Hizo *concept* anazozizungumza ndugu Jussa ndizo zilizokusudiwa, ndio maana nikawa nakubaliana na yeye kwa sababu hizo ndizo *concept* zilizokusudiwa hasa. Kwa hivyo hakuna matatizo, yeye anajaribu kutuwekea sawa ile *language*. Sasa nafikiri vijana wetu wajifunze zaidi kufanya *translation* wasiwe wanatafsiri neno kwa neno, mara watasema kwanda kwa mguu maana yake mmoja mmoja mwili haukanyagi. Sawa sawa ahsante, nakubali Mheshimiwa.

Kifungu cha 21 Hesabu za Bodi na Ukaguzi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 22 …

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, nilivyokuwa nikichangia jana Mswada huu katika kifungu cha 22 cha viapo, makosa na adhabu nilimshauri Mhe. Waziri afanye mabadiliko kidogo katika hii aya ambapo inasema "Bodi inaweza kumtaka mtu yeyote" badala ya kuiahirisha kwamba "Baraza inaweza kumtaka mtu yeyote anayefanya kazi za Baraza au anayetakiwa kuendesha mitihani *so and so* basi ale kiapo mbele ya Mkuu wa viapo"

Nikamuomba Mhe. Waziri iwe sasa ni kitu cha lazima kutokana na unyeti wa shughuli yenyewe na matukio ambayo yamejitokeza. Kwanza Baraza lenyewe lote lile kiapo mbele ya Mkuu wa Kiapo, lakini na watendaji wote wale viapo. Kwa hivyo badala yake iwe "Baraza litamtaka kila mtu anayefanya kazi za Bara …." Ni hivyo tu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Sawa katengeneza vizuri.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ni ndogo sana. Nilipokuwa nachangia Mswada huu nakumbuka nilimsikia waziri katika majumuisho kama vile alikubali lakini nataka ikae vizuri katika *record* za hansard tu. Nilipendekeza katika kifungu cha 22(2) katika jumla ya makosa ambayo yameorodheshwa, nilipendekeza Mhe. Mwenyekiti, kwamba kuna maeneo mawili.

1) Nilipendekeza kwenye kifungu cha 10(2) kinachozungumzia muhuri nilipendekeza kwamba huku uje kuorodheshwa kwamba katika makosa mtu ambaye anatumia vibaya muhuri wa Baraza kwamba pia liwe ni kosa.

2) Nilipendekeza katika kifungu cha 13(5) pale nilisema pametajwa kosa kwa mtu ambaye atamzuia yule afisa aliyepewa mamlaka. Lakini nikasema na yule afisa mwenyewe na yeye akitumia vibaya madaraka yake haikufanywa kwamba ni kosa. Kwa hivyo nikapendekeza huku mwisho katika kifungu cha 22(2) yaorodheshwe makosa yao ya ziada mawili.

    (i) Kwa mtu ambaye bila shaka atakuwa ni mtendaji wa Baraza atakayetumia vibaya muhuri wa Baraza.

(ii) Vile vile iorodheshwe huyo Afisa mwenye mamlaka iwapo na yeye kwa kitambulisho alichopewa cha kufanya kazi zake atakitumia vibaya kwa madhumuni kinyume aliyopewa. Hilo nalo pia ni kosa kwa hivyo yaorodheshwe.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nashukuru sana.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Sawa.

Kifungu cha 22 Viapo Makosa na Adhabu Pamoja na Marekebisho Yake.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Kifungu 22(3) ambacho tumeomba neno "inaweza kusimamisha hili neno "inaweza" liondoke na isomeke kama hivi ifuatavyo:

"Kwamba Bodi itakaporidhika kuwa kumetumika utaratibu ambao sio wa kawaida unaotakiwa katika mitihani Bodi itasimamisha badala ya neno inaweza kusimamisha au kuikataa mitihani hiyo au sehemu inayohusika na hilo"

Lakini na kifungu cha 4 pia neno "inaweza nayo" iondoke ambapo badala yakusomeka kama hivi ilivyo isomeke kama hivi ifuatavyo:

"Kwamba itakapotokea zaidi ya thuluthi moja ya watihaniwa katika kituo cha mtihani kufanya mambo kinyume na masharti, Baraza litakataza kituo kupanga, kusimamia au kuwa wakala wa Bodi"

Hili neno linaweza kuhiarisha liondoke. Naomba kufanywe marekebisho hayo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Mwenyekiti, mimi nina wasi wasi kwamba itakuwa tumelifunga Baraza katika kufanya ule uchunguzi wa lile suala lililotokea, tunasema "inaweza kusimamisha" inakuwa inasimamisha kwa muda ikiona kwamba ipo haja ya kusimamisha.

Pengine uharibifu wenyewe sio mkubwa sana ni mdogo sana, inaweza kusimamisha halafu ikafanya uchunguzi wake. Ikitokezea kwamba jambo lile ni kubwa hapo tena Baraza ndio litakataa moja kwa moja. Niliona hiya maneno "inaweza" katika sheria naona wanasheria wanapenda kuyatumia, bila shaka yana hekma yake. Sisi tuliokuwa sio wanasheria hekma hizo hatuzijui, kuna hekma fulani ndio maana wanapenda kutumia hayo mambo ya "me". Nadhani wanasheria wanaweza kutusaidia zaidi kwenye hili.

Mimi ningeona tumeshakubali mengi haya mengine wengelituachia tukaendelea nayo Ishallah. Sisi tumekuwa wakarimu kili kinachosemwa tunakubali, tena matatizo ya nini.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, hiki kifungu kidogo cha 3 kimeanza kwamba "Baraza litakaporidhika" maana yake imeshafanya uchunguzi, imeshafanya kila kitu na ikaridhika kwamba utaratibu ambao sio wa kawaida katika mitihani na mambo mengine. Yaani itakapokuwa imesharidhika maana yake hili Baraza limeshafanya uchunguzi na limeridhika na hii hoja ndio maana yake. Sio kwamba isimamishwe kwa muda halafu bodi itakaporidhika kuwa kumetumika utaratibu sio wa kawaida unatumika katika mitihani. Hii yote Mhe. Mwenyekiti ni kuepusha haya mambo ambayo yametokea, ndio maana tukasema inaweza, kwa sababu unapozungumzia kitu inaweza maana yake ina hiyari. Lakini tayari hapa kesharidhika kwamba kuna mambo yamefanyika sio ya kawaida katika masuala ya mitihani.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, katika sheria Nam. 5 ya mwaka 1985 katika Baraza la Manispa ambapo kuna sheria iliyokuwemo mle imemtaka mkurugenzi wa Manispaa kukata miti na matawi katika mji na ikasema kwamba Mkurugenzi wa Manispaa anaweza kutoa kibali cha kukata miti ambayo imekaa katika hali ya hatari. Lakini sheria ya kukata miti au kibali cha kutoa miti ipo katika idara ya misitu ambayo wao ndio wanaotoa vibali. Kwa bahati wakati fulani Idara ya Misitu wamekataa kutoa kibali. Nikamuandikia mkurugenzi wa Manispaa kumuomba kwa kutumia kifungu hichi cha sheria ili Baraza la Manispaa sasa likubali kukatwa ule mti, Mkurugenzi atoe kibali ule mti ukatwe. Lakini mkurugenzi akanambia sheria hii haikunilazimisha imesema nnaweza kutoa, nnaweza nisitoe.

Kwa maana hiyo hili neno “inaweza” hili linamadhara yake tusione kwamba ni nyepesi, hii inamuhiyarisha mtu kufanya jambo na kuto kufanya jambo. Ndio maana tunakuwa hatuipendi katika sheria hasa kwa sisi. Kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri akubali hii kwenye hiki kifungu cha 3, basi hichi kifungu cha 4 tutamuachia. (*Vicheko*)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Ishallah kwa kuwa moja kachukua yeye na moja kanipa mimi nakubali. (*Vicheko*).

Kifungu cha 22 Viapo, Makosa na Adhabu Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 23 Kanuni.
Kifungu cha 24

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilitofautiana na maoni yaliyotolewa na kamati. Kamati ukisoma waraka wake umependekeza hichi kifutwe. Nilipochangia nikasema ukikifuta maana yake unazibakisha hizi kanuni. Sasa katika majumuisho yake Mhe. Waziri nilimfahamu kama vile yeye kaona kama mimi nimependekeza kama ilivyopendekezwa na Kamati. Lakini mimi nimetaka kibakie ili hizi kanuni zifutwe kutoa nafasi ile aliyoisema kwamba kutungwe kila kitu kipya na sasa kuna utaratibu mpya. Kwa hivyo nilikuwa nataka nieleweke hivyo.

Kwa sababu tunafunga majumuisho Mhe. Mwenyekiti naomba niseme Mhe. Waziri pamoja na kumsimamisha sana lakini tunamshukuru kwa mashirikiano yake na namuhakikishia sheria hii itakuwa moja katika *league* zake katika kipindi kifupi alichokitumia alivyokuwa Waziri wa Elimu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Aahh! Hamna tatizo. (*Vicheko*)

Kifungu cha 24 Kufuta na Kubakiza Pamoja na Marekebisho Yake

(Baraza lilirejea)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza zima imeupitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake sasa naomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa Iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Vipini na Tathmini ya Elimu Zanzibar usomwe mara ya pili.

(Hoja ilitolewa Iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

Mhe. Spika: Ahsante sana. Namshukuru Mhe. Waziri, wanashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote kwa mashirikiano makubwa tuliyompa Mhe. Waziri katika kukamilisha kazi hii. Nataka niyatumie maneno ya Mhe. Jussa kwamba kazi hii anayomalizia katika Wizara ya Elimu itamuwekea kumbukumbu nzuri katika Wizara hii.

Lakini kwa sababu ya usoefu huo nadhani na kwa sababu serikali inafanya kazi kama timu moja ataendelea kusaidia hapa na pale inatokea haja ya kufanya hivyo. Waheshimiwa Wajumbe sasa naakhirisha kikao hichi hadi saa 11:00 jioni.

(Saa 7:00 Mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Utalii 2012

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Kny: Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa idhini yako nichukue fursa hii na kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo nichukue fursa hii kuwasilisha Mswada wa Marekebisho ya Sheria Nam. 6 ya Utalii ya 2009. Lakini kabla ya kufanya hivyo nichukue fursa hii vile vile na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Magogoni kutoa salamu za rambi rambi kwa aila ya marehemu Salim Amour Mtondoo. Mwenyezi Mungu ailaze, amsamehe na ampe kila rehma huko aliko.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nichukue fursa hii kutoa pongezi na hongera kwa Mhe. Mohammedraza Hasanali Mohamedali kwa kuchaguliwa kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Uzini, natumai salamu zitafika. Baada ya nasaha hizo naomba niwasilishe mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu la Wawakilishi kinachofuatia hapa ni kuwasilisha warka huu wa marekebisho ya sheria Nam. 6 ya utalii. Waheshimiwa Wajumbe kama tunavyoelewa kwamba mikakati mikubwa ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kiuchumi imeelekea zaidi kwenye dira ya 2020 pamoja na dira ya MKUZA na vyote hivyo vinalenga katika kuleta uchumi na kupunguza umasikini kwa wananchi wake. Lakini pamoja na kupunguza umasikini huo mikakati hii imeangalia zaidi sekta mbili muhimu ambazo ndizo mihimili mikubwa ya kiuchumi kwa nchi yetu, nayo ni utalii na biashara. Kwa hivyo, imeona kwamba ili kuhakikisha utalii unaleta tija ni wajibu kwanza utalii wenyewe kwa vile ndio muhimili wa kutegemewa kiuchumi kwa Zanzibar na kupunguza umasikini, basi la kwanza ni kuweka utalii wenyewe katika mazingira sahihi yenye kukubalika na ambayo yanaweza yakaleta tija kwa wote. Mhe. Spika, vile vile ni kuutangaza utalii wetu kwa maana ya kutangaza vivutio vyote tulivyonavyo ndani ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika miaka ya karibuni tu sekta hii ya utalii ilikumbwa na matatizo makubwa na mengi ya kidunia, na miongoni mwa matatizo hayo yalikua ni matatizo ya ugaidi lakini vile vile kulikua na matatizo ya kiuchumi ya dunia na mabadiliko ya tabia ya ndani ya nchi. Vile vile kulikua na majanga mbali mbali ambayo yametokezea duniani kote. Haya yote yalipelekea sekta hii ukuaji hafifu.

Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe matatizo haya kwa ujumla wake yameleta mabadiliko ya kidesturi ya masoko duniani, lakini vile vile namna ya watu wanavyozidi kusafiri na kusababisha ukuaji wa masoko mapya ambayo hayakutarajiwa katika dunia ya utalii. Kwa hivyo, kutokana na mabadiliko ya tabia za watu na uchumi wa baadhi ya nchi imeletea watu wengi kua na hamu ya kusafiri. Kwa hivyo, imetuletea masoko mapya kabisa kama vile masoko ya Asia ya Kusini na Afrika, hivyo Serikali nyingi duniani zimegutuka na zimeamua kwamba sekta ya utalii haifai kuachwa peke yake, na bila ya usimamizi thabiti wa Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi. Mhe. Mwenyekiti, dhana kubwa ni kuhakikisha kwamba tunakua na bidhaa ya utalii madhubuti na chombo madhubuti kitakachohimili vishindo vya ushindani na mtikisiko wa dunia.

Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe kutokana na mabadiliko ya kidunia imepelekea sheria tuliyonayo hivi sasa kua na mapungufu ambayo yanahitaji kurekebishwa ili kuhakikisha tunafikia malengo. Mhe. Mwenyekiti, madhumuni ya mswada huu ni kufanya marekebisho kwa baadhi ya vifungu vya sheria vya utalii Nam. 6 ya 2009, naamini mabadiliko haya itaipa nguvu Serikali kutaka kusimamia na kuendeleza utalii wenye tija kwa manufaa ya umma.

Kwa ufupi ni kwamba labda nisome vifungu ambavyo tumevifanyia marekebisho katika mswada huu ni kifungu cha 2 ambacho sasa kama mtaangalia mswada wa zamani mtaona kulikua na bodi, lakini sasa badala yake marekebisho yamekuja kutakua na mwenyekiti na Mwenyekiti maana yake ni Mwenyekiti wa Kamisheni aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 5 (1a) cha sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile katika mabadiliko hayo kutakua na Katibu Mtendaji maana yake ni Katibu Mtendaji aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 11 cha sheria hii. Vile vile Kamishna maana yake ni mtu atakaeteuliwa chini ya kifungu cha 5 (1b) cha sheria hii. “Neno mtalii” maana yake ni mtu ambaye yupo katika sehemu ambayo sio makaazi yake lakini yupo kwa ajili ya kazi, mapumziko au starehe. Vile vile tafsiri ya “biashara ya utalii” imetafsiriwa kwamba ni biashara yoyote inayotoa huduma kwa watalii inayohusu mkahawa, mambo ya muziki, hoteli, nyumba za wageni, chumba, watembeza wageni, maduka ya utalii, waongozaji watalii, maeneo ya kufuga wanyama, mafugio ya viumbe wa baharini kwa maonesho, biashara ya kutoa taarifa kwa watalii, jumuiya za kitalii,

wakodishaji baiskeli, vyombo vya moto, vyombo vya baharini, vyombo vya michezo vya baharini kwa watalii, maeneo ya kuegesha vyombo vya baharini na shughuli nyengine zinazofanana na hizo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hicho kuna "muongoza watalii" maana yake ni mtu anayetoa taarifa kufahamisha au kuelekeza watalii kwa malipo kuhusu maeneo, uoto, tamaduni, uwasili, jiografia, historia na mambo yanayofanana na hayo yaliyomo ndani na kuhusiana na Zanzibar. Vile vile imetoa tafsiri ya "Mzanzibari" maana yake ni Mzanzibari kama alivyotafsiriwa katika sheria ya Mzanzibari Nam. 5 ya mwaka 1985.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 4 kimefanyiwa marekebisho kama yafuatayo:-

Kifungu cha (a). Kuanzisha kanuni za maadili na viwango kwa ajili ya uendeshaji shughuli za utalii na kusimamia utekelezaji wa kanuni hizo na viwango.

Kifungu cha 5 (a) vile vile kimefanyiwa marekebisho kamisheni itakua na mambo yafuatayo:

(a) Mwenyekiti atakayekua Mkuu wa Kamisheni kwa wote na ambaye atateuliwa na Rais
(b) Makamishna wengine wasiozidi sita watakaoteuliwa na Waziri kutoka:
(i) Wadau wa utalii;
(ii) Jumuiya ya watembezaji na kusafirisha watalii;
(iii) Tume ya mipango ya Zanzibar;
(iv) Mkurugenzi Mipango, Sera na Utafiti wa Wizara yenye dhamana ya utalii;
(v) Mamlaka ya ya kukuza uwekezaji ya Zanzibar;
(vi) Mjumbe mwengine yeyote ambaye atakua ni mwanamke.

Kifungu cha 5 (2). Mwenyekiti atakua madarakani kwa muda wa miaka minne kuanzia tarehe ya kuteuliwa, na anaweza kuteuliwa tena.

Kifungu cha 5 (3). Mtu hatoweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti mpaka awe:

(i) Na utaalamu wa kipekee katika fani inayofanana na utalii, uongozi wa wadau wa utalii au uhusiano wa kimataifa;
(ii) Ujuzi wa kutosha wa kupigania mambo;
(iii) Mahusiano mazuri na watu
(iv) Na taaluma nyengine inayoendana na hiyo ambayo ni muhimu katika sekta ya utalii Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, marekebisho mengine ni kifungu cha 6 (1) kutakua na Mwenyekiti wa Kamisheni atakua sio mkuu wa utawala, na atafanyakazi zifuatazo:

(a) Kutoa maelekezo ya mikakati kwa uongozi katika kuendeleza na kukuza biashara ya utalii;
(b) Kuwa mbele katika kuanzisha dhana ya utalii kwa wote;
(c) Kusimamia utekelezaji wa sera ya utalii na kutoa miongozo kwa uongozi juu ya utekelezaji wa sera hiyo;
(d) Kuwa Mwenyekiti wa mkutano wa Makamishna na wadau wa utalii;
(e) Kushauri na kuchukua hatua za kuanzisha mikakati kwa lengo la kuwashajiisha wananchi katika kujihusisha na biashara ya utalii ili waweze kupata manufaa kutokana na utalii;
(f) Kufanya jambo jengine lolote ambalo linaenda sambamba au linaendana na majukumu yake ya jumla.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu hicho hicho cha 6 (2). Ili kuondoa shaka, inaelezwa wazi kwamba Mwenyekiti hatofanya kazi za kiutawala za Kamisheni, ambazo kazi hizo zimewekwa chini ya mamlaka ya Katibu Mtendaji.

Kifungu cha 6 (3). Mwenyekiti atawajibika kwa Waziri na

Kifungu cha 6 (4). Mshahara na mafao ya Mwenyekiti baada ya kumaliza kazi yatakua kwa mujibu wa sheria ya utumishi wa umma, Nam. 2 ya 2011 kulingana na masharti ya uteuzi wake.

Mhe. Mwenyekiti, marekebisho mengine ni kifungu cha 7 (1) ambayo sasa yatakua. Makamishna kwa pamoja watakuwa wajumbe wa Kamisheni na watakuwa na majukumu yafutayo:

(a) Kuwa washauri wa wakuu wa Serikali na uongozi wa Kamisheni kwa mambo yote yanayohusiana na maendeleo, taratibu, kukuza na kuendeleza biashara ya utalii na huduma zinazoendana na utalii;
(b) Kuwa mstari wa mbele katika kukuza shughuli za utalii wa ndani, kikanda na kimataifa;
(c) Kusimamia uendelezaji na utekelezaji wa dhana ya utalii kwa wote na
(d) Kutoa miongozo kwa ujumla katika uongozi wa Kamisheni na wadau wa utalii.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 7 (2) ni. Uwezo wa Kamisheni ulioelezwa chini ya sheria hii, isipokua kama imeelezwa vyenginevyo, utatekelezwa kwa makubaliano ya Makamishna kupitia vikao vitavyoitishwa kwa mujibu wa taratibu zao.

Mhe. Mwenyekiti, lakini wanaweza kukutana wakati wowote itakapotokea haja ya kufanya hivyo. Vile vile kifungu cha 8 (2) akidi ya kikao cha Makamishna itakua zaidi ya nusu ya idadi ya Wajumbe wote wa Kamisheni.

Kifungu cha 8 (3). Vikao vyote vya Makamishna vitaongozwa na Mwenyekiti, lakini akiwa hayupo Makamishna waliohudhuria watamteua mmoja wao kuongoza kikao hicho.

Kifungu cha 8 (4). Kwa kufuta masharti ya sheria hii, Makamishna wanaweza kupanga utaratibu wa vikao vyao.

Vile vile kifungu cha 9 kimefanyiwa marekebisho kimefutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

Kifungu cha 9. Uamuzi wa Makamishna utakua kwa kukubaliana lakini ikiwa watashindwa kufikia makubaliano katika ajenda yoyote, ajenda hiyo itaamuliwa kwa kura na ikitokea kura sawa Mwenyekiti atakua na kura ya uamuzi. Kifungu hicho hicho kinaongezwa kifungu kipya cha 9 (a) nacho kinasema. Makamishna watalipwa mafao kama Waziri atakavyoamua.
Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 10 nacho kimefanyiwa marekebisho kimeeleza pale katika kifungu cha (a). Katika kijifungu cha (1) kwa kufuta maneno “Bodi kwa ajili ya kuzingatiwa na kuidhinishwa” na badala yake kuweka maneno “Kamisheni itaandaa mpango mkakati, mpango kazi na mpango wa kuendeleza na kukuza utalii kwa kila mwaka kwa kushirikiana na wadau wengine wa utalii na kuwasilisha kwa Makamishna kwa ajili ya kuzingatiwa na kwa Waziri kwa ajili ya kuidhinishwa”. Vile vile mipango itaonesha wazi wazi muelekeo na malengo kwa kipindi, mipango ya utekelezaji, mikakati na fursa katika utalii.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 11 kitafutwa na kuandikwa kama ifuatavyo:
Kifungu cha 11 (1). Kutakua na Katibu Mtendaji badala ya Mkurugenzi Mkuu ambaye atakua mtendaji mkuu wa Kamisheni atakayeteuliwa na Rais. Vile vile mtu hatofaa kuteuliwa kua Katibu Mtendaji mpaka awe na sifa zifuatazo:

(a) Awe na angalau shahada ya kwanza au elimu inayolingana na hiyo na uzoefu wa kazi kwa kipindi kisichopungua miaka saba au
(b) Awe na taaluma ya kutosha na uzoefu katika masuala ya utalii au usimamizi wa biashara au uchumi au masuala ya sheria na awe mweledi wa mambo ya uongozi.

Kifungu cha 11 (3). Katibu Mtendaji atakua na mambo yafuatayo:

(a) Atakua Mkuu wa Sekretarieti ya Kamisheni;
(b) Atakua msimamizi wa kazi za kila siku juu ya utendaji wa Kamisheni;
(c) Mwenye dhamana ya usimamizi wa fedha, mali na shughuli za Kamisheni;
(d) Msimamizi wa udhibiti wa maofisa na watumishi wa Kamisheni;
(e) Mwenye dhamana ya uhifadhi wa muhuri na kumbukumbu na nyaraka zote za Kamisheni
(f) Atakayewajibika kwa Kamisheni.

Kifungu cha 11 (4). Katibu Mtendaji atahudhuria vikao vyote vya Kamisheni na kifungu cha 11 (5). Kutakua na Wakurugenzi wa Idara za Kamisheni watakaoteuliwa na Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 11 vile vile kinaongezwa kifungu kipya cha 11a (1) ambacho kinasema: Kuanzishwa mkutano wa wadau wa utalii utakaofanyika kila baada ya miezi sita kuzungumzia mambo yanayohusu maendeleo ya utalii.

Kifungu cha 11 (2). Mwenyekiti wa Kamisheni atakua Mwenyekiti wa mkutano wa wadau wa utalii. Na kifungu cha (3). Mkutano wa wadau wa utalii utafanya kazi zifuatazo:

(a) Kutoa mawazo na mapendekezo kwa jambo lolote linalohusiana na kukuza na kuelekeza biashara ya utalii;
(b) Kuishauri Kamisheni na Serikali juu ya mambo yenye faida au manufaa katika kukuza na kuendeleza utalii;
(c) Kupendekeza hatua muhimu za kukuza na kuendeleza utalii;
(d) Kufanya kazi nyengine ambayo inaenda sambamba na kazi za msingi za mkutano.

Kifungu cha 11 (4). Kwa kufuata kanuni zitakazotungwa na Waziri kuhusiana na utaratibu wa kufanya kazi za mkutano wa wadau, mkutano huo unaweza kujipangia taratibu zake wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 12 vile vile kinarekebishwa katika kijifungu cha 2 kwa kufuta aya ya (a) na kuweka aya mpya nacho kinasema:

(a) Kiwango chengine cha fedha kama ruzuku kama kitakavyotengwa na Baraza la Wawakilishi.

Na kifungu cha 13 kinafutwa na kifungu cha 14 nacho kimefanyiwa marekebisho kwa kufuta neno “Bodi” na badala yake kuweka neno “Mwenyekiti”. Mwenyekiti sio zaidi ya miezi mitatu kabla ya kufungwa mwaka wa fedha atawasilisha kwa Waziri taarifa ya mwaka juu ya kazi za Kamisheni na taarifa ya ukaguzi kwa mwaka huo wa fedha.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 15 kinarekebishwa kwa kufuta kifungu cha 2 (2) na badala yake kuwekwa kipya na kitakua kama ifuatavyo:

Kwa mujibu wa kijifungu cha (2) cha kifungu hiki, mtu hatakiwi kuendesha au kufanya biashara au kujitangaza kama anafanya biashara ya utalii mpaka awe na leseni ya biashara ya utalii iliyotolewa na Kamisheni.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 16 kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) Katika kijifungu cha (1) kwa kufuta maneno “Mkurugenzi Mkuu” linaondoka na badala yake kuweka maneno “Katibu Mtendaji”. Kwa hivyo, Katibu Mtendaji atatoa leseni kwa mtu atakayefanya biashara ya utalii baada ya kukamilisha masharti yaliyoelezwa chini ya sheria hii.

Mhe. Mewnyekiti, kifungu hicho hicho (3). Endapo kama leseni iliyotolewa chini ya kifungu hiki itapotea au itaharibika, Kamisheni inaweza kutoa nakala ya leseni hiyo baada ya kulipwa ada iliyoelezwa katika kanuni. Na (4) kila leseni iliyotolewa chini ya sheria hii itawekwa katika sehemu ya wazi ndani ya sehemu ya biashara inayohusika na leseni hiyo na pale itakapohitajika kwa ukaguzi wa ofisa aliyeidhinishwa atatakiwa kuionesha.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 17 kinarekebishwa kwa kufuta neno “Bodi” na badala yake kuweka neno “Kamisheni”. Kamisheni baada ya kupokea maombi ya leseni itaweza kutoa tena au kubadilisha masharti ya biashara kwa namna ya masharti kama ilivyoombwa baada ya malipo ya ada iliyowekwa na Kamisheni.

Vile vile kifungu cha 18 kinarekebishwa kama ifuatavyo: Kila mmiliki wa hoteli au nyumba ya kulala wageni atatakiwa kuweka daftari la kumbukumbu ambalo litakua na jina, uraia na makaazi ya kila mtu anayehudumiwa kama mgeni peke yake au akiwa na mtu mwengine pamoja na nambari au jina la chumba alichopanga, tarehe ya kuingia na kutoka.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu ya pili ya kifungu hicho hicho 18 kila mmiliki wa hoteli au nyumba ya kulala wageni atalazimika kua na uongozi unaotambulika na Kamisheni iwe inaongozwa na mmiliki au mtu mwengine aliyeajiriwa

na mmiliki na endapo kutakua na mabadiliko ya utawala Kamisheni aijuilishe ndani ya siku 30 baada ya mabadiliko haya.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 19 kinaongezwa kifungu kipya cha 19a (1) ambacho kinasema: Mtu aliyeruhusiwa kufanya biashara ya utalii hatofanya mabadiliko katika ofisi yake au jengo, wanahisa au wakurugenzi, jina la biashara au huduma anayoitoa mpaka awasilishe kwa Kamisheni maelezo ya mapendekezo ya mabadiliko au marekebisho yanayokusudiwa kwa maandishi.

Kifungu cha 19 (2). Endapo Kamisheni itaridhika na mapendekezo ya marekebisho yanayokusudiwa inaweza kuruhusu kwa maandishi kufanyika kwa mabadiliko hayo au Kamisheni inaweza kufanya marekebisho ya ziada katika mapendekezo ya marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 23 vile vile kinaongezwa kifungu kipya cha 23a na 23b nacho kinasema kama ifuatavyo:

Kifungu cha 23a (1). Kutakua na Kamati za Utalii za Wilaya katika Wilaya zitakazokua na wajumbe kutoka katika taasisi zifuatazo:-

(a) Ofisa Mkuu wa Polisi wa Wilaya;
(b) Mwenyekiti wa Masheha katika Wilaya;
(c) Mtu mmoja kutoka taasisi ya Makumbusho na Mambo ya Kale;
(d) Mfanyabiashara katika Wilaya;
(e) Mkulima katika Wilaya;
(f) Mtu mmoja kutoka jumuiya ya wafanyabiashara ya utalii katika Wilaya;
(g) Mtu mmoja kutoka Wizara ya Ardhi;
(h) Mtu mmoja kutoka Wizara ya Mazingira;
(i) Mtu mmoja kutoka Jumuiya ya Kiraia ndani ya Wilaya;
(j) Viongozi wa kidini katika Wilaya na
(k) Mtu mmoja kutoka Mamlaka ya Kukuza Vitega Uchumi.

Katika kifungu hicho hicho cha 23 (2). Kamati za Utalii za Wilaya zitashirikiana na Kamisheni kwa ajili ya kusukuma mbele maendeleo ya utalii ndani ya Wilaya.

Kifungu cha 23 (3). Mkuu wa Wilaya atakua Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii ya Wilaya katika Wilaya yake na Ofisa wa Utalii wa Wilaya atakua Katibu wa Kamati hiyo katika Wilaya yake.

Kifungu cha 23 (4). Kamisheni kwa kushirikiana na wadau muhimu wa utalii, itaandaa miongozo kwa Kamati za Utalii za Wilaya.

Kifungu cha 23 (5). Kamisheni itaratibu na kutoa fedha kwa utekelezaji wa kazi kwa Kamati za Wilaya.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 23b (1). Kamati za Utalii za Wilaya zitatekeleza majukumu yafuatayo:

(a) Kuendeleza dhana ya utalii kwa wote;
(b) Kulinda usalama na amani kwa wageni na jamii katika maeneo ya utalii;
(c) Kuanzisha mfuko wa fedha kwa wananchi kwa njia ya michango ya hiari ambazo zitatumika kwa maendeleo ya vijiji;
(d) Kuunga mkono jumuiya za kiraia zinazofanya shughuli za utalii na kuzisaidia kwa kujihusisha katika mipango yao kwa kushauriana na Kamisheni na wadau wengine wa utalii;
(e) Kulinda, kuendeleza na kukuza utamaduni wa kiasili wa Zanzibar kama ni sehemu ya bidhaa ya utalii;
(f) Kulinda sifa ya kimaadili katika Wilaya;
(g) Kuwa kama kiungo baina ya utalii na sekta nyenginezo;
(h) Kupandisha thamani kwa bidhaa za ndani na
(i) Kuimarisha uelewa wa wananchi na kua kama zana ya utalii kwa wote.

Kifungu cha 23 (2). Kwa mujibu wa kijifungu cha (1) cha kifungu hiki, Kamati za Utalii za Wilaya zitaanzisha mipango kazi ya mwaka na mikakati ya utekelezaji wake itakayowasilishwa kwa Kamisheni kwa kuidhinishwa.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 23 (3). Mtu yeyote anayefanya biashara ya utalii aliyeajiri mtu ambaye sio Mtanzania kutoa huduma iliyoelezwa chini ya kijifungu cha (1) cha kifungu hiki, lazima apate ruhusa ya maandishi kutoka kwa Waziri, baada ya kumthibitishia Waziri kua hakuna wa ndani wa kujaza nafasi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 25 vile vile kinarekebishwa kwa kufuta neno "nyumba ya kuuzia ulevi" badala yake kufunga duka lolote, mkahawa, hoteli au biashara yoyote itayofanywa bila ya leseni au kibali cha maandishi kinachohitajika chini ya sheria hii.

Pia kifungu cha (c) atakayekataa kuonesha leseni au kutoa maelezo au atakayeshindwa kufika mbele ya Kamisheni baada ya kutakiwa kufanya hivyo na Ofisa aliyeidhinishwa na Kamisheni.

Mhe. Mwenyekiti, utakuta kuna kifungu cha 28 ambacho nacho kimefanyiwa marekebisho na kufuta sehemu ya (c) atakayekataa kuonesha leseni au kutoa maelezo au kushindwa kufika mbele

Mhe. Mwenyekiti, hayo yalikuwa ni marekebisho ya Muhtasari wa Sheria Nam. 6 ya Mwaka 2009 kwa Kamisheni ya Utalii. Naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

Mhe. Asha Bakari Makame (Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama mbele ya Baraza lako tukufu, nikiwa mzima wa afya. Pia nikushuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusu Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Utalii Namba 6 ya mwaka 2009.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati yangu napenda kuchukua fursa hii kutoa mkono wa pole kwa Baraza lako tukufu kwa ndugu na familia ya Marehemu Mhe. Salum Amour Mtondoo, kutokana na kifo cha mjumbe huyo kilichotokea tarehe 15/3/2012, tunamuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema Peponi **Amin**.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii, kutoa shukurani za dhati kwa Wajumbe wa Kamati, watendaji wa Wizara ya Habari, Utamaduni Utalii na Michezo pamoja na wanasheria wetu wa Baraza na Serikali kwa michango, miongozo na ufafanuzi wao kwa baadhi ya mambo wakati wa kuujadili mswada huu. Napenda kuwataja Wajumbe wa Kamati hii.

1. Mhe. Asha Bakari Makame - Mwenyekiti
2. Mhe. Moh'd Said Moh'd - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Mzee Ali - Mjumbe
4. Mhe. Asaa Othman Hamad - Mjumbe
5. Mhe. Abdi Mosi Kombo - Mjumbe
6. Mhe. Kazija Khamis Kona - Mjumbe
7. Mhe. Salim Abdalla Hamad - Mjumbe
8. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Mjumbe
9. Nd. Haji Khatibu Haji - Katibu
10. Nd. Asma Ali Kassim - Katibu

Mhe.Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii adhimu kutoa pongezi za dhati kwa uongozi mzima wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kuona umuhimu wa kuleta mswada huu, ambapo pindi utakapopitishwa unatarajiwa kuleta mabadiliko makubwa katika sekta ya utalii, kwa vile utamshirikisha moja kwa moja mwananchi wa Zanzibar.

Mhe.Mwenyekiti, Mswada huu unakusudia kufanya marekebisho ya Sheria ya Utalii Namba 6 ya mwaka 2009 inayorekebishwa kwa kufuta muundo wa Uongozi uliopo sasa wa Kamisheni ya Utalii, na kuweka muundo mpya utakaobeba dhima ya "Utalii kwa wote".

Mhe.Mwenyekiti, Sekta ya Utalii ni sekta kiongozi inayoiingizia nchi yetu fedha nyingi za kigeni kwa asilimia 80%. Hata hivyo, sekta hiyo bado imekuwa ikikumbwa na changamoto nyingi zikiwemo za uvujaji wa mapato yanayotokana na utalii, pamoja na ukosefu wa takwimu sahihi za watalii wanaoingia hapa nchini. Hivyo basi, ni jukumu la Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kuhakikisha kuwa marekebisho ya sheria hii ya utalii yanakwenda sambamba na utatuzi wa changomoto hizo sugu, ili Sekta hii ya Utalii ilete tija na manufaa zaidi kwa nchi yetu na watu wake.

Mhe.Mwenyekiti, Mswada huu unalenga kuleta mabadiliko makubwa ya mfumo wa utendaji na uendelezaji wa shughuli za utalii, hasa kwa vile mfumo huo mpya unatoa fursa zaidi kwa wananchi kushirikishwa moja kwa moja katika shughuli za kusimamia na kuendeleza utalii, kutokana na ukweli kuwa mfumo huo wa kusimamia shughulli za utalii utapewa hadi ngazi za wilaya. Kwa mnasaba huo basi, Serikali haina budi kutoa kipaumbele maalum cha kutoa taaluma ya kutosha kwa wananchi wenyewe kwa kuhamasisha kuwa utalii ni wao, na hivyo wana jukumu la kuusimamia, kuulinda na kuuendeleza ndani ya nchi yao. Aidha, watendaji wa Serikali wanaohusika na utalii huo, hawana budi kubadilika, nitarudia, hawana budi kubadilika na kuachana na mfumo wa zamani.

Mhe.Mwenyekiti, kamati yetu imeupitia kwa kina mswada huu, ambapo kimsingi imekubaliana na mapendekezo ya rasimu ya mswada huu. Hata hivyo, imefanya mabadiliko kadhaa ya kimaandishi na yale ya msingi kwa lengo la kuufanya mswada huu uwe bora zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nieleze baadhi ya marekebisho ya msingi ambayo kamati yetu inaona yangefaa kufanyiwa mabadiliko.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza ukurasa wa 42 kifungu cha 5(2) kinachoeleza kuwa Mwenyekiti ambaye atakuwa Mkuu wa Kamisheni ya Utalii, atakaa madarakani kwa muda wa miaka minne na anaweza kuteuliwa tena**.**

Kamati inapendekeza kuwa Mwenyekiti wa Kamisheni akae madarakani si zaidi ya vipindi viwili. Hii ni kwa sababu kamati inaona kuwa katika nchi ya kidemokrasia na inayofuata misingi ya Utawala Bora kama yetu, ni vyema kwa kiongozi kuwekewa ukomo wa muda wa kukaa madarakani.

Vile vile kamati inaiomba Serikali kuliangalia upya suala la mafao ya Mwenyekiti, kwani Mwenyekiti huyo kwa mujibu wa kifungu cha 6(4) atalipwa mshahara na mafao baada ya kumaliza kazi kwa kufuata sheria ya Utumishi wa Umma. Hivyo Mwenyekiti huyo mmoja atakuwa anapokea mafao kila baada ya miaka minne kwa vile anaweza kuendelea kuteuliwa tena.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 42 kifungu cha 5(3) kinaelezea sifa zinazofaa kwa mtu kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamisheni ya Utalii. Hata hivyo, katika sifa hizo kifungu hicho hakikuweka sifa ya kuwa Mzanzibari, narudia, hakikuweka sifa ya kuwa Mzanzibari.

Hivyo kamati inapendekeza kuongezwa kwa kifungu chengine kidogo cha 5(3) (v) kitakachotaja sifa ya kuwa Mzanzibari kama ni miongoni mwa sifa zinazofaa kwa mtu kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamisheni, kwa maana ya kuwa ni lazima awe Mzanzibari. Hii inatoa kipaumbele zaidi kwa mzalendo yeyote mwenye sifa ya kuweza kushika nafasi hiyo muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, katika Mswada huu ukurasa wa 48 kifungu cha 23(a) kimetaja Kamati za Utalii za Wilaya, na pia kimeainisha watu mbali mbali watakaounda kamati hizo za utalii za wilaya. Kamati katika kipengele hiki inapenda kutoa indhari kwa serikali kuwa makini katika kufanya uteuzi wa Wajumbe wataounda kamati hizo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hicho hicho cha 23a (1) pamoja na kuainisha wajumbe mbali mbali watakaounda Kamati za Utalii za Wilaya, kamati imeona ni vyema akaingizwa muhusika wa masuala ya utamaduni katika kamati hizo. Hivyo kamati inapendekeza kuongezwa kwa kifungu chengine kidogo cha 23a (1) (i) kitakachomjumuisha Ofisa wa Utamaduni wa Wilaya. Hii ni kwa sababu ofisa huyo atasaidia kufanikisha utekelezaji wa jukumu moja kati ya majukumu muhimu ya kamati hizo za utalii za wilaya, ambalo ni kulinda, kuendeleza na kukuza utamaduni wa kiasili wa Zanzíbar, kama ni sehemu ya bidhaa ya utalii, kama lilivyoelezwa katika kifungu cha 23(1)(e).

Mhe. Mwenyekiti, kamati imebaini kuwa katika kifungu hicho hicho cha 23a (1) hakikutaja mwenye mamlaka ya kuteua wajumbe wa Kamati za Utalii za Wilaya. Hivyo kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho kifungu hicho

kwa kufafanua kuwa, Wajumbe wa Kamati za Utalii za Wilaya watateuliwa na Waziri kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya husika.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 49, kifungu cha 23, marekebisho ya kifungu cha 24(3) kimempa uwezo waziri kutoa ruhusa ya maandishi kwa mtu yeyote anayefanya biashara ya utalii, aliyeajiri mtu ambaye si Mtanzania baada ya Waziri kuthibitisha kuwa hakuna mtu wa ndani wa kujaza nafasi hiyo. Kamati inapendekeza kuwa mamlaka hayo iachiwe Kamisheni yenyewe ili kumpunguzia kazi Mhe. Waziri na kuepusha mlundikano wa maombi utaopelekea kuwepo kwa uchelewaji wa kupata majibu ya maombi hayo, yakisubiri idhini ya Mhe. Waziri ambaye ni mtu mwenye majukumu mazito ya kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu pia imebaini kuwepo kwa tafsiri isiyo sahihi ya maneno "Katibu Mtendaji**"** kwenda katika lugha ya Kiingereza. Hivyo, kamati inapendekeza kuwepo tafsiri sahihi ya maneno hayo ambayo ni "*Executive Secretary*" na sio "*Executive Director***"** kama ilivyoandikwa katika mswada.

Mhe. Mwenyekiti, marekebisho mengine madogo madogo yakiwemo ya kimaandishi na uchapaji yameshachukuliwa na wanasheria wetu, kama yanavyoonekana katika karatasi ya marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu inaunga mkono Mswada huu na inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wachukue nafasi hii kutoa maoni, kadri watakavyoona inafaa na hatimae kuunga mkono na kuupitisha Mswada huu muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaondoka kwa mujibu wa kanuni ya 83(8) naomba nichangie kidogo. Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwa jumla kwa sababu katika ziara zetu mbali mbali ambazo tunashughulikia hizi wizara, hasa wizara zangu, naomba sana kuna baadhi ya watendaji pamoja na wakurugenzi ni wakaidi unapowaambia mambo.

Kwa hivyo, naomba nitanabahishe, nitahadharishe, nitoe indhari, unapokuwa wewe ni katibu na una waziri wa *CUF* basi uhakikishe kwamba huyo waziri wa *CUF* anatumia ilani ya Chama cha Mapinduzi kutekeleza wajibu wake katika serikali hii ya Chama cha Mapinduzi. Haina maana kwamba Waziri wa CCM na Waziri wa *CUF* kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi tuna Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Ni vyema tukafanya wajibu wetu kwa mujibu wa taratibu na kwa mujibu wa uwezo mtu alionao, si vyema kuitia itikadi kwa sababu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, atakuja kupima vipi kipindi cha miaka mitano katika kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba sana watendaji, tuhakikishe tunakwenda sambamba na mambo ya utendaji hatutii itikadi. Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kuweza kunipa nafasi ya kuchangia Mswada huu wa Marekebisho ya Sheria ya Utalii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi niunge mkono hoja ya kamati, na tutamhakikishia Mwenyekiti kuwa tutaipitisha kwa kura zote asiwe na wasi wasi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo nina mengi sana na ningeomba uniachie hata kama dakika 50, lakini unipe fursa leo niweze kutoa vitu ambavyo vya uhakika na kwa nia ya kuwakomboa Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, naanza na mlezi wangu wa katiba. Katika ukurasa wa 42 namtafuta nani Mzanzibari, kifungu hicho cha nambari 5 naingia katika katiba. Katiba yetu inasema tukianzia kifungu cha 6(1) lakini tunakiacha hicho twende katika kifungu cha 6(2) kinachosema kwamba:

> "Kila Mzanzibari, kwa misingi ya katiba hii, ataweza kufaidi haki na fursa zote anazostahiki Mzanzibari, na atapaswa kutekeleza wajibu, majukumu na dhamana za Mzanzibari kama ilivyo kwenye katiba hii au kwenye sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi".

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nikiangalia hizo fursa zenyewe na hususan katika masuala haya ya utalii, naona Mzanzibari fursa zake hajapewa kwa mujibu wa katiba hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi siku hizi huwa *alert* sana, ninakuwa na wasiwasi kupitisha vitu halafu baadae vikaja vikanirudi mwenyewe, hiki ni kitu ambacho mimi nakuwa mnyonge sana. Nitaonekana mkaidi lakini si mkaidi, ndio haki yenyewe ilivyo, kila unavyomsomesha mtu pengine mimi nitamshinda mwalimu wangu aliyenisomesha, kwa bahati mbaya leo mwalimu wangu mmoja hayupo hapa Mwanasheria, na leo tumemsomesha kidogo, hiyo ndio hali halisi ilivyo.

Lakini sasa ninachotaka kusema tuitafute haki ya Mzanzibari tutaikuta huko, lakini kwanza mimi niliutafuta mswada huu kuna mambo lazima tuyaangalie. Kuna vitu ambavyo waziri amenyimwa katika mambo haya, yeye ana utalii lakini sheria hana. Sheria hii iko sehemu ya kazi huko kunako sehemu ya waziri mwengine, sasa hapa hatuoni kwamba hiki ni kitu mchanganyiko? Waziri ana utalii tu, lakini sheria ya wafanyakazi imo katika wizara nyengine. Mimi naona na hii tungefanya marekebisho tukawaondoa kule tukawaleta huku tusione tabu, najuwa Mhe. Waziri ataona sasa anataka kuninyang'anya, simnyang'anyi namsaidia kazi.

Kwa sababu utakuta waziri anajitahidi, lakini sasa anashindwa na sheria, kuna mambo mengine hawezi kutumia sheria, tutayakuta mbele katika mswada huu athari zake.

Mhe. Mwenyekiti Mzanzibari tunamtafuta huko mbele ya safari tutamkuta tu, vipi haki zake tunavyompotezea. Mhe. Mwenyekiti, kwa unyonge sana na hili neno nataka niliseme katika kifungu cha 4(a) 'kuongeza aya' nikiisema hivi aya kama nilivyosema juzi basi mwili unanisisimka. Leo nimejaribu kutafuta tafsiri ya aya na ni tangu juzi kila shehe ninayemwendea ananambia tafsiri ya aya ilivyo, kuna mmoja aliniletea simu akanambia aya tafsiri yake ni *paragraph*, nikaona huyu hajui situ, *paragraph* haiwezi kuwa aya hata siku moja. Lakini aya humu kwenye vitabu vyetu vya Kiswahili mimi bado nitakuwa mbishi tu, tusitumie neno 'aya'.

Sasa kuna shehe mmoja nilimuuliza nini tafsiri ya aya? Aya kwenye Qurani ni kitu kilichokamilika, sasa leo nambieni kwenye sheria zetu zinakamilika? Hazikamiliki ndio maana yake tafsiri ya aya. Sasa wanasheria hebu nambieni siku zote sheria inakuwa haikamiliki, tuziangalie vizuri hizi sheria wanasheria wenzangu sio tupende kuitumia tu.

Mimi hiki kitu aya nakataa kabisa sikubaliani nacho, na nitakuwa mkaidi sana hili neno kama halikuondoka nitakuwa sipitishi, nitakuwa mgumu sana. Si kitu cha masihara kuna mambo mengine tusichezee chezee kwa sababu hatukiendeshi vizuri, hatukikamilishi ndio maana yake aya hii sasa kwa mashehe watanambia kama kweli watasema sawa unaendelea kijana mzuri, lakini hii aya lazima iondoke kwa nini tusitumie neno la kifungu. Kuongeza kifungu kipya cha *T* mabano sawa sawa, kimekaa vizuri tu, lakini tutumie kitu aya. *Wallahi* nataka niiseme tena aya lakini na mwili unanisisimka kwa sababu tunaitafsiri vibaya sana, aya hii mimi sikubaliani nayo tunamuomba Mhe. Waziri aiondoe aya itatupeleka pabaya.

Mhe. Mwenyekiti, twende katika kifungu cha kumtafuta Mwenyekiti. Ni kweli Mhe.Mwenyekiti wa Kamati alisema kuwa sifa nyengine zimekosekana, moja aliitaja kuwa lazima awe Mzanzibari hilo mimi naunga mkono ndio haki yake hii na haya ndio matunda yenyewe ale humu tunaanza hapa, lakini haikuoneshwa humu.

Pili, hapakuoneshwa kama ana shahada humu yeye kaambiwa awe na sifa tu, anaambiwa kuwa awe na utaalamu wa kipekee katika fani iliyofanana na utalii wa uongozi, lakini hakuna kama shahada au kitu gani hakuoneshwa huyu mtu, sifa yake hiyo moja awe na shahada fulani hamna humu. Sasa naona hapa tutampotosha kabisa huyu Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba na hiki nacho kiongezwe, awe Mzanzibari aliyetajwa ndani ya Katiba kifungu Nam. 5 halafu isitoshe, sifa nayo iainishwe, tunakwenda na wakati sasa hivi hatutaki sifa za karatasini tu. Ni lazima tuoneshwe, sasa hapa nimesema kuwa hilo moja liongezwe.

Sasa niende katika ukurasa wa 43. Mhe.Mwenyekiti, nimeshituka sana kusikia huyu mtu atakuwa na mshahara, mafao, na nini, naona wenyeviti wako wengi hatujaona mambo haya. Mhe. Mwenyekiti, walikuweko wenyeviti wengi sana hata Mhe. Ali Mzee Ali alikuwa Mwenyekiti wa Bodi, lakini sikusikia kupata mafao kama haya, hayakuwepo kabisa. Sasa hebu tuangalie jamani hizo fedha za walipa kodi, saa nyengine hebu tuzionee huruma, tuzikasimu, tuzipunguze kwa maslahi mengine ili kuweza kuwasaidia hawa walipa kodi wetu wanaochangia.

Kwa sababu kuna mambo mengi sana yanakuwa yanapungukiwa kupatikana, kwa sababu kumbe tunaongeza mambo mengi kabisa, sasa hatari yake ndio kama hiyo. Mimi hilo bado sijakubaliana nalo, hili naomba kabisa tumpe hayo hayo mafao na siku ya kuondoka ile, basi *minalfaidhina* tunaagana naye, tunamwambia haya karibu sana mwenyekiti tutakuja kuonana. Mimi nafikiria hicho kitu tuangalie sana.

Lakini ukurasa wa 45 Katibu anaoneshwa hapa awe angalau ana shahada, hapa kuna 'wa' sijui inakuwaje tafsiri hii, awe na angalau shahada wa, wa kwanza au ya kwanza? Na hii naomba tusahihishe hapa tuangalie au nije nitafsiriwe vizuri kwa sababu pengine sikuvaa miwani sikuiona vizuri. Imesema wa kwanza au elimu inayolingana, sasa hapa tutaangalia. Huku Katibu ameoneshwa hivyo, lakini kule Mwenyekiti hakupewa vile, jamani tusije tukaokota tu watu ovyo ndio wasiwasi wangu mimi ulipo hapo, basi kama tunaona tabu tungesema japo cheti, huku kuna shahada huku kuna cheti ingekuwa afadhali, lakini kuja kuokota mtu tu kwa ubinafsi au kumpenda mtu, hatari yake itatukuta huko mbele ya safari.

Nikiingia ukurasa wa 46 kuna hawa wadau, nani wadau? Hebu naomba Mhe. Waziri ukija unifafanulie vizuri kwa sababu lugha hii ina mambo mengi, ina upana wa kutafsiriwa nani wadau? Mhe. Waziri naomba uje kuniambia nani mdau ili nipate kufahamiana na wewe vizuri.

Lakini pia imesemwa kuwa kutakuwa na kamati za utalii za wilaya, na hapa tunaambiwa mwenyekiti au wenyeviti wa masheha, hawa wenyeviti wa masheha ni nani? Mimi siwajui mpaka sasa hivi, sisi tunaowajua kule kwenye shehia zetu kuna sheha na katibu wake, au huyu tunamtafisiri ndiye atayekuwa mwenyekiti au wenyeviti, hebu tuiangalie vizuri hii lugha hapa kidogo. Ukiniambia wenyeviti masheha bado mimi naitafuta, nimeangalia kwenye *dictionary* sijaipata mimi hii, sasa sijui mwenzangu kaipata papi? Mhe. Waziri ningeomba uje kunisaidia kunifahamisha hapa. Kwa sababu kule kwetu sisi tuna masheha hatuna wenyeviti, hili ningeomba nalo anisaidie.

Hapa pameelezwa Mhe. Mwenyekiti, mlolongo mkubwa hao wajumbe wenyewe ambao watakaounda mimi ningependekeza basi angalau na Wawakilishi wawemo. Miongoni mwa Wawakilishi watasaidia kwa mfano, si lazima unambie mimi, mimi nakupa mfano tu, ni mkereketwa mkubwa sana wa utalii katika jimbo langu na ninao utalii huo, lakini sasa ukininyima fursa hii hutonitendea haki.

Kwa sababu mimi hiyo jamii ndio ninayo miongoni mwao mle katika wilaya yangu. Mimi nafikiria ungefanya hicho kitu ambacho kitakuwa na msingi kabisa, ili wawakilishi na wabunge na wabunge wawemo katika hao wajumbe, ili kazi yako iende vizuri sana. Mhe. Waziri liangalie hilo katika marekebisho yako utapokuja basi na hilo ulitizame ili kuweza kusaidiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nishuke chini katika kifungu cha 23(b) kinachozungumzia kulinda usalama na amani na wageni jamii katika maeneo ya utalii. Mhe. Mwenyekiti, sasa hapa katika marekebisho yako basi utakapokuja na hili ulitazame ili kuweza kusaidia.
Mhe.Spika, nizungumzie kifungu cha 25 (b) kulinda usalama na amani kwa wageni ni jumla katika maeneo ya utalii.Mhe.Spika, sasa hapa tunaanza kumtafuta Mzanzibari vile vile. Mhe.Spika, nakubaliana na Mhe.Waziri hawa ndio watakaokuwa walinzi lakini tusidanganyane kama hukuwaondoa makampuni ya kina KK, sijui kina nani hawa si kweli hutokuwa na usalama huo katika utalii wako.Sasa ndio haki ya Mzanzibari unapotakiwa umpatie hapa.

M Mhe. Mwenyekiti, tuna makampuni yetu sasa hivi hapa hawa askari wastaafu hawapati haki hapa ya Kizanzibari ya kulinda nchi yao, wanapostaafu wanajiunga vizuri, tunawashajihisha vizuri lakini tunawatelekeza.Mhe.Spika, utaunda hata kamati 50 hapa kama hukuwaondoa hawa usijidanganye, na ndio maana nikasema kuwa mapungufu ya haya yanakuja hapa. Leo watu wanaiba tu kuna hoteli ya *Residence* kule Kizimkazi imeibiwa lakini pakiibiwa wanaonekana Wazanzibari wezi. Mhe.Spika, tunapoteza sifa zetu, tumepewa nishani ya utalii hivi juzi tu, lakini kwa makusudi itakuwa inapotea hiyo kwa kuwaweka hawa wizi mtupu. Lakini Mhe.Waziri ukitaka kulinda usalama wako kwa watu hawa basi nakuomba sana waweke hawa, ukishawaweka hawa hakuna tatizo lolote. Ndio nikasema kuwa kuna haki nyengine za Kizanzibari tunawanyima kwa kweli kusema hatuwapatii haki za Kizanzibari kama vile inavyotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, tunaelewa kuwa sote sasa hivi Zanzibar tuna hoteli nyingi sana na hoteli hizo zinategemea kupata ajira wananchi wetu wa Kizanzibari kwa kuuondoa umaskini. Lakini Mhe. Spika, tukienda katika ukurasa wa 49, nakubaliana na Mhe. Waziri kuwa hii "Kuimarisha ufahamu wa wananchi wa kuwa kama dhana ya utalii kwa

wote." Hili sina pingamizi nalo, na naamini kuwa sasa ndio lengo lako unataka tuelekee huko. Lakini je, hii itakuwa ni kweli, tutatazama huko tunakokwenda katika hiku kuchangia kwangu, tutajua kama kweli au uongo.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 23 (3) naomba kunukuu "Mtu yeyote anayefanya biashara ya utalii aliyeajiriwa, mtu ambaye sio Mtanzania kutoa huduma iliyoelezwa chini ya kifungu cha ..." Basi na hii tungeendelea hivyo hivyo kifungu cha… kuliko kutumia aya *a* haiwezekani.

Kifungu 23 (1) lazima apate ruhusa ya maandishi kutoka kwa waziri, baada ya kumthibitisha waziri kuwa hakuna mtu wa ndani wa kujaza nafasi hiyo.Sasa hapa ndio kunako mchezo nafungua vitu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kuna mambo ya kusikitisha, mimi ningesema hivi nikubaliane na kifungu hichi, halafu nisikubali kifungu hichi, kwa sababu kuna makosa tayari huko nyuma yameshafanywa sana tu.Sasa sijui wakati ule waziri alikuwa hayupo ndio sasa tunamtafuta waziri awepo. Mhe.Mwenyekiti, tunadanganywa sana na wenzetu wa nje hususan Kenya, Congo tumeshadanganywa sana, tena sana nasikitika sana. Wenyewe wale waimbaji husema "inauma sana" tena inauma.

Mhe. Mwenyekiti, nina *document* ambazo za uhakika, mimi siku zote nasema sisemi kwa kubahatisha wala simuogopi mtu, katiba inanilinda hapa na hakuna mamlaka nyengine itakayoniingilia isipokuwa kama kwa kadri mtamaliza wataalamu. Ninayo haki hiyo kwenye mamlaka yangu ni hapa kwenye *red carpet* niyaseme maneno niliyokuwa nayaona, na nikisema neno husema vitu vya ushahidi tosha.

Sasa tena huyu mwengine atakayeniita huko nje kusema kuna idara nyengine itatokezea katiba hii hapa, afungue katiba sio aniite tena mimi nasemea hapa, akifika nje mdomo kwii nimenyamaza, kwa sababu nje sina sheria lakini hapa nina sheria, ninayo hii hapa katiba iko kwapani ndio inayoniongoza inayonifanya mimi niseme. Sisemi vitu vya kubahatisha mimi.Sasa leo tunafika pahala pengine, waziri kama huko nyuma alikuwepo au hayupo, ndio sasa hivi tunamtengenezea hali halisi tumeshapigwa bao.

Mhe.Mwenyekiti, wenzetu Wakenya wanadanganya vyeti wanakuwa na *side* mbili, anajua Wazanzibari asilimia kubwa ni Wazanzibari, lakini ana upande mwengine tunakwenda kule kule kwenye dini yetu nyengine ya Kikristo. Mhe.Mwenyekiti, hatari sana tuliyokuwanayo, sasa niseme sijui tunakuwa hatuoni au basi tu ndio tumeshakaa kwenye kiti, tunaona utamu wa madaraka tu tunajisahau *afanalek*.

Mhe.Mwenyekiti, mimi nasema siku zote Mhe.Makamo wa Pili wa Rais naomba unisikilize, sio jambo la kujaribu lakini kama ungekuwa unajaribu nimekwambia hebu fanya zoezi siku moja tu, halafu utasema kama *yes* huyu jamaa kumbe akisema jambo la hakika. Tuna uzito wa ufuatiliaji, tatizo letu ufuatiliaji unakuwa ni mgumu sana.

Mhe.Mwenyekiti, kuna jamaa hapa amesema kama yeye ni Mzanzibari amepewa shahada ya ID No. 520028885 wakati ni mtu wa Kenya. He, jamani, sasa mimi nauliza hizi anazipata vipi, amechukua nafasi za kutembeza wageni na shahada kapewa katika ofisi yetu ya Kamisheni ya Utalii, sijui huyu kenda kadanganya vipi pale hata akapewa hii. Katika sheria hii Mzanzibari aoneshe cheti cha kuzaliwa, aoneshe ID yake, aoneshe amesoma pale Maruhubi ndio sheria inavyosema. Sheria hii inasema imekubalishwa kabisa, lakini leo huyu amepewa, ndio kazi aliyoletewa hapa huyu, ndio hivi sasa kuwa kweli hatuna uwezo huo kifungu hichi.

Sasa kifungu hichi kina tafsiri namna nyingi, kila mtu ana tafsiri yake anavyoona, mimi tafsiri yangu ninavyoona hiyo. Kwa hivyo, Wazanzibari bado tuna uwezo sisi hatuna haja ya kuletewa mtu mwengine, ndio maana waziri hichi kifungu apunguziwe makali, ndio ninachosema mimi hapa hatari yake huwa kama hii. Mhe.Mwenyekiti, huyu mtu mpaka sasa hivi anatembea Zanzibar hii keshafanya udanganyifu wa hali ya juu.

Mhe.Mwenyekiti, siku moja nilisikia hotuba ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alisema, kuna mtu mmoja wa kabila la Kihindi alisema kuwa serikali ya Mwalimu Nyerere nimeiweka hapa kwenye kiganja, mwalimu alishtuka sana na alimtia ndani siku hiyo hiyo.Hao watasema hivyo hivyo Serikali ya Mapinduzi iko kwenye kiganja hapa, tunalolitaka tutalipata ndio maana yake. Mzanzibari anashindwa kupata ID, leo huyu anapata ID kwa nini. Amechukua kazi zetu za Kizanzibari, imesema ndani ya katiba sikusema mimi kama ni Mshimba, nasema jamani nilikuwa natafuta nani Mzanzibari na Mzanzibari ana fursa gani ya kuweza kupata, ndio hizi fursa zenyewe lakini Mzanzibari hapati.

Mhe.Mwenyekiti, naendelea na nyengine kuna watu wengine wamepewa *permit* ya kukaa hapa, ati kwa ukulima anatoka Congo.Mzanzibari gani asiyejua kulima hapa, hii hapa kama nasema uongo, si vitu vya kubahatisha. Mhe.Makamo wa Pili wa Rais ona vitu hivyo, *still going strong* yuko hapa kaletwa kwa kulima ni kitu cha kushangaza kweli. Kikwajuni kuna shamba la kulima hii hapa kama nasema uongo nendeni.Leo yuko karafuu, karafuu kuna kulima kweli, sijui Mhe.Waziri unazo karafuu za kulima labda mpeleke.

Mhe.Mwenyekiti, pia huyu kapewa ID ya Mzanzibari inasema hivi Nam. 281135119, Mzanzibari wa Makunduchi hana ID anahangaika kila leo hajapewa hajakamilisha. Wananchi wangu wa Jimbo la Kitope mpaka leo ID hawajapata, huyu leo kapata ID tunakwenda wapi jamani, Mzanzibari ananyimwa haki yake.Raha ya Serikali ya Kitaifa ndio hii unaruhusika useme unavyotaka. Tena Mhe. Mwenyekiti, naipenda sana Serikali ya Kitaifa *wallahi laadhim,* ninavyokwambia kutokujua tu na kutokwenda kwenyewe, lakini ukishajua unajua kwenda sana tu.

Mwengine halikadhalika hawa watu chungu nzima ninao hapa sitaki kuwataja wote wana ID hawa, na wote Wakenya na wanafanya kazi kwenye hoteli mbalimbali. Wenyewe tumelala Wazanzibari hapa tunaibiwa hivi hivi, sasa mimi nashangaa sijui wanapata *permit* vipi kwenye wizara yako Mhe. Haroun Ali Suleiman, wanapewa *permit* hawa za kuishi hapa Zanzibar. Wazanzibari sasa wamechoka wanataka haki zao na mswada huu mliouleta maana yake hiyo.

Mhe.Mwenyekiti, nitakwambia jambo la kusikitisha, juzi tu katika hoteli ya *Residence* kule Kizimkazi, Mzanzibari amedhalilishwa na mtu huyo aliyemdhalilisha mpaka leo hajakamatwa tunakwenda wapi. Jamani naomba Mhe.Mwenyekiti, nikisema kitu sikusudii matusi, kitu chake cha ndani kimechukuliwa kimeoneshwa hivi, na Mkenya anakitangaza kinapigwa picha. Ndio maana ya kuwapeleka watu kampuni za nje kuja kuwadhalilisha ndugu zetu wa Kizanzibari. Aibu, leo anaambiwa alipwe shilingi milioni tatu, milioni tatu kumdhalilisha utu wake, kitu cha ndani ni kitu cha siri, mbona sisi hatukivui tukakionesha si kwa kuwa ni siri, lakini kimetembezwa hivi hakuna asiyejua, nani hapa aliyechukua *action* hiyo. Mimi naomba hapa waziri gani aliyekwenda kuchukua *action* hiyo, lakini tukienda kwa Rais na bango kitita tunakwenda kumdanganya hatutembei.

Mhe.Mwenyekiti, mimi nitakuwa mkali sana tena mimi nimeshajitolea vibaya vibaya. Mhe.Mwenyekiti, mimi kama nitarejeshwa sawa kama sikurejeshwa Mwenyezi Mungu ataniweka pahala pengine popote, lakini ukweli nitausema kwenye dunia hii.Aibu, leo Mzanzibari anakwenda kuvuliwa ndubwana ya ndani inakwenda kupigwa picha, inatembezwa halafu yule mtu hakamatwi ni mtu wa nje.

Hebu nenda nchi za nje, mimi siku moja nilikwenda Dubai nikenda dukani ikatokea *mistake* tu nikaja nikamgusa mama mmoja kidogo tu, kama hivi niliharisha debe tano alikwenda kunishtaki anasema nimemgusa. Hata baada ya saa moja nilipotolewa kule ndani nilikuwa taabani nimeshakonda si mchezo, tazama wenzetu walivyokuwa nchi yao hawataki masihara, *mistake* tu na *walking* hivi kwenye maduka basi niliparaza kidogo tu hivi, tena hapa tu wala sikuparaza huku.

Leo anachukuliwa Mzanzibari anatembezwa tunacheka kabisa, watu wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika wapo, watu wa Kamisheni ya Utalii wapo, lakini sijui mpaka leo hatua gani mtu huyo amechukuliwa. Isipokuwa wanamzunguka wale wenyewe wanasema kuwa wanamghilibu yule mtoto kukubali alipwe shilingi milioni tatu, shilingi milioni tatu kwa kukashifiwa huku.

Mhe.Mwenyekiti, ndio maana ninaposema kifungu hichi kinanipa mashaka makubwa sana, bora tuseme moja kwa moja kuwa Wazanzibari wapo wenye kukamata sasa hivi. Chuo cha Utalii Maruhubi kinatoa mambo mazuri sana hatutaki tena watu wa nje, *expert* anakuja kusimamia kukosha madishi. Tunasema kifungu hichi moja kwa moja kioneshe kuwa Mzanzibari apewe fursa hii ya moja kwa moja.

Mhe.Mwenyekiti, kwa kumalizia naomba sana vitengo husika, Wazanzibari wameshasema wamechoka na kadhia hii sasa wanataka nafasi zao, ili waondoe ukali wa maisha. Kwa sababu tuna ukali wa maisha, umaskini umetuvaa wakati utajiri tunao ndio huu Mhe. Abdillah Jihad Hassan hapa anautengeneza, kaona hili na mwenyewe ni mstari wa mbele huyu katika kufuatilia mambo anajua wazi. Mhe.Mwenyekiti, naomba sheria ichukue mkondo wake tusiwaone hawa mara moja kwa mujibu wa sheria.

Mhe.Mwenyekiti, mimi naunga mkono mswada huu na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope wananisikia nawatetea haki zao za hotelini warejeshewe wenyewe.Ahsante sana.

Mhe.Asaa Othman Hamad: Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye nguvu nikushukuru na wewe Mhe.Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kusema machache ndani ya sheria hii ya marekebisho.

Mhe.Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Wizara husika, kwa hiyo nitakuwa na machache ya kusaidiana tu na Waheshimiwa Wajumbe ili dhana iliyokusudiwa na Mhe. Waziri na watendaji wake iweze kufikiwa.

Mhe.Mwenyekiti, utalii ndani ya nchi ya Zanzibar sasa hivi ni tegemeo kubwa, na karibuni tu tuliipa nafasi ya kipaumbele cha kwanza cha kuingiza mapato ya nchi.Sasa hivi tunataka kurekebisha sheria ya muundo uliopo sasa, ili uwe bora zaidi kwa uzuri.

Mhe.Mwenyekiti, dhana hii ningeomba sana wizara kwa ujumla wake, serikali na wadau wa sekta hii kwamba, sasa tubadilike ili twende sambamba na mabadiliko ya sheria. Haitokuwa vyema hata kidogo kubadilisha sheria lakini mazingira yaliyoizunguka sheria ni yale yale.Sidhani kama tutakuwa tunakwenda, ni ile sifa tuliyonayo kwamba ni mahodari sana wa sheria, kutunga sheria Zanzibar *Alhamdullilah*, utekelezaji wa sheria zenyewe ndio tatizo. Sasa tubadilike ulimwengu ni wa *digital analogue* basi na inaambiwa ikifika mwezi Disemba mwaka huu tunatiririka miezi inakatika, tukibaki tu tunavyokuwa na *analogue* yetu *digital* tutasikia hadithi.

Mhe.Mwenyekiti, nilichokusudia kusema kwanza ningewaomba sana watendaji wa taasisi hii, na wadau kwa ujumla, na sisi waheshimiwa, tuelekeeni kwenye *digital* sasa ya kitalii, na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe.Mwenyekiti, madhumuni ya mswada wa sheria kwa ruhusa yako ni kutunga sheria ya marekebisho ya Sheria ya Utalii Nam. 6 ya 2009, ambayo inarekebishwa kwa kufuta muundo wa uongozi uliopo sasa wa kamisheni na kuanzisha muundo mpya. Kamisheni ipo, lakini wenzetu wamehisi kwamba haifanyi vizuri zaidi, na tunataka ifanye vizuri zaidi. Wameleta sheria hii ni jambo jema.

Mhe.Mwenyekiti, marekebisho yako kwenye vifungu mwanasheria mdogo amezungumzia, na sisi wengine tutataja taja na Waheshimiwa Wajumbe wako watajimwaga, alimradi tufike mahali palipokusudiwa na sheria.

Mhe.Mwenyekiti, nimesema tubadilike au tubadilishe na mazingira yetu, tukivutana na mazingira na sheria hatutofika. Bado mimi ninapotoa mfano huu mtalii tunayemtaka Zanzibar kwa lengo la kuongeza kipato cha nchi hii, si tu hawa wanaobeba mikoba yao mabegani, tunataka mtalii yule *five star, six* kwenda huko, anaweka *perfume* kwenye chumba wiki moja hakuhitajiki *perfume* tena, si hawa watalii akija akivua soksi ni mtihani.

Sasa kama hatukubadilika, maana yake tutaendelea kupokea watalii hao niliowasema akivua soksi hupiti mbele yake. Lakini tutampataje mtalii mwenye *perfume* ile ya wiki moja chumbani bila ya kurudia, ni kubadilika mazingira tuliyonayo sasa, si tu kubadilisha sheria.

Mhe.Mwenyekiti, tunataka tuwawezeshe watalii kwenda kuona *beach* za Vumawimbi na hoteli zilioko huko, barabara yetu imemalizikia hapa Kiuyu kwa Manda kwa Mhe.Suleiman Hemed Khamis. Mhe.Suleiman hutaka angalau aifanye barabara ile pale msituni papitike vizuri zaidi angalau kwa fusi ndio uwezo wake yeye. Amezungumza huko na Mhe.Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano wamekubaliana hilo, lakini watu wa misitu hawataki hivyo wanasema miti yao itaharibika, sijui itakufa. Sasa huwezi kujenga bila ya kuvunja tukubali, labda ni miti mingapi tutaathirika ikikatwa au itaambukizwa ugonjwa wa vumbi la fusi au lami. Wataalamu watwambie hiyo tutakosa kiasi gani na tutapata kiasi gain, endapo patapitishwa lami pale maana mwengine tunaona mambo sio hivyo tunavyoambiwa. Ndio hii hii ninachosema kwamba, hebu tujenge mazingira kwanza ya kupokea utalii halafu iende sambamba na hizi sheria.

Mhe.Mwenyekiti, mila, tamaduni, silka za Kizanzibari nashukuru sana Mhe.Waziri kuiona hii, kwamba sasa tutakuwa na kamati za kiwilaya. Ni jambo jema sana kwa sababu tumejifunza kutokana na makosa. Tunayaona hakuna haja ya kurudia, lakini sasa kama ni lawama wilaya yenyewe itabidi ijilaumu kukaribisha utalii kwa kuharibu mila zetu, desturi zetu na mengine yanayofanana na hayo. Lakini Mhe.Mwenyekiti, kwenye mabadiliko kulikuwa na hii bodi inayoondolewa sasa, kwenye bodi tulikosa nini na kwenye kamisheni sasa tunatarajia nini.Mhe.Mwenyekiti, labda Mhe.Waziri atatusaidia wajumbe wako atakapokuja kuhitimisha. Maana tumefundishwa, na karibuni tulikuwa na mtaalamu na bahati nzuri Baraza hili lina wataalamu wazuri wa sheria,

lakini na juzi tukapata mwenzetu. Sheria iwe ni ile ambayo inatekelezeka na pia ieleweke kwa wale walengwa. Sasa tunataka kupitisha hii sheria ya marekebisho lakini tuelewe tulikuwa vipi, na tunatarajia kipi kwa kufanya hivi.

Mhe.Mwenyekiti, labda nianze kwenye Muundo wa Kamisheni hapa ametajwa Mwenyekiti naomba kunukuu "Mwenyekiti atakuwa Mkuu wa Kamisheni kwa muda wote, na ambaye atateuliwa na Rais." Sina tatizo na hilo. Pia kamisheni itakuwa na makamishna wametajwa watapatikana vipi. Lakini kifungu cha 5(6), mjumbe mwengine yeyote ambaye atakuwa ni mwanamke. Mhe. Mwenyekiti, hawa ni makamishna wa utalii ambapo kazi zao huku mbali zimetajwa sifa. Mimi sisemi kuwa ni mwanamke hata kidogo, ninachosema ni lile neno 'yeyote' tu, hakutajwa na sifa hata moja, atawezaje kwenda kuyatekeleza majukumu hayo, kama neno 'yeyote' linavyosomeka hapa, hii ni kamisheni ya utalii, makamishna hawa nadhani wangekuwa na sifa zinazolenga kwenye hizo shughuli za kitalii.

Kifungu hicho hicho kidogo cha (3) hatoweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati tulipendekeza nadhani Mhe. Waziri atakubaliana na sisi. Lakini kifungu kidogo cha 3(2) kinasema, pia awe na ujuzi wa kutosha wa kupigania mambo, kupigania mambo, mimi najiuliza mambo gani. Hii sheria Mhe. Mwenyekiti, haitakiwi kubanwa, sheria lazima iwe wazi ili tuelewe. Ni hii lugha tu tunayosikia ya vijana huku au imekusudiwa nini, hebu Mhe. Waziri uje utuweke sawa, tusikuidhinishie kitu hatimaye tukaja kulia machozi. Mambo tusiyoyafahamu hatutokuwa tayari kuyaidhinisha, yataje tuyajuwe.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 6 ni kuhusu hizo kazi za Mwenyekiti. Kushauri na kuchukua hatua za kuanzisha mikakati kwa lengo, nadhani kulikuwa kuwe na neno hapo, la kuwashajihisha wananchi katika kujihusisha na biashara ya utalii ili waweze kujipatia manufaa kutokana na utalii.

Mhe. Mwenyekiti, kushajihisha wananchi bado wananchi wameshajihika, tumeona dhana ya utalii walivyoipokea. Lakini kwa kutokuwa na uelewa wa dhana halisi, hivyo hasara tuliyoiona tumeiona, hata usumbufu katika maeneo yao wanayoishi. Sasa kushajihisha tu wananchi itakuwa bado, kwa hatua tuliyofika nadhani sasa tushajihishe na vyombo vya fedha viweze kutoa mikopo nafuu kwa wananchi, tusikaribishe tu wageni katika suala la kuekeza. Utalii kwa wote maana yake ni wote, kila mmoja kwa namna yake aweze kufaidika na dhana hiyo. Sasa duniani kote hatuwezi kwenda hivi ni lazima mikopo iwepo ya bei nafuu, taasisi za fedha zikubali hilo, watoe fedha ili wananchi waweze kuekeza kwenye sekta ya utalii. Mwengine ataingia kwenye kilimo ndio kwa wote, mwengine kwenye uvuvi, mwengine mifugo na mwengine usafiri wa ndani. Kwa hivyo, bila ya kumpa fedha huyu mwananchi basi atashuhudia tu utalii na hata ukimuuliza haelewi chochote labda zile hasara ndizo atakazozifahamu yeye, lakini tija ya utalii ni kama hivi sasa haupo.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 6(2) kinasema, ili kuondoa shaka inaelezwa wazi wazi kwamba Mwenyekiti hatofanyakazi za kiutawala, za kamisheni ambazo kazi hizo zimewekwa chini ya mamlaka ya Katibu Mtendaji. Mimi pia nimepata mashaka kidogo, Mwenyekiti huyu mbona anatajwa mishahara na mafao. Kuna tofauti zipi wenyeviti tuliowazowea na huyu na yeye si mtendaji katajwa humu, lakini baada ya muda wake wa kazi utumishi watamshughulikia kwa mafao na mambo mengine na kama atachaguliwa tena basi mambo yatakua ni hivyo hivyo. Hebu Mhe. Waziri utakapokuja tusaidie, kulikoni, mabadiliko haya ya sheria yaliyompa nafasi hii.

Mhe. Mwenyekiti Serikali kwa ujumla wake naomba sana ijipange ili kuhakikisha kwamba utalii unamfaidisha mwananchi wa nchi hii ya Zanzibar mahali popote pale alipo. Maana yangu ni kwamba yule ambaye hawezi kufanya shughuli zozote kati ya nilizozitaja na nisizozitaja, lakini kwa sababu yuko Matemwe, ardhi ya Matemwe imetumika kujengwa hoteli na mwekezaji, inapatikana faida na yeye afaidike kwa namna moja au nyengine. Kama Mhe. Waziri hilo halipo basi naomba ukae sana na watendaji, sasa tunataka kama mwananchi yuko kitandani ni mgonjwa, basi utalii na yeye umfike pale kimaslahi huu ndio utalii kwa wote. Zanzibar ni ya Wazanzibari, kilichomo humu ni lazima tugawane sote na kitakachopatikana basi twende hivyo hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 10, kuongezwa kwa kifungu kipya cha 9(a) malipo ya makamishna hayo. Mahali pamoja tu nambari 9(a) makamishna watalipwa mafao kama Waziri atakavyoamua. Mhe. Waziri Abdilla Jihadi ni mtu mwema ni Alhaj na yeye mwenyewe ni mcha Mungu awatizame vizuri. Mhe. Mwanasheria atakapostaafu hapa Mhe. Mshimba anasema hapana nitakwenda kwa mujibu wa sheria. Naona hapa Mhe. Waziri tumempa nafasi ama akiwa kama nilivyotaja mwanzo makamishna akhuweni, lakini pengine watu wa sheria wanakaa kwenye sheria, hakuna lugha nyengine. Mimi nadhani tungekwenda na utumishi. Sheria za utumishi zinasemaje, tumezitunga, tumezipitisha na Mhe. Rais kasaini nadhani turudi kwenye sheria za utumishi. Tusimwachie Mhe. Waziri atakavyoona, hapana hii mambo ya kuona tena iwe basi.

Mhe. Mwenyekiti nataka nifike mwisho kwa haraka haraka kuna Katibu Mtendaji, ndiye huyu atakayekamata nafasi sasa baada ya mabadiliko. Kutakua na Katibu Mtendaji ambaye atakua ni afisa mtendaji mkuu wa kamisheni atakayeteuliwa na Mhe. Rais. Mhe. Mwenyekiti, mimi bado nina shawishika Mhe. Rais ni kiongozi wa nchi. Mhe. Mwenyekiti, shughuli kama hizi na nafasi kama hizi kwa nini tusizitangaze, tutangaze.

Mhe. Spika, hapa anaambiwa huyu afisa tunayemtaka hatofaa kuteuliwa kua Katibu Mtendaji mpaka awe na sifa zifuatazo, angalau shahada ya kwanza au elimu iliyolingana na hiyo na uzoefu na mambo kama hayo. Mhe. Spika, sijui kama Kiswahili nitakua niko sahihi, angalau basi shahada ya kwanza, siku hizi tunataka shahada ya pili na tungewapata vizuri kwa sababu tuna Wazanzibari Mhe. Mwenyekiti, wamesambaa Afrika na nje ya Bara la Afrika, fursa hizi ni zao, tutakapokua tunazitangaza watasikia huko ulimwenguni, alipo popote kule ataona na ataweza na yeye kuona akiwa popote, matokeo yake tunatumia neno angalau, kwa sababu tutatizamana sisi tuliopo hapa tutakutana Darajani. Sio chengine tunatumia neno angalau tunataka utalii wa leo, uzoefu umeshatutia angalau, basi lakini tutakapotangaza sifa zile hakuzitimiza hatuna lawama, aliyezitimiza ndiye ambaye tunamchagua.

Mhe. Mwenyekiti, nakuona lakini naomba sana nimalize malize kwa kusema machache sana. Kamati nimeshazipongeza sana, kwa hivyo naamini zitafanya kazi nzuri sana kufuatana na yale ambayo nimeyatanguliza. Lakini naomba wenzangu watendaji, watendaji wa taasisi hii, wananchi wa Zanzibar wamejenga imani sana na Mhe. Rais Shein, uongozi wake bado wanauhitaji. Mhe. Shein ni Rais wa kwanza Mzanzibari aliyepewa jukumu la kuiongoza Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Tunataka Rais aweke kumbukumbu nzuri ya dunia. Kama vile dunia inavyotushangaa kwa nini tumemudu kwa muda huu mfupi, sio jambo dogo. Sasa nani kamudu ni Mhe. Rais Shein, lakini Mhe. Rais Shein hatoweza kumudu katika hatua tunayoitaka kama hatukumpa msaada tena mkubwa tu, hebu kila mmoja aone kua ana wajibu wa kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kwa kupitia sisi Waheshimiwa Wawakilishi hapa ambao tumechaguliwa na wananchi na wananchi wamechagua mfumo huu kwa kura nyingi tu za kutosha. Heshima hii kapewa Mhe. Rais Shein. Watendaji wa Serikali hebu tupeni nafasi tafadhalini, tunawaombeni sana wananchi huko ambao hawako kwenye hizo meza na viti mnavyovikalia, basi mnawavuruga vichwa vyao kuona mambo hayendi vile ambavyo wao walitegemea, walitegemea kua ndani ya mfumo huu Wazanzibari sasa *Alhamdulillah* tunaelekea kule tunakokuhitaji.

Sasa tunaposikia nong'ono nong'ono zisizo na msingi hazitusaidii. Subiri muda ufike tukifika uchaguzi kila mmoja atakaa kwenye uwanja wake. Kwenye masuala ya utendaji tafadhalini tuwatumikieni wananchi waliotuchagua, nawaombeni sana. Suala la Waziri wanatoka wapi ni nani hayo hatutaki kuulizana.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tumejaza fomu na tukifika hapa ni Wazanzibari wote tena tumechujwa wananchi wakatuamini na wakatukubali. Kwa hivyo, umebahatika kua na Waziri pengine sio wa chama chako ulichonacho wewe. Hebu hamtuoni sisi tunavyokaa humu, sisi tumechanganywa, tunakwenda sote na wala hatujulikani huko nje na tunatoka nje tunakabiliwa nchi hii dhamana kubwa za kuongoza kwenye ghafla mbali mbali. Ni wapinzani kina Asaa Othman, lakini ni wapinzani wa itikadi sio wa maendeleo ya nchi hakuna hilo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais kaja kakaa na sisi katuachia milango wazi kwa lile ambalo itakua mtu linamkera na mimi sitosita kamwe nitakapogundua kua kuna mtu anatupeleka sivyo.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwanza kwa kunivumilia. Lakini kwa sababu ni wajibu basi naomba sana tukamilishe wajibu wetu, kuna siku tutaulizwa. Wale wenzetu ambao wana harufu ya haya niliyoyasema watakuja kutulaumu kwamba hatukuwaambia. Kwa hivyo, tunawaambia kwa wote hivi sasa. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Shawana Bukheti Hassan: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi jioni hii ya leo ili na mimi niweze kuchangia mswada huu wa marekebisho ya utalii ambao ndio mswada ulioko mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kumshukuru Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kutuwasilishia mswada huu ambao mategemeo yetu tunategemea kwamba kwa kua hali ya utalii wetu na shughuli zetu za utalii kwa jumla, kwa mswada huu ulioletwa tunategemea mambo yatakua mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kikao hiki kinachoendelea ndio mara yangu ya mwanzo kusimama, basi pia nichukue nafasi hii kutoa pole kwa ndugu yetu Marehemu Salum Amour Mtondoo aliyetutoka hivi karibuni. Pia niwape pole sana ndugu na jamaa zake ambao wamepata msiba huu mzito Mwenyezi Mungu awajaalie awape subira na yeye Mwenyezi Mungu amjaalie ampe malazi mema peponi, amin.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Mohammedraza kwa ushindi mkubwa alioupata na hatimaye kua leo ni Mwakilishi wa Jimbo la Uzini. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Dole nachukua nafasi hii kumpongeza na Mwenyezi Mungu amuezeshe kwa nafasi hii aliyomjaalia.

Mhe. Mwenyekiti, mswada ulioletwa mbele yetu ni mswada mzuri ambao tunasema sisi viongozi tuliomo humu na Wazanzibari wote kwa jumla tunategemea mswada huu utatufikisha pale tulipopategemea. Lakini nataka kusema Mhe. Mwenyekiti, kwamba kutengeneza sheria, kurekebisha sheria ni sehemu moja, lakini kufanikisha ile sheria yenyewe ni sehemu ya pili.

Mhe. Mwenyekiti, katika marekebisho haya ambayo Mhe. Waziri katuletea leo yanaonekana kua huwenda Mwenyezi Mungu akatujaalia zile kasoro ambazo aliziona kwa jumla katika Wizara hii au kamisheni hii, basi zitafanyiwa marekebisho ili sasa hivi upatikane ufanisi zaidi katika kamisheni hii.

Mhe. Mwenyekiti, wajumbe wengi waliozungumza, wamezungumza kwamba sheria kweli ni kitu kizuri, lakini uwajibikaji ni kitu kizuri zaidi. Sheria ambayo haifuatwi na haina uwajibikaji basi tutafanya sheria na kubadilisha masheria hapa kila siku. Leo tutaunda kamisheni hii tutaiona haifai tutabadilisha, kesho kamisheni hii haifai, sisi hapa itakua kazi yetu kuja badala ya kuendelea na mambo mengine basi tutakua katika kubadilisha makamisheni tu.

Suala kubwa Mhe. Mwenyekiti, ni uwajibikaji. Waheshimiwa Wajumbe wengi wamesema kwamba sasa hivi ni lazima tubadilike, ni kweli tubadilike. Kama tulikua na taratibu za kutufanya sisi utalii wetu usiweze kwenda, basi huu mtiririko ulioandaliwa humu, makamishna, wenyeviti na watendaji mbali mbali, basi sasa hivi iwe ni wakati wa kuwajibika ili utalii wetu uende vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, utalii wetu wa sasa hivi unaonekana una dosari nyingi. Lile lengo na azma ya nchi yetu kuona kua wananchi wetu wanafaidika na nchi yetu inafaidika pamoja na kua kuna mchango unaotoka kwenye sehemu ya utalii, lakini bado mapato tunayoyategemea hatuyapati kama tulivyoyatarajia.

Mhe. Mwenyekiti, suala moja ninalotaka kuzungumza ni kwamba watalii sasa hivi *Alhamdulillah* wanakuja kwa wingi. Kwa taarifa tulizopata hivi karibuni kila kukicha wanazidi kuongezeka na dalili tunaziona, kwa sababu dalili moja ni zile ndege zikimiminika kuja hapa, wageni wengi basi sisi tunafurahi na tunasema wageni wameingia na mapato yatapatikana katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo ambalo lipo kwenye utalii na hili Mhe. Waziri ningeomba hii kamisheni itakayoundwa sasa hivi basi waliangalie sana hilo na kulirekebisha. Watalii wengi wanaingia katika nchi yetu, inavyosemekana kua mambo yote yanayohusu wao kulipa hapa nchini basi wanalipa huko wanakotokea. Kuanzia vyumba, vyakula, mpaka chupa za maji, kila kitu wanalipa huko, wanakuja hapa hawana *single cent* ya kulipa katika huduma ambayo wanatakiwa walipe. Kinachofanyika ni nini Mhe. Mwenyekiti, utakuta sasa hapa nchini kuna ndugu zetu wanaochukua *tender* mbali mbali kwenye mahoteli, lakini wakienda kudai utakuta fedha zile za malipo hawazipati, tatizo ni nini. Tatizo fedha zimelipwa kule mpaka zitolewe huko zije hapa ndio walipwe, basi inafika miezi mitatu, minne hadi sita. Kwa hivyo, yule mpelekaji vyakula pale kama samaki, mayai na vitu vyengine vyote keshafilisika, hili ni tatizo. Kwa hivyo, tungewaomba wenzetu wawajibike vizuri kulisimamia hili, ili hawa watu wetu na wananchi wetu waweze kufaidika na utalii ambao tunautegemea.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile limezungumzwa suala la maadili, kweli maadili yetu kidogo yamepungua na ukiacha wenzetu hawa wanaokuja, mfano kutoka Tanzania Bara na maeneo mengine, lakini asilimia kubwa tunaowaona hapa ni wageni wetu wa kizungu. Mhe. Mwenyekiti, kivazi wanachokivaa kuranda barabarani wanavaa vile vibukta vifupi mpaka juu, haipendezi Mhe. Mwenyekiti. Kivazi hiki kwao hawavai wanatufanyia sisi tu hapa, kuna maeneo maalum ya kuvaa hizo nguo na maeneo maalum ya starehe zao na kila mahala pana nguo yake unavaa. Lakini humkuti mtu Darajani kavaa kibukta, lakini hapa kwetu wanatufanyia kusudi.

Unapita na mtu ambaye unamstahi barabarani basi hamuwezi kutizamana, inabidi ghafla mbadilishane njia kila mmoja apite njia yake. Kwa hivyo, huu sio utaratibu mzuri, uandaliwe utaratibu mzuri. Kwa sababu wanachosingizia kubwa au taarifa tunazozipata wanasema eti ni joto, hivi hakuna nguo ambazo zinaweza kuvaliwa wakati wa joto, mbona ziko hizi bahama na nyenginezo tunavaa.

Mhe. Mwenyekiti, nimemuona mzungu mmoja kavaa bahama, ndani kavaa bukta yake lakini juu kavaa bahama. Kwa nini hauandaliwi utaratibu huu wa kua akifika pale nguo aliyoivaa sio basi avae bahama ambayo haina joto, lakini wanatutembelea vibaya katika mji wetu sio vizuri, kamisheni suala hili waliangalie ili utaratibu uwepo.

Mhe. Mwenyekiti, nimesema tubadilike. Viongozi watakaopata bahati ya hii nafasi basi wabadilike kiutendaji. Kubadilika kiutendaji sio kusema kwa mdomo tu, wabadilike kiutendaji kwa kutoka kwenda kuona, kukaa tu na kusubiri taarifa zinaletwa na kungojea sijui miezi mitatu ile basi mnakaa pale, mambo mazuri yanakwenda ya vikao na mambo mengine, basi hii haitotusaidia. Wawajibike waende wakaone hali halisi ya kwenye mahoteli yetu. Wawajibike viongozi lakini pia katika utaratibu mzuri wakaangalie pia na utendaji.

Mhe. Mwenyekiti, kidogo hapa nataka nizungumze jambo katika utendaji wetu na sisi vijana wetu. Mhe. Mwenyekiti, ningeomba kamisheni hii isimamie pia masuala ya utendaji wa vijana wetu katika maeneo ya kazi. Hilo ndio lengo letu toka mwanzo tumeanzisha utalii vijana wetu wapate ajira. Lakini tunaona sisi wenyewe katika Wizara, Idara, na kwenye taasisi za binafsi basi ukenda utakuta malalamiko mengi. Mtu anataka ajira lakini kufanyakazi hataki. Kwa mfano, leo mama anaumwa na kweli tunazo dharura, kesho mama mdogo anaumwa, kesho kutwa shangazi wakati mwengine kuna harusi pamoja na mambo mengine.

Kwa hivyo, na hili hii Kamisheni basi nayo ikae na vijana wetu kwa ajili ya kuwaelekeza, kwa sababu kuna haki na wajibu, kwani kuajiriwa ni haki yetu, lakini wajibu wa kufanya zile kazi ambazo tumeajiriwa basi nazo tuzifanye na sio dharura za kila siku wenzetu tunawachosha na kuwatia hasara na ndipo wanapoamua maamuzi mengine. Kwa maana hiyo, tujikaze kidogo pamoja na kwamba tunazo dharura za hapa na pale, lakini kwa hili ni vyema kujitahidi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo niingie kwenye mswada. Kwa kweli kuna Kamisheni ambayo itakua na Mwenyekiti pamoja na watu wengine waliopendekezwa humu. Nadhani ni vyema kwanza kupongeza kwa hao wajumbe waliopendekezwa humu ambapo wengine wametajwa sifa zao, lakini wengine sifa zao hazikutajwa.

Sasa ninachokiomba Mhe. Mwenyekiti, kwa kua wale Makamishna 6 na wala sifa zao hazikutajwa, tukiachia Mwenyekiti, Katibu nadhani wametajwa sifa zao, lakini Makamishna hawakutajwa sifa zao. Je, wao hawahitaji sifa maalum?

Mhe. Mwenyekiti, kwenye mtiririko huo mwisho, yaani mkiani imeelezwa na mwanamke yeyote yule mmoja aa! Mhe. Mwenyekiti, hapa naona Mhe. Waziri angetumia busara katika hawa Makamishna 6, basi angaula watatu wawe wanawake na watatu wanaume, kama si hivyo angalau kati ya 6, basi wawili wawe wanawake na halafu tena na huyo mmoja yeyote atakayehisi anafaa basi awekwe, hata mimi mkiniteua wala sikatai. *(Makofi)*

Suala jengine ni kuhusu wadau kuwashirikisha. Mhe. Mwenyekiti, nataka kupongeza sana suala hili, kwa sababu tutakapowashirikisha wadau wanaohusu masuala ya utalii, basi hapa ndipo tutakapopata shida, matatizo na vipi tufanye ili tuendelee na wapi tumeharibikiwa tuweze kutengeneza.

Mhe. Mwenyekiti, tunao watu mbali mbali kama vile watu wa *Private Hire*, wanaopokea wageni pamoja na wamiliki wa mahoteli wenyewe, yaani tunao watu wa fani mbali mbali.

Kwa hivyo, suala hili nalipongeza sana kwa sababu ni jambo zuri litatusaidia na hata zile kasoro zinazotokea kwenye maeneo haya niliyoyataja basi zitatusaidia. Kwa kweli hasa niliyokusudia ni yale manung'uniko, kwa sababu huwa kuna manung'uniko mengi ambayo yanatokea kwa hawa ambao niliowataja, kwa hivyo nazo zitatusaidia.
Mhe. Mwenyekiti, wadau hawa ni vyema kushirikishwa katika masuala haya sijui mtachukua kwa ngazi gani, lakini watu wa *Airport*, yaani nilichokusudia ni Mamlaka ya Uwanja wa Ndege na Shirika la Bandari mtatafuta viongozi gani wa kuwahusisha, maana yake Bandarini pamoja na *Airport* ndizo sehemu wanazopita wageni. Kwa hivyo, tuone nao hawa tunawashirikisha katika suala hili.

Kwa kweli nimeusoma mswada huu haraka, hivyo sikua na michango mingi sana, isipokua ni kusisitiza tu kwamba Mhe. Mwenyekiti naomba sana katika suala zima la uwajibikaji kwenye Kamisheni hii tuweze kuona kwamba inapiga hatua, kwa yale manung'uniko, kero pamoja na zile kasoro.

Vile vile sivibaya Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti ikiwa tutakuwa tunapata taarifa ya kipindi kisichopungua miezi 6 baada ya kukutana labda awamu mbili ya hatua ya huko tulikotoka na zile kasoro tulizoziona na hata ikabidi tuweze kuunda Kamisheni na kufanya marekebisho ya Kamisheni hii iliopo sasa.

Kwa hivyo, sivibaya na sisi litatupa moyo hilo na kama kuna jengine ambalo tutaliona kwamba bado kuna kasoro na sisi kama viongozi, basi tunaweza kulichangia.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa taarifa nimesikia kwenye redio Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ameteuliwa kwenye Wizara nyengine, kwa hivyo ni vyema kumpongeza kwa nafasi nyengine aliyopewa na Mungu, Mungu amsaidie huko anakokwenda. *(Makofi)*

Baada ya hayo niseme kwamba naunga mkono marekebisho ya mswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kupata fursa ya kuzungumza machache kuhusiana na hoja iliopo mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi, pili nimpongeze Mhe. Waziri kwa kutuletea mswada huu. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, kama kuna kitu ambacho kinahitajika hapa Zanzibar kwa kipindi hiki basi ni mswada huu.

Nadhani ingekua vyema tukaletewa mswada mpya kabisa na sio wa kufanya marekebisho, kwa sababu kama kuna jambo ambalo Zanzibar hivi sasa linatutatiza au Wazanzibari linatuathiri basi ni hii Sekta ya Utalii Mhe. Mwenyekiti.

Sekta ya Utalii katika nchi yetu kwa kweli hivi sasa imekua ni mzigo kiasi ambacho naweza kusema umetufika shingoni. Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Utalii imekuwa ni mzigo kwa sababu kwanza ile mila, silka na maadili ya Wazanzibari tangu kuruhusu utalii katika nchi hii yameondoka kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Utalii inatufanya Wazanzibari kua watumwa, yaani tunatumwa na utalii hapa. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikisema katika kitabu chake cha *Neo-colonialism* kwamba katika kitu kibaya sana katika ulimwengu ni huu Ukoloni Mambo leo, yaani umo ndani ya nchi yako lakini unatumwa na huku ukiwa na uhuru wa bendera tu. *(Makofi)*

Sasa tumeruhusu utalii kiasi ambacho hivi sasa tunalo tatizo kubwa ndani ya nchi. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, nimesikia kwenye hotuba zake nyingi kwamba Tanzania haina dini, lakini Watanzania wanazo dini zao. Kwa kweli yeye alikua na dini yake tena alikua akiheshimu dini nyengine. Kwa hivyo, tokea kuingiza utalii katika nchi hii kwa kweli hata dini zetu Watanzania hazithaminiwi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa ni jambo la kawaida kupita barabarani mwezi wa Ramadhani na kuwaona watu wanavuta sigara, watu wanakwenda nusu uchi na hili ni tatizo. Kwa kweli awamu ya mwanzo na ya pili walijitahidi sana kuheshimu mila na silka za Kizanzibari, leo hivi sasa tunao Usalama, KMKM, JKU, KVZ, hapa kuna tatizo, kwa sababu hata sheria maana yake zinaruhusu mambo haya ya kupoteza maadili yetu, hali hii inasikitisha sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wakati wa awamu ya mwanzo tulikua hatuna KMKM, KVZ wala JKU tulikua na Valantia tu Sakabona hapa Unguja na Pemba Mtemamoto, lakini mtu alikua hathubutu kwenda nusu uchi, lakini leo vikosi vyote hivi vipo na wala hatuviftar. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kuja kwa mswada huu nadhani itakua ni ukombozi kwa Zanzibar. *(Makofi)*

Suala jengine ambalo linalowaathiri Wazanzibari ni lile ambalo amelizungumza Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kwamba kuingia kwa utalii kumeingiza wimbi la wageni, yaani tunanyanyasika ndani ya nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, leo Mzanzibari hapati ajira katika hoteli za kitalii japo kama anayo taaluma ile ya utalii na badala yake anapata mgeni, tunakaa sisi hapa kama watumwa ndani ya nchi yetu, yaani aibu. Kwa kweli kama ingekua naweza kuleta mswada Serikalini na wananchi wa Zanzibar wakafanya *vote* ya kutokua na imani na Sekta ya Utalii, basi ningefanya hivyo, ili kusudi Wazanzibari wakafanya maamuzi ya kukosa imani na utalii katika nchi hii. *(Makofi)*
Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha kuna Wakenya katika Hoteli ye *Neptune* asilimia 70 ya wafanyakazi mpaka wasafishaji vitanda, jamani Watumbatu kutoka Nungwi hawawezi kusafisha vitanda. Hivi Mpemba wa Vitongoji Umangani hawezi kusafisha kitanda, kwa kweli aibu na inasikitisha sana.

Kutokana na hali hiyo, nasema hivi kwa uchungu sana kwa sababu sisi tumefanyakazi kubwa ya kukomboa nchi hii. Kwa kweli mwaka 1964 tumefanyakazi kubwa ya kukomboa nchi hii na leo wanakuja Wakenya kututawala ndani ya nchi yetu. Vile vile wanakuja Wazungu kuteremsha maadili yetu na sisi tupo hivi hivi na wala hatuwezi kukubali. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sana kwa sababu vijana wetu wanyanyasika mahotelini. Kwa mfano, kijana wetu anavuliwa nguo ndani ya nchi yake. Kwa kweli laiti ingelikua mimi ninakauli katika nchi hii, basi ningewapiga *patration* wale wote ambao wanakwenda kinyume na maadili yetu, kwa sababu tayari tulishawahi kuwapiga *patration* sisi katika nchi hii wakati wa Rais wa Zanzibar Marehemu Mzee Abeid Amani Karume na watu kuondoka hapa, kwa nini sisi tushindwe jamani. Kwa hivyo, kama Marehemu Mzee Abeid Amani Karume ameweza kuwapiga watu *pat-ration*, kwa nini Serikali mnashindwa, basi laiti kama sisi *backbenchers* tunaongoza Serikali tungewapiga *patration*, yaani inasikitisha sana kwa sababu tunanyanyasika ndani ya nchi yetu. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wanawake wa Nungwi kwa kweli Mhe. Mwakilishi wa Nungwi alilia machozi katika semina ile, yaani wanawake wa Nungwi wananyang'anywa waume zao hivi hivi. Sasa kama tungekua na sheria inayowadhibiti wale kufanya biashara ya ukahaba wangenyang'anywa? Inasikitisha sana. *(Kicheko/Makofi)*

Nadhani Serikali ina hofu, yaani Serikali inaogopa wageni. Mhe. Mwenyekiti, katika ulimwengu kwa mujibu wa *Lenin* kuna utumwa wa aina mbili. Kwa mfano, kuna huu wa *slave and lord*, yaani wa bwana na mtwana na utumwa wa pili wa *slave of fear*, yaani utumwa wa hofu. Sasa kwa mujibu wa *Lenin* utumwa wa hofu ni mbaya zaidi kuliko huo wa bwana na mtwana.

Mhe. Mwenyekiti, *Lenin* alisema kwenye kitabu chake naomba kunukuu kidogo. "*The worst slavery in the world is slavery of fear*". Sasa leo Serikali mnatuachia vijana wetu wananyanyasika na mnawaachia akinamama wa Nungwi wananyanyaswa na Wakenya pale ni aibu. Kwa kweli sisi tumetofautiana sana na Watanganyika, kwa sababu uhuru wa nchi hii haukupatikana kwa maneno, wale wanawake wa Nungwi wazazi wao ndio mwaka 1964 waliohangaika kuleta Mapinduzi ya nchi hii, leo wananyanyaswa wale. *(Makofi)*
Mhe. Mwenyekiti, laiti kama Marehemu Mzee Abeid Amani Karume angekua hai basi naamini mambo haya yangekua yameshaondoka. Vile vile kuna watu wanakwenda uchi mwezi Mtukufu wa Ramadhani, Mhe. Mwenyekiti Mwenyezi Mungu anatuchukulia tu hizo swaumu zetu, lakini Mwezi Mtukufu wa Ramadhani watu wanakwenda uchi pale, inasikitisha Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, naishauri Serikali sisi katika miaka ya 1960 kulikua na Hoteli ya Bwawani na *Africa House* na zilitosha kabisa kuchukua wageni pamoja na mambo mengine. Sasa leo mnaleta utitiri wa mahoteli na kutuletea aibu katika nchi, badala ya kuifufua Hoteli ya Bwawani pamoja na mambo mengine, yaani inasikitisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri kwa sababu kwenye *Teaching Profession*, unaposomesha wanafunzi na ukaona kwa njia hii hawafahamu, yaani kwa njia ya *lecture*, basi unatakiwa wende kwa *discovery method* au kwa aina nyengine ya kufundishia.

Sasa ikiwa utalii njia hii ya uchumi imekua tatizo, basi nadhani tuachane nayo hii na twende kwenye njia nyengine ambayo itakua na maslahi zaidi na italinda maadili na Baraza hili tayari limeshamua mafuta yapo, lakini leo tunang'ang'ania utalii tu sisi na mafuta tunayo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuna muimbaji mmoja pale alikua muasisi wa Afro-Shirazi Part, mama mmoja alikua akipiga msondo pale kwa Mhe. Mohammed Aboud Mohammed Wawi anaitwa Binti Fihimu, alisema kwamba "hiki ni

chaso kulala na njaa na kitu tunacho", basi hiki ni chaso. Kwa kweli sisi tunahangaika bure kwenda kwenye utalii na huku Uislamu unaondoka, maadili yanavunjwa na wake zetu wananyang'anywa waume zao. Lakini mafuta yapo hapa na vyema tukaachana na utalii huu unaotunyanyasa tu Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli inasikitisha sana.

Kwa maana hiyo, tutafute *another alternative means* ya uchumi na tuachane kabisa na utalii. Mhe. Mwenyekiti, leo wawekezaji tunawagopa, yaani tunawaabudu. Kwa mfano, kuna sheria katika *Sand Beach*, yaani hizi *beach* za fukwe pajengwe mita 30 kutoka kwenye bahari na hiyo ndio sheria inavyosema na kwenye *Coral Beach* ni mita 10 kama sikosei. *(Makofi)*

Lakini leo hoteli za kitalii zimejengwa ndani ya bahari na sisi tunawatizama tu na kusema aaa! Inasikitisha tena ni aibu au fedheha mnaidhalilisha Serikali ya Mapinduzi Mhe. Mwenyekiti. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende kwenye vifungu katika kifungu cha 5(1) kuhusu Muundo wa Kamisheni. Kwa kweli hapa kwenye muundo wa Kamisheni naomba aingizwe Kamishna wa Polisi kwa sababu kuna manyago mengi yanafanyika kwenye Sekta ya Utalii. Kwa hivyo, aingizwe Kamishna wa Polisi Zanzibar, yaani awe Kamishna kwenye Kamisheni kama alivyoingizwa *OCD* katika Kamati za Wilaya, basi na hii ya kitaifa huyu Kamishna wa Polisi aingizwe Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Suala jengine kwa sababu tunataka kuona mambo ya maadili yanapatikana, yaani maadili yanakuwepo, basi lazima awe Kamishna mmoja kutoka Afisi ya Mufti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia kifungu cha 5(i) na (ii) wawepo wadau wa watalii, yaani Jumuia ya Watembezaji na Kusafirisha Watalii. Mhe. Mwenyekiti, hawa nadhani ni wamoja, yaani wadau wa Utalii na Watembezaji wa Watalii. Kwa hivyo, nafikiri iwekwe moja tu wadau wa watalii na hii Jumuia ya Watembezaji Watalii iondoshwe, kwa sababu tusitie utitiri wa makamishna. *(Kicheko/Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye kifungu cha 5(3) (1), Mhe. Mwenyekiti naomba kunukuu.

Kifungu cha 5(3) (i) kinaeleza hivi:-

(3) "Mtu hatoweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti mpaka awe:

(i) Na utaalamu wa pekee katika fani inayofafana na utalii, uongozi wa wadau wa utalii au uhusiano wa kimataifa".

Mhe. Mwenyekiti, hapa zimetajwa zile sifa tu, lakini hakikutajwa kiwango cha taaluma. Kwa mfano, awe na *degree* ya kwanza au stashahada tu ama cheti cha Mambo ya *International Relations*. Kwa hivyo, ni vyema ikatajwa hasa kwamba Mwenyekiti lazima awe na *degree* ya kwanza katika masuala ya utalii na wala tusiwe hivi.

Kifungu cha 5(3) (ii). Kwa kweli kifungu hiki ni bora kiondolewe haina maana yoyote, isipokua ni kuongeza maneno tu kwenye mswada huu. Kwa mfano, ujuzi wa kutosha wa kupigania mambo, sasa ni kupigania mambo gani. Kwa hivyo, kifungu hiki kiondoshwe hakifai, yaani kifutwe kabisa. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Wawi akiwemo Mhe. Mohammed Aboud Mohammed ambaye ni mpiga kura wangu, tunaunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima kwa kuweza kukutana jioni yetu ya leo, kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu ambayo tuliokujia katika Baraza hili tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kutoa maoni yangu machache katika mswada huu uliopo mbele yetu, ambao ni mswada muhimu kuhusu utalii na uliotuzunguka kwenye mazingira mengi ya nchi yetu ya Zanzibar.

Nianze mchango wangu katika mswada huu kwenye ukurasa wa 41 sehemu ya tafsiri. Mtalii, maana yake ni mtu ambaye yupo katika sehemu ambayo sio makaazi yake, lakini yupo kwa ajili ya kazi mapumziko au starehe. Mhe. Mwenyekiti, nadhani hakuna mtu hata mmoja mwenye kuupinga utalii, kwa kweli sote tunakubali kwamba utalii unatunufaisha.

Lakini kwanza mimi nina tatizo kidogo kuweka hili neno au starehe. Mhe. Mwenyekiti, starehe ina maana pana, nadhani hili ndilo linalotushughulisha sana. Kwa kweli mtalii yeyote atakayekuja hapa, basi hii hali ya starehe inatushughulisha hata kula ikiwa umekaa kwenye mkeka nyumbani kwako basi pia ni starehe. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, nafikiri ni vyema tuzidi kuitafuta maana nzuri ya utalii, hiki kitu starehe tu ndicho kilichonishughulisha, kwa sababu kitu starehe kina maana pana.

Mhe. Mwenyekiti, utalii baada ya kuja katika nchi yetu, basi matumaini yetu ni kufarajika na kuingiza mapato katika nchi yetu. Lakini kama tunavyosema mara nyingi kua utalii una faida na hasara. Kwa hivyo, ni kitu cha kutizama faida na hasara zake zikoje.

Kwa kweli anapoingia mtalii, matumaini yetu ni kwamba yale mapato tunayotarajia kuyapata. Kwa mfano, *Tax Holiday*, lakini utakuta mara nyingi kwamba tunapoteza hatuyapati, kwa sababu hata huyo mwekezaji anapokuja kuajiri tunatumai kua vijana wetu wapate ajira.

Mhe. Mwenyekiti, hivi juzi tulikua Mangapwani tuliona yule mwenye kugawa vitaula si Mzanzibari, yaani kule kugawa vitaula hata mimi nikipewa naweza kuchukua kile kitaula kwenye kisinia na kugawa, si Mzanzibari. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, ukifanya tathmini mara nyingi utahisi kwamba utalii mbona tunapoteza kwa mara nyingi na faida yake utaihisi ni ndogo tunayoipata sisi. Mhe. Mwenyekiti, nadhani tutizame vizuri na pengine marekebisho ya sheria ambayo tunaifanyia marekebisho, basi tutaisaidia.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nije kwenye kifungu cha 5 kinachoeleza kuhusu Muundo wa Kamisheni. Mhe. Mwenyekiti, kwenye Muundo wa Kamisheni naomba hawa makamishna wengine ambao watachaguliwa wasiozidi sita ningeliomba *Gender* izingatiwe, ili tuweke uwiano mzuri katika muundo huu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kwanza nashukuru sana kwa sheria hii, katika ukurasa wa 48 umeelezea juu ya kamati za utalii za wilaya, katika kamati hizi Mhe. Mwenyekiti, kuna sehemu ya (j) viongozi wa kidini katika Wilaya kwanza hapa natoa shukurani kwamba hawa viongozi wa kidini wameingizwa katika hizi kamati za Wilaya, lakini basi ninachokiona kwamba mara nyingi viongozi wa kidini wanakua hawapewi fursa nzuri.

Kwa sababu wanapokuja na maoni yao, na hawa wana sheria ambazo hazifutiki, sheria zao walizokua nazo ni sheria ambazo tayari zimeshafutwa wakati huo zilipokua mansuh, sasa hivi ni sheria ambazo zinafanya kazi kwa hivyo mara nyingi viongozi hawa mimi husema kwamba kama watu wanaoonekana wanakuja na kitu kipya wakati ambapo sio kitu kipya. Wanachokuja nacho wao ni Mwenyezi Mungu kasema nini Mtume katoa hadithi gani ndio wanachokuja nacho hawa.

Kwa hivyo mimi nimefarajika kuona kwamba hawa viongozi wa kidini wametiwa katika kamati hizi, basi nadhani yale matarajio yetu ya kuona utalii ambao tunao hivi sasa unakiuka maadili basi huenda tukapata manusura. Kwa kweli wageni wetu wanaokuja kwa utalii tuko katika hali mbaya baada ya kupata manufaa tumuombe Mwenyezi Mungu asije akatupa nakama, kwa sababu tutaona ni kitu cha mchezo lakini leo unamkuta mtu kavaa nguo hazikuridhisha.

Mhe. Mwenyekiti, juzi tuko Pwani Mchangani nashuka ngazi mimi nadhani wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wananijua wote ni wakwe zangu, unashuka ngazi unamkuta mtu Mkwe wangu pale Mhe. Saleh anaita mamkwee utanipa mwanao tunaona haya kutizamana uso na macho, hali kama ile mimi nadhani kwa kua tumefanya sheria nyepesi nyepesi lakini kama alivyosema Mhe. Saleh labda tunawaogopa kwa hivyo tunafika hadi leo sisi wenyewe Wazanzibari tunakwenda kukaa pahala kufanya mambo yetu basi wewe mwenyewe unaona haya na unashindwa. Kwa hivyo utalii kama huu mimi nadhani kama itapigwa tathmini basi bora iwe basi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine tunakuja majukumu ya kamati za utalii za Wilaya, inasema kulinda usalama na amani kwa wageni pia na hapa tunasema kwamba ndio kuweka Wazanzibar, lazima tuwape kipaumbele ndugu zetu wa Kizanzibari bado imani za Kizanzibari zipo, hivi karibuni Mhe. Mwenyekiti nadhani kama wiki mbili au wiki tatu nyuma Zanzibar Beach Resort palitokea wizi, wizi ule ulipotokea Mheshimiwa tayari baadhi ya ndugu zetu wa Kizanzibari waliokuwepo kwenye bustani walikua wameshakamatwa na kushtumiwa kwamba wao ndio wezi.

Lakini baada ya muda ikaja *taxi* kwenye mlango ikaleta bahasha ambayo ina vitu ambavyo vimeibiwa ndani baadhi yake vimerejeshwa, risiti, passport bahasha tu imeletwa ipelekeni mapokezi hakujulikana mwizi yule, dhahiri inaonekana kwamba hapa palikua na watu ambao ni wageni kinyume na hawa watu wa Zanzibar, kwa hivyo hii ni hali ya kua na mazingatio makubwa tuwape umbele watu wetu wa Zanzibar bado imani Zanzibar ipo usione mambo tu hivi sasa panaingia uharibifu kidogo kwa muingiliano uliopo na watu kutoka sehemu mbali mbali.

Mhe,. Mwenyekiti, jengine katika kifungu cha 23(3) mtu yoyote anayefanya biashara ya utalii aliyeajiriwa ndio ile ile tunarejea kwamba aliyeajiriwa kua sio mtanzania kutoa huduma iliyoelezwa chini ya kifungu cha kwanza, kifungu hiki lazima apate ruhusa ya maandishi. Pia kutokana na sheria hii yale manung'uniko na malalamiko ambayo yaliyokuwepo kwa muda mrefu juu ya uajiri basi nashukuru Mhe. Waziri pia na hapa paangaliwe vizuri, tujitahidi kama tunavyosema kwamba hebu tuone na sisi Wazanzibari tuna haki katika ajira hii.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wengi wameshachangia huu mswada ni mswada ambao una lengo la kuweka sheria nzuri kwa utalii wetu, lakini ile taarifa ambayo tuliipokea kwamba kuna mama ambaye amedhalilishwa akavuliwa nguo mimi niliumia katika nafsi yangu, kama ni mtoto wa kike na mimi ni mwanamke basi niliona uchungu kwamba alivuliwa mpaka nguo za ndani akadhalilishwa. Tunaomba aliyefanya kitendo hiki basi achukuliwe hatua ili tuone kwamba kudhalilishwa kwa mwanamke mmoja basi tunahisi tumedhalilishwa sote, ni kitendo ambacho kimetuuma sana na kitendo ambacho sio cha ubinaadam wala sio cha utu kilichofanyika. Tunaomba Serikali ichukue hatua kwa kitendo hiki kilichotokea ili kuona kwamba huu udhalilishaji hautotokea tena.
Lakini Mhe. Mwenyekiti, kuendelea kuachiwa kwa suala hili mimi nadhani utakua ni mchezo wa siku zote, kwasababu kwa kusema ukweli kuna udhalilishaji mkubwa katika mahoteli mbali yanayojulikana na kuna yasiyojulikana, Mhe. Waziri tunaomba suala hili ulifuatilie na tujue muhusika wa suala hili anachukuliwa hatua, leo wakati nakuja huku kuna mtoto anatokea Kusini alikuja mtoto wa kiume ambae anahusika na kutembeza watalii basi mtoto wa kiume lakini kahuzunika sana juu ya tokeo lililotokea. Alisikitika na aliumia katika nafasi juu ya kitendo hiki kilichotokea kwa hivyo wananchi wanasikiliza Serikali imechukua hatua gani juu ya suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi naunga mkono mswada huu mia kwa mia Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, lakini naomba radhi kwamba sitosimama na mimi nitazungumza machache katika mswada huu wa kurekebisha Sheria mama ya mswada huu. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri na niwapongeze wote watendaji wake na niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakuja kwenye utalii lakini sitokuja kwenye vifungu ila nitazungumza kidogo tu kama walivyozungumza wenzangu kwanza utalii na utamaduni kwa nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, utalii ndio chombo sasa hivi kinachotuingizia mapato katika nchi yetu lakini tuangalie na utamaduni wa nchi yetu Wazanzibari je, unaendana na watu hawa wanaokuja, Sheria zinapangwa vipi na katika haya marekebisho yatarekebishwa haya nitakayoyazungumza au kwa marekebisho mengine tu kwa kuvuta watalii kwa kua tutapata hizo pesa za kutumia katika nchi hii au vyenginevyo.

Mhe. Mwenyekiti, watalii wanavyoingia katika nchi Mila, Silka na utamaduni wa nchi hii kwa hakika haufuatwi kwa sababu hawa wenzetu wanapoingia katika nchi wanaingia wanavyotaka wao, sisi tunamuomba Mhe. Waziri pale uwanja wa ndege wanapoteremka basi pawe na kibao maalum wakifika waone, kua hapa mtu akiteremka anatakiwa avae hivi na desturi zake ziwe hivi. Kwa sababu tunadhalilika kikweli kweli kama walivyosema wenzangu, mimi mwenyewe nashuhudia mambo si mara moja wala mara mbili kwa watalii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilipanda ndege na wakati huo nilipopanda hiyo ndege nilikua na Mkuu wa Mkoa tukaingia nae katika ndege ile tuliyoingia tulibahatika tuliingia na wale tu na tulikua tunateremka hapa Unguja, lakini mimi mwenyewe kwa vile nilivyoingia na wenzangu Wazanzibari watatu mimi na Mkuu wa Mkoa na Mtoto mmoja ana

miaka kama ishirini au kumi na nane sikujisiki vizuri katika ile ndege na nilimwambia Mkuu wa Mkoa. Kama ningelikua najua kama naingia ndege hii na nitakutana na wenzetu hawa mimi ningeahirisha hiyo safari nikaja kesho, jinsi watu walivyoingia kwenye ndege nguo hawana na vile vitendo vilivyokuwemo mle kwenye ndege mimi havikunipendeza.

Mhe. Mkuu wa Mkoa kwa ubishi wake alinisogelea ananambia hujaona harusi kwenye ndege wewe utaiona leo, mimi sichanganyi nimeelekea chini kwa sababu nimekaa na mtoto mdogo ambae ni kijana nayale mambo mimi hayakuniridhisha tukafika Unguja tukateremka na wenzetu wengine wakateremka na wengine wakaendelea na safari nafikiri walikua wanateremka Pemba. Kwa hivyo ikiwa hapa pana marekebisho tunamuomba Mhe. Waziri pawe na marekebisho ya mila, silka na desturi za nchi hii kwa watu hawa watakapoingia katika nchi yetu, pawe na kibao maalum cha kueleza na hata nguo ziwekwe.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mara moja nilikua na Mwenyekiti wangu Mhe. Salmin Awadh katika kamati tukatoka tukenda kwenye matembezi yetu halafu ikabidi tuende hoteli mchana kula, sijui ilikua ndio Kiwengwa kule tulipofika wao wakafika mwanzo mimi nikachelewa kuteremka gari, pale ile hali iliyokuwepo mimi nilimuuliza Mwenyekiti mara tatu yule aliyelala pale mwanamke ananambia mwanamme, nikamuuliza tena mwanamke akanambia mwanamme yule. Mhe. Mwenyekiti kalala kwenye ufukwe pamewekwa kijitanda cha kibao pale watoto wa Kizanzibari wapo, watoto wengine wanaopita wapo kama alivyozaliwa mimi sikuweza kumtizama kwa sababu nilichanganyikiwa sikumjua mwanamke au mwanamme mara tatu namuuliza Mhe. Salmini Awadh ananambia mwanamme yule mwanamke analala vile ndivyo alivyonijibu.

Hii hali halisi ya nchi yetu tuweze kuilinda watu hawa waingie tupate kipato na watoto wetu wapate kazi na sisi vile vile tupate ustawi wa nchi hii, lakini na maadili ya nchi hii katika marekebisho haya pia Mhe. Waziri ayazingaatie, halafu mila na desturi za nchi hii ni kuvaa nguo na kusuka nywele na mambo mengine. Hata kupanda miti ya haiba wakaja kuiona kama miwardi na mambo mengine, lakini kuje tu wakafanya wanavyotaka itakua ni matatizo juu ya matatizo, kwa hivyo Mhe. Waziri tunakuomba, Mwenyezi Mungu akitujaalia mswada utapita lakini kwenye marekebisho yako mambo mengi ambayokuwa yanatudhalilisha Wazanzibari uweze kuyazingatia.

Halafu wanazuangumza wenzetu wanapoingia katika nchi wanaingia pengine kwa nia safi, lakini pengine wale waliokuwa wapo hapa waliokuwa wanamiliki yale mahoteli wao hawana nia njema, kwa sababu unakokwenda hoteli yoyote humkuati Mzanzibari yoyote aliyekuwa pale yupo angalau ana kazi ya kufagia fagia au kukuletea ile *tissue* kufutia mikono wote ni wenzetu kutoka nje, kweli jamani ndio tunaambiwa hatuna sifa ya masomo hata kuosha sufuria, kufagia, au kuosha nguo. Hili jambo linatudhalilisha tunaomba watoto wetu na sisi tujikomboa katika umasikini pia na hizi kazi zipatikane na wawekezaji wasiende kuchukua watu nnje tu kuingia hapa.

Mhe. Mwenyekiti, udhalailishaji mahoteli upo Mhe. Mtumwa amesema watu kuvuliwa nguo hata kulipwa haki zao hao Wazanzibari wapo tele waliokuwa wanakwenda pale na haki zao hawapati, ukenda pale ukimkuta mtoto wa Kizanzibari basi anavyoteseka basi wewe utaumia, tunaomba Mhe. Waziri katika masuala ya mahoteli uzingatie makini sana watu wa Zanzibari hii ni nchi yetu na ile ni mali yetu na ule ni uwekezaji wetu, wao wanakuja hapa kuwekeza lakini hawana chao ni chetu. Sasa chetu sisi kisiwe watu wanachukua tu, kwanza kinachoniuma ni wenzetu kupata *passport* kuingia nchi hii kwa wingi lakini ukitaka kuondoka wewe utamaliza miezi hapa *passport* hupati, lakini hii ndio hali halisi na tunawakaribisha sisi waje sasa je sie wakija hapa wanakuja kwa usalama, utamaduni wetu haupotei, silka zetu hazipotei ingawa tunaingiza pesa sisi hatuwafukuzi tunoamba waje lakini tunaomba sheria zizingatiwe kikamilifu jinsi ya wenzetu watakavoingia kaika nchi.

Mhe. Mwenyekiti, maadili ya nchi yetu yanapotea kwa kuiga, wanaiga kivazi, wanaiga miendo na hulka wanazofanya wale kila mtoto atakuwa yeye yuko tayari kwa watalii basi na yeye utamuona tu ameshabadilika. Kwa hivyo mswada unarekebishwa, huu wa marekebisho basi tunaomba na mambo yote yarekebishike ili tuweze kwenda vizuri katika nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti baada ya kusema hayo machache naunga mkono mswada huu mia kwa mia na *inshaalla* namuombea waziri upite mswada aweze kutufanyia mambo mazuri zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsanteni sana waheshimiwa wajumbe kwa namna tulivyoweza kushirikiana pamoja hadi kufikia wakati huu, kabla ya kuahirisha kikao hiki nina matangazo matatu.

Tangazao la kwanza ni kwamba Wawakilishi wote wa CCM wanaombwa mara baada ya kuahirishwa kikao hiki wao wabakie.

Tangazo jengine ambalo limetoka kwa Katibu wa Baraza la Wawakilishi yeye anaomba kwamba wajumbe wote wa Baraza mara tutakapomaliza kikao hiki pia na wao wabakie.

La tatu tulipokuwa tunakuja kwa ajili ya kuendelea na sehemu hii ya jioni tulikuwa tunatafakari sana mimi na katibu pamoja na baadhi ya makatibu waliokuwemo ndani, kwa kweli hali ilikuwa hairidhishi. Katibu alikuja ndani akakuta kuna wajumbe kumi tu pamoja na kwamba hakutokezea mjumbe ambae alikuja kuleta hoja wakati tunaendelea na taratibu zetu, lakini mjumbe yule alikuja katika njia ya kistaarabu na kunifahamisha kwamba vipi tunaendelea na utaratibu hali ya kuwa wajumbe wapo kidogo. Sasa tulizungumza tulipokuwa ndani tusaidiane basi ili tuweze kuja kwa wakati na shughuli zetu zisiweze kusita humu ndani.

Baada ya maelekezo hayo sasa nachukua fursa hii kuakhirisha Baraza hili hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 1.45 Usiku Baraza liliahirishwa hadi
tarehe 05/04/2012 Saa 3.00 Asubuhi)